# CHANGAMOTO ZA KUTAFSIRI USHAIRI “WIMBO WA LAWINO ” WA PAUL SOZIGWA

**BEATRICE ADONGO OKERE**

**Ripoti hii imewasilishwa katika Shule ya Mahafala kwa ajili ya Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**MEI 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi.............................. Tarehe.......................

**Beatrice Adongo Okere**

AM12/2305/09

**IDHINI**

Ripoti hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu sisi kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu Cha Egerton.

Sahihi........................... Tarehe...........................

**Prof. James Ogola Onyango**

Idara ya Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu Cha Laikipia

Sahihi............................. Tarehe...........................

**Prof. Furaha Chai**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu Cha Pwani

## SHUKRANI

Utafiti huu umeweza kukamilika kutokana na ushirikiano wa watu mbalimbali. Ningependa kuwashukuru wote walionipa msukumo na fadhili zilizonigusa katika kufanikisha utafiti wangu. Ni vigumu kumtaja kila mtu kwa jina lake, kwani ni wengi walionisaidia katika hatua mbalimbali za utafiti huu. Hata hivyo, nitawataja wachache kwa niaba ya wote. Namshukuru Mola kwa kunijalia afya na uwezo wa kupata shahada hii ya uzamili. Ameniongoza katika safari hii ndefu na kunijalia kutimiza ndoto yangu ya miaka mingi ya kupata shahada hii. Pia nashukuru tume ya kuwaajiri walimu TSC kwa kunipa nafasi na wakati niendeleze masomo yangu.

Natoa shukrani jazila kwa wasimamizi wangu Profesa Ogola na ProfesaChai kwa maelekezo na mashauri yao katika kipindi changu cha utafiti. Nawashukuru sana kwa juhudi zao ambazo zimeniwezesha kukamilisha utafiti huu.Nawashukuru kwa kuchukua muda wao kuisoma na kuihakiki ripoti yangu. Siwezi kusahau nasaha na mwongozo wao hasa pale nilipoonekana kukosa mwelekeo. Nayathamini sana maelekezi yao ambayo kwayo ndiyo sababu ya ufanisi wa kazi hii. Wazazi wangu wapendwa nawashukuru daima kwa mwongozo, upendo  na kunitia motisha wa kufanikisha utafiti wangu. Mungu awabariki sana kwa kunitia moyo, kuniombea na kunihimiza kukamilisha kazi hii.

Mwisho kabisa, shukrani kwa wanafunzi wenzangu, Kenneth Maina, Roselyne Kasuma na Janice Mutua kwa mchango wao wa mawazo ulionisaidia katika utafiti huu. Walinihimiza kuendelea na safari japo ilionekana kuwa ngumu. Nawashukuru kwa kunipa msukumo wa kuniwezesha kufanikisha kazi hii.

# ABSTRACT

Poetry texts are amongst many texts that are said to be challenging to translate. This research analysed the challenges in translating poetry in the book: *Wimbo wa Lawino,* by Paul Sozigwa (1975). The purpose of this research was first, to investigate the reasons behind the linguistic challenges when translating poetry in the above mentioned book. Secondly, the research also investigated how these linguistic challenges affect language use. Finally it investigated how the language use affect aesthetics in poetry, in the above mentioned book. The theories used were: The Linguistic theory and the Communication theory. The research design was descriptive analysis. The researcher analysed thirteen poems focusing on the linguistic challenges, language use and aesthetics. The source text was the English text: *Song of Lawino* by Okot P' Bitek who wrote *Wer Pa Lawino* in Acholi, laterhe translated it into English. The target text was the Kiswahili text: *Wimbo wa Lawino* written by Paul Sozigwa. The findings revealed that the translator succeeded in maintaining the form of the poem which was free verse. However, he failed to maintain the structure of verses, stanzas due to the variation of the three languages: Acholi, English and Kiswahili, mistranslation, overtranslation and undertranslation.

## IKISIRI

Matini za kishairi ni miongoni mwa matini ambazo zimesemekana kuwa tata kutafsiriwa kwa ufasaha. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza changamoto za kutafsiri ushairi wa: *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa (1975). Utafiti huu ulinuia kuchunguza sababu zilizopelekea kuwe na changamoto za kiisimu katika ushairi mfano wa: *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa. Kadhalika, tulichunguza jinsi changamoto hizi za kiisimu ziliathiri matumizi ya lugha, hivyo kupelekea kuwe na athari katika ujumi. Nadharia zilizotumiwa zilikuwa niza kiisimu na kimawasiliano.Muundo wa utafiti ulikuwa ni uchanganuzi wa kiuthamano. Mtafiti alichunguza mashairi kumi na tatu huku akiangazia masuala ya kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi.Matini chanzi ilikuwa kitabu cha Kiingereza: *Song of Lawino* cha Okot P' Bitek aliyeandika *Wer Pa Lawino* katika lugha ya Kiacholi. Matini lengwa ilikuwa kitabu cha Kiswahili: *Wimbo wa Lawino* cha Paul Sozigwa. Matokeo yalionyesha kuwa kwa kiasi fulani mtafsiri aliweza kudumisha umbo la shairi la matini chanzi ambao ulikuwa huru. Hata hivyo hakufaulu kudumisha miundo ya beti na mishororo kwa sababu za utofauti wa mifumo katika lugha mbili, kutotafsiri baadhi za istilahi, kutafsiri kupita kiasi cha haja na kutotafsiri kikamilifu baadhi ya istilahi zilizotumiwa katika matini chanzi.

# YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** .......... **ii**
**IDHINI** .......... **ii**
**SHUKRANI** .......... **iii**
**ABSTRACT** .......... **iv**
**IKISIRI** .......... **v**
**YALIYOMO** .......... **vi**
**SURA YA KWANZA:** .......... **1**
**UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Usuli wa Mada .......... 1
1.1.2 Wasifu wa Waandishi : Okot P' Bitek .......... 4
1.1.3 Paul Sozigwa .......... 6
1.1.4 Wimbo wa Lawino .......... 8
1.2 Suala la Utafiti .......... 10
1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 10
1.4 Maswali ya Utafiti .......... 10
1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 10
1.6 Upeo na Mipaka .......... 10
1.7 Maelezo Ya Istilahi .......... 11
**SURA YA PILI** .......... **12**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** .......... **12**
2.1 Utangulizi .......... 12
2.2.2 Tafsiri ya Ushairi .......... 18
2.2.3 Kipengee cha Kiisimu .......... 22
2.2.4 Kipengee cha matumizi ya lugha .......... 28
2.3 Misingi ya Nadharia .......... 36
2.4 kielelezo cha dhana .......... 43
**SURA YA TATU** .......... **44**
**MBINU ZA UTAFITI** .......... **44**
3.1 Utangulizi .......... 44
3.2 Muundo wa Utafiti .......... 44
3.3 Kikundi Lengwa .......... 45
3.4 Uteuzi wa Sampuli .......... 45
3.5Ukusanyaji wa Data .......... 45

3.6 Uchanganuzi wa Data ....................................................................................................46
**SURA YA NNE ...........................................................................................................50**
**UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DATA ..................................................................50**
4.1 Utangulizi....................................................................................................................50
4.2 Kubainisha Changamoto za Kiisimu ..........................................................................50
4.2.1 Kiwango cha sauti katika lugha husika...................................................................51
4.3 Kubainisha Changamoto za Matumizi ya Lugha........................................................76
4.3.1Tamathali za Usemi na Mbinu za Sanaa...................................................................77
4.3.2 Imani, thamani na taasisi...........................................................................................82
4.3.3 Misimu na majina .....................................................................................................83
4.3.5 Ekolojia: Flora na fauna............................................................................................85
4.4 Kubainisha Changamoto za Ujumi .............................................................................87
**SURA YATANO ............................................................................................................93**
**MUHTASARI,  HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....................................................93**
5.1 Utangulizi....................................................................................................................93
5.2 Muhtasari ....................................................................................................................93
5.2.1 Kubainisha Changamoto kiisimu.............................................................................94
5.2.2 Kubainisha Kubainisha Changamoto za matumizi ya lugha ...................................95
5.2.3KubainishaChangamoto zaUjumi .............................................................................95
5.3  Hitimisho....................................................................................................................96
**MAREJELEO ................................................................................................................98**
**KIAMBATISHO 1:Umbo .............................................................................................98**
**KIAMBATISHO 2:  Matini za Wimbo wa Lawino.......................................................112**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Kulingana na Enyaga (2019) kazi nyingi za tafsiri hudhamiria kuiboresha matini ikizingatia matatizo, makosa, dosari na athari zake katika fasihi. Naye Bhana (2014) alidokeza kuwa, hakuna bara ambalo linashinda Afrika katika kuzionea fahari lugha zao za kwanza. Jambo hili linapelekea kuleta changamoto katika tafsiri hasa katika nyanja ya biashara. Awali lugha kuu za Uingereza ndizo zilitumika. Hivi sasa serikali za nchi za Afrika zinahimiza matumizi ya lugha ya kwanza mathalan, Gambia ilipanga mikakati ya kufutilia mbali lugha ya Kiingereza na kupendekeza lugha ya Kiswahili. Hivyo basi pana haja ya kuwa na watafsiri wengi ili kukidhi mahitaji ya nchi.

Nao watafsiri wa Alphaomega (2012) walisema kuwa, idadi nyingi za lugha barani Afrika zimezua changamoto za kutafsiri kutokana na ukosefu wa kisawe cha kiisimu au uwezo wa kutafsiri kutoka lugha ya kiafrika hadi lugha nyingine. Watafsiri hawa waliendelea kusema kuwa ni vigumu kupata visawe vya istilahi za sayansi na kiteknolojia katika lugha za Kiafrika kwa mfano, "*clinical depression*," "*cloud computing*" na "*social media*." Istilahi hizi zilihitaji ufafanuzi wa kina ili zieleweke.

Waliendelea kudokeza kuwa watafsiri wa Afrika walihitaji kufahamu lugha nyingi na kuwasiliana na mataifa mbalimbali ili kuelewa mada mbalimbali. Hapa kulikuwa na pengo katika tafsiri. Watafsiri hao waliangazia taarifa kutoka *Shirika la Common Sense Advisory* katika ripoti yao yenye mada "*The Need for Translation in Africa"*ambapo walichunguza watafiri mia tatu sitini na nne kwa niaba ya shirika la *Watafsiri Wasio na Mipaka*. Kutokana na utafiti wao, asili mia tisini ya tafsiri husaidia waafrika kukumbana na changamoto za kimaisha. Asili mia sitini na tatu ya waliotafitiwa waliamini kuwa maelezo yaliyotafsiriwa yaliwasaidia wanajamii katika kuepukana na majanga kama vifo. Aidha, walidokeza umuhimu wa tafsiri katika maendeleo ya Afrika kwa kuwasaidia waafrika kuelewa masuala ya sheria yanayohusiana na haki, kuboresha afya, kuzuia majanga na migogoro ya kijamii au ya kikabila.

Katika makala ya kutathmini umuhimu wa tafsiri ya matini katika kuunda mitandao ya kilimwengu Andrews (2014) alidokeza kuwa ili kufanikisha tovuti ya kilimwengu lazima matini yako iwe na mvuto kote ulimwenguni.

Aliongeza kuwa mtu anaweza kuwa na tovuti inayopatikana ulimwenguni kote ila si watu wote waliweza kuisoma matini iliyo kwenye tovuti hiyo. Ni watu wachache ambao wangeweza kununua bidhaa kupitia tovuti ambazo hawaelewi matini yake kwa hofu ya kutapeliwa. Wengi walikuwa na imani na waliweza kununua bidhaa kutoka tovuti ambazo zimetafsiri matini zao kwa lugha zao za kiasili.

Kwa mujibu wa chapisho katika jarida la *Taus Review*,Andnesen (2015) alisema kuwa Afrika inajumuisha asili mia kumi na nne ya idadi ya watu duniani ambapo asili mia ishirini na nane huwa na matatizo ya kiafya katika mataifa ambayo asilia mia tatu tu ni madaktari na manesi. Katika muktadha huu maelezo kuhusu masuala ya kiafya ni muhimu sana ili kuokoa maisha. Alitoa mfano wa ugonjwa wa Ebola ambao umeenea katika nchi tatu ambazo zina jumla ya lugha asili tisini. Ilani kuhusu ugonjwa huu katika Kiingereza na Kifaransa huwafikia tu wachache. Mashirika ya kimataifa hayakutambua umuhimu wa kutafsiri ilani hizo katika lugha asili ili tahadhari hiyo iwafikie wengi. Kadhalika, watafsiri wengi wa nchi za Afrika hukabiliwa na changamoto katika kutafuta visawe vya istilahi vilivyo katika lugha kuu. Hii ni kwa sababu lugha nyingi za asili hazina kamusi au hazina tafsiri za istilahi za Kiingereza.

Kroulek (2016) alidokeza kuwa japo lugha ya Kiingereza inatambulika kote ulimwenguni palikuwa na haja ya kutafsiri lugha hii kwa sababu si kila mtu huzungumza lugha hii. Pia watu wengi hupendelea lugha zao za asili ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Aidha alisisitiza kuwa tafsiri husaidia katika kuendeleza uchumi duniani kwa kusambaza habari na dhana mbalimbali miongoni mwa tamaduni mbalimbali. Katika jarida la *Jalada* katika warsha iliyokuwa na mada: "*Jinsi ya kuchapisha fasihi ya waafrika katika lugha mbalimbali ikiwemo lugha za kiafrika"*,waandishi mbalimbali walijadiliana kuhusu kuchapisha fasihi zao katika lugha mbalimbali. Suala la ujumi lilijitokeza ambapo wengi waliona kuwa kulikuwa na athari ya ujumi kazi zao zilipotafsiriwa katika lugha nyingine. Katika warsha hii, mwandishi Renee (2016) alidokeza kuwa kulikuwa na sababu nyingi ziliwapelekea waandishi wengi wa kiafrika kutafsiri kazi zao. Baadhi yao walitafsiri ili kupata umaarufu mbali na kufanya kazi zao ziwafikie wengi. Aidha alidokeza kuwa tafsiri ilikuwa ni chombo cha kuwaunganissha waafrika.

Alitoa mifano ya kazi za waandishi maarufu kama vile Ahmadou Kouruma, Camara Laye na Chinua Achebe ambazo zilitafsiriwa na kuwaunganisha waafrika walipokuwa wakipigania uhuru.

Alihitimisha kwa kusema kuwa mengi yalifaa kufanywa katika tafsiri ili kazi za fasihi ziweze kuwafikia wengi. Hii ni kwa sababu hadithi nyingi hazikuwa zimetafsiriwa hivyo palikuwa na pengo.

Wrong (2017) alitoa maelezo kuhusu ualishi wa Ngugi wa Thiong'o kuhusu jinsi ya kubatilisha utabaka katika lugha. Ngugi alionyesha umuhimu wa tafsiri kama njia mojawapo ya kukuza lugha zenye tamaduni tofauti. Maendeleo ya tafsiri yametokana na sababu nyingi. Zile muhimu zaidi ni tatu: za kisiasa, za kitamaduni na kielimu. Katika uwanja wa elimu, maendeleo ya kiteknolojia yanajitokeza hususani tafsiri mashine.Uchunguzi wa hivi karibuni na wataalam ulijaribu kuonyesha ni kwa njia gani waafrika walivyochukulia lugha kuu za waingereza katika maandishi yao. Kulikuwa na kuchunguza mikakati iliyochukuliwa na waandishi walivyojihusisha na lugha hizo zilizolazimishwa kwao. Kwa maoni yake, mtazamo huu unaweza kuchukuliwa kuhakiki fasihi za waafrika kwa kuzingatia mtazamo wao kuhusu lugha kuu. Kulikuwa na waandishi kama vile Ngugi wa Thiong'o ambao walisusia kuandika kwa kutumia Kiingereza. Kwa upande mwingine, kulikuwa na wengine kama vile Achebe 1958 katika Mule (2002) waolijaribu kutafsiri kazi zao kutoka lugha za kiasili hadi Kiingereza.

Tetesi zilitokea kwamba tafsiri za mashairi ni jambo lililowezekana. Savory (1968: 75) alidokeza kuwa, "wafasiri wengi wanaonyesha kukubaliana katika jambo moja tu: kuwa kutafsiri ushairi ni zoezi lisilowezekana."(Katika Mwansoko, 2006: 54).Naye Fitts (1966: 33) alisema kuwa, "washairi wanapozungumzia kutafsiri ushairi, kwa kawaida huanza kuhitimisha kuwa hili ni zoezi lisilowezekana," kuna wafasiri ambao hutafsiri kwa kujaribu kutafuta visawe vya maneno kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa." (Katika Mwansoko, 2006: 54). Hali kadhalika, kulikuwa na wale ambao walikuwa waaminifu kwa matini chanzi hivi kwamba tafsiri ilikuwa ni ya moja kwa moja. Yaani, iwapo ulitaka kuwa mwaminifu kwa matini chanzi ulipotafsiri hukuwa na budi kupoteza urembo wa matini iliyotafsiriwa.Kadhalika, ulipojaribu kudumisha urembo wa matini iliyotafsiriwa ilikuwa ni dhahiri kuwa hungekuwa mwaminifu kwa matini chanzi.

Kutafsiri matini za kishairi kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili kulikuwa na changamoto nyingi. Utafiti huu ulinuia kuonyesha changamoto za kiisimu za kutafsiri matini za kishairi.

Changamoto hizi zililetwa na sifa za kiisimu za matini za kishairi na vilevile sifa zingine ambazo si za kiisimu. Lugha ya shairi ni lugha inayohusu lugha inayotumika katika mawasiliano.

Tafsiri za matini za kishairi pia ziliathiriwa na mambo mengine ambayo si ya kiisimu. Lugha ya kishairi hufungamana na historia, ukuaji na tamaduni za mfumo wa shairi. Mifumo ya kishairi huwa na upekee wa kijamii. Kila jamii huwa na mfumo tofauti wa kitamaduni, kijamii na kiisimu. Dhana za shairi, mila na desturi hutofautiana kutegemea jamii husika. Sheria ya taifa fulani huwa ni mfumo huru wa kisheria ulio na istilahi zake, dhana zake na kanuni zake za uainishaji. Mifumo hii hutofautiana kutoka taifa moja hadi nyingine. Jambo hili huzua changamoto wakati wa kutafsiri kutoka mfumo mmoja hadi mwingine. Awali, uaminifu katika matini chanzi ulichukuliwa kama mbinu mwafaka katika mchakato wa kutafsiri. Siku hizi marekebisho katika matini chanzi yalifanywa na wafasiri ili kukidhi mahitaji ya masuala ya kitamaduni, kiisimu, kijiografia, kihistoria, kiisimujamii na kisiasa za lugha mbalimbali.

Marekebisho haya yalifanywa kwa muwala hasa katika utanzu wa ushairi. Hii ni kwa sababumatini ya kishairi ilijikita katika ujumi na mhemko wa hali ya juu. Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu uliangazia changamoto za kiisimu, kiujumi na matumizi ya lugha katika kutafsiri kitabu: *Wimbo wa Lawino* cha  Paul sozigwa (1975). Kitabu hiki kilikuwa ni tafsiri ya kitabu: *Song of Lawino* cha Okot P’ Bitek (1972).

### 1.1.2 Wasifu wa Waandishi : Okot P’ Bitek

Kulingana na Heron (1984), Okotp’Bitek alizaliwa katika eneo la Gulu, kusini mwa Uganda katika mwaka wa 1931. Alisoma katika shule ya upili ya Gulu kisha akaelekea katika chuo cha Kings katika eneo la Budo. Mnamo 1952, alifanya kozi ya ualimu katika taasisi ya walimu kule Mbarara. Okot alifundisha Kiingereza na somo la Dini katika shule iitwayo Sir Samuel Baker karibu na eneo la Gulu. Wazazi wake walijulikana katika jumuiya ya waprotestanti, hivyo Okot alikuwa mkristo. Uraibu wake ulikuwa muziki hivyo, alikuwa ni kiongozi wa kwaya alikofundisha. Alikuwa anajihusisha na masuala ya siasa katika nyakati hizo. Kazi yake ya fasihi ilianza kule Budo na Mbarara alipoandika shairi lijulikanalo kama ‘*The Lost Spear*.’ Katika mwaka wa 1953, kule Mbarara, alichapisha riwaya ijulikanayo kama ‘*Lak Tar’* katika lugha ya Kiacholi.Uraibu mwingine wa Okot ulikuwa ni kandanda.

Tangu alipokuwa shuleni alicheza mchezo huu hata kufikia katika kushiriki katika vilabu mbalimbali, timu ya wilaya na timu ya kitaifa. Uraibu huu ndio uliomfanya kutalii katika maeneo ya magharibi mwa Uganda. Jambo hili lilimfanya atambue tamaduni za watu wa kabila lake. Kandanda ilimfanya apate kusafiri kule Uingereza mnamo 1958.

Okot alichukua nafasi hiyo kujiendeleza na masomo, hivyo alibaki humo kusoma. Alifanya kozi ya mwaka mmoja ya stashahada katika chuo kikuu cha Bristol. Aliendelea na shahada ya sheria katika chuo kikuu cha Aberstystwyth. Hapa ndipo Okot alipopoteza msimamo wake wa dini ya kikristo. Ni wakati huo huo ndipo alipoacha kujishughulisha na tamaduni za Kiingereza na akafanya utafiti zaidi katika tamaduni za waacholi. Alifanya hivi alipomaliza shahada yake katika sheria. Alifululiza hadi chuo kikuu cha Oxford ambapo alisoma shahada ya Fasihi na Anthropolojia. Ni hapa ndipo alipokolea katika masuala ya kiakademia na ushairi. Hapa ndipo alipoandika kitabu, "*African Religions in Western Scholarship*" kinachohusu migogoro ya tamaduni za kiafrika katika usomi wa Magharibi.

Alipata kwamba somo la Anthropolojia liliunga mkono suala la ukoloni. Hivyo kwa kiwango kikubwa alipatwa na changamoto za kutumia maumbo ya mashairi za kiafrika. Mnamo mwaka wa 1962, nchi  yake ilikuwa inajiandaa kupata uhuru, hivyo ilimbidi nyumbani ashirikiane na wananchi wenzake. Alijiunga na chama cha U.P.C. ambapo alikuwa na azma ya kuwania kiti cha uongozi lakini baadaye alibadilisha nia. Kule Uganda, alichukua nafasi ya kwenda nyanjani katika somo la fasihi. Alirudi Oxford. Utafiti wake ulijikita sana katika fasihi simulizi ya waacholi. Alimaliza tasnifu yake, '*Oral Literature and its Background among the Acoli and Lang'o'* katika mwaka wa 1964. Alirudi kufanya kazi kule Uganda. Kwanza, alifanya kazi kule Gulu katika chuo cha Makerere. Aliendelea na utafiti wake katika nyimbo za kitamaduni, hasa masuala ya kidini yaliyokuwa yanaelezwa katika nyimbo hizi. Alijihusisha pia na marafiki wake katika uundaji wa sherehe ya Gulu. Alikuwa mwigizaji, msimamizi, mwimbaji na mchezaji wa nyimbo za kitamaduni. Ni wakati huu ndipo alipoandika shairi la *'Wer Par Lawino'* ambalo lilikuwa shairi la kiacholi la '*Wimbo wa Lawino*.' Aliathiriwa na nyimbo katika utunzi wake.

Mnamo 1966 alihamia Kampala. Hapa alisisitiza uigizaji wa kitamaduni  badala ya kazi za kigeni katika Kituo cha Utamaduni cha Uganda. Aliunda kikundi cha wachezaji wa nyimbo za kitamaduni kilichojulikana kama *'The Heart beat of Africa.'* Baadaye alichaguliwa kuwa mkurugenzi katika Kituo cha Utamaduni cha Uganda. Alipanga sherehe ya kitamaduni ya siku nane kufuatana na sherehe za uhuru mnamo 1968.

Alipotoka Zambia alipata kwamba amefutwa kazi. Sababu ni kwamba ilisemekana kwamba alihakiki wanasiasa vikali katika shairi lake '*Song of Lawino*.' Baada ya hapo alihamia Kenya ambapo alifanya kazi katika chuo kikuu cha Nairobi, kwanza Kisumu halafu Nairobi. Katika mwaka wa 1975, alitunga mkusanyiko wa insha, '*Africa's Cultural Revolution*.'

Katika miaka ya 1974 na 1978, mkusanyiko wa nyimbo za kiacholi zilichapishwa katika, '*Horn of my Love'* na hadithi ya '*The Hare and The Hornbill*.' Katika vitabu vyake, Okot alijishughulisha na kusisitiza kwamba mataifa ya kiafrika yalifaa kujengwa katika misingi ya kiafrika na wala sio misingi ya Ulaya. Alirudi Uganda katika chuo kikuu cha Makerere kama Profesa wa uandishi wa kubuni. Hata hivyo, baada ya miezi mitano Okot aliaga dunia kutokana na ajali mbaya barabarani katika mwaka wa 1982.

### 1.1.3 Paul Sozigwa

Kwa mujibu wa Mbonea (2017) katika gazeti la Jicho la Arusha, tarehe 31 mei (2017) alirejelea mahojiano aliyokuwa nayo na Sozigwa. Sozigwa alisema kuwa alisoma nchini Uganda Chuo Kikuu cha Makerere mwaka 1953 hadi 1957. Baada ya kumaliza masomo yake alipewa ajira ya afisa wa wilaya ya Kisarawe alikozaliwa mwaka wa 1933. Alisema kuwa wakoloni waliamini kwamba kama msomi angewasaidia kupambana na TANU eneo alilozaliwa bila kujua Sozigwa alikuwa mwana TANU. Sozigwa alikata kadi ya TANU mwaka wa 1956 kwa vile wakati huo ukiwa mwanachama wa TANUhupati ufadhili wa masomo. Aliificha kadi hiyo kwa mwalimu aliyekuwa akifundisha shule ya Minakiambayo aliyosomea.

Alifanya kazi ya D.O Kisarawe vizuri na wakoloni walimtaka aondoke akafanye kazi kubwa zaidi ya propaganda. Kazi zote hizo alitauliwa na Gavana. Aliondoka Kisarawe kwenda Tanganyika Broadcasting Corporation (TBC) kuwa mtangazaji.Akiwa TBC iliyogharamiwa na Uingereza Sozigwa akiwa kiongozi wa Idhaa ya Kiswahili alifanikiwa kuinua hali ya utangazaji akiwa na wa wafanyakazi wakiwemo Suleiman Hega. Kwa bahati nzuri wakoloni hawakuwahi gundua ndani ya roho yake kuna TANU. Alichofanya redioni kwa faida ya chama chake yalikuwa ni makubwa Alitolea mfano wa mambo magumualiyofanya ni wakati Ian Smith alipotoa maelekezo ya kutangazwa kwa tukio la Rhodesia (Zimbabwe) kupata uhuru alizima redio kwa sababu alizojua yeye. Baada ya kuendelea na kazi alisema walimuamini hivyo walimpeleka masomo kusomea shahada ya mawasiliano mwaka mzima nchini Uingereza.Baada ya kurejea kutoka masomo aliteuliwa kuwa mkurugenzi mkuu wa TBC na kufanya kazi mpaka siku ya uhuru akiwa ndiye mtangazaji wa sherehe hizo.

Baada ya uhuru alionekana alifaa kusimamia nchi kwenye mambo ya propaganda. Mwalimu Julius Nyerere alimteua kuwa kuwa katibu mkuu, wizara ya Habari na Utangazaji. Alifanya kazi hiyo kwa miaka minne na kuifanya redio isikilizwe maeneo ya Afrika Mashariki. Katika mwendelezo huo mwalimu Nyerere aliamua kumchukua kuwa katibu wake wa rais akiwa na jukumu kubwa la kuuelezea ujamaa.Kila siku alitoa hadithi za ubunifu kuhusu makabila akaunganisha na ujamaa mpaka watanzania waliukubali huku wengine wakiwa hawauelewi lakini waliukubali. Katika kipindi hicho ndipo aligombea Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya MNEC, kisha kufanikiwa kuwa mjumbe wa kamati kuu. Akiwa ikulu alisema kulikuwa na utaratibu wa kufundishwa mazoezi ya mgambo kupitia maofisa wa jeshi na baadaye ndipo vita vya Iddi Amini vilipoanza Kagera. Alitumwa katika eneo hilo la propaganda ya vita. Paul Sozigwa alikuwa ni mwandishi kutoka nchi ya Tanzania.

Mbali na kuwa mwandishi yeye alikuwa pia ni mwanapropaganda mahiri wa Chama Cha Mapinduzi (C. C. M) na katibu wa waandishi wa habari katika afisi ya rais Julius Nyerere. Alikuwa katibu wa kwanza wa rais huyo. Nyadhifa nyingine alizoshika ni mkrugenzi wa kwanza wa Redio Tanzania (RTD), D.O wilaya ya Kisarawe katika serikali ya kikolioni na katibu mkuu, wizara ya Habari na Utangazaji. Vile vile alishawahi kushika nafasi mbalinbali ndani ya chama cha C.C.M. zikiwemo za mjumbe wa NEC,C,C. Na mwenyekiti Tume ya Taifa ya Udhibitina Nidhamu na mwenyekiti wa C.C.M. mkoa wa pwani.Miongoni mwa vitabu alivyotafsiri ni kama vile: *Wimbo wa Lawino:Ombolezo* cha Okot P'Bitek (1975), *Risasi Zianzapo Kuchanua*: *Mashairi ya Ukombozi kutoka Angola*, *Msumbiji na Guinea* cha Margaret Dickinson (1975) na *Mwalimu Julius Kambarage Nyerere* kilichoandikwa na William Edgett Smith(1977), Majukumu ya nchi za Kusini (1993).

Paul Sozigwa alifariki dunia mnamo Mei tarehe 12 mwaka wa 2017 alipokuwa akipata matibabu kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (J.K.C.I.). Mtoto wa mzee Sozigwa, mchungaji Moses Sozigwa alisema tatizo la kwanza lililokuwa likimsumbua baba yao ni kupoteza kumbukumbu. Baadaye ilikuja kubainika alikuwa na tatizo la moyo. Madaktari walisema moyo wake ulikuwa mkubwa. Kulingana na gazeti la mwanachi julai15 (2015), kulikuwa na mgogoro baina ya Sozigwa na mke wake Monica Kuga na walikuwa wameachana mnamo mwaka wa 1974. Walikuwa wamejaliwa watoto wanne: Salome, Irene, Ephata na Moses.

### 1.1.4 Wimbo wa Lawino

Kwa mujibu wa Orthofer (2015) shairi hili lilikuwa limeandikwa katika lugha ya Kiacholi yenye anwani *Wer Pa Lawino* (1966) na mwandishi Okot P'Bitek. Mwandishi yuyu huyu alikitafsiri katika lugha ya Kiingereza na alilipa anwani ya *Song of Lawino* (1972) na kulikuwa na utangulizi kutoka kwa Heron katika kitabu cha Song of Lawino (1972) Shairi hili lilitafsiriwa tena kwa lugha ya Kiingereza na Liyong (2001) na anwani ilikuwa *The Defence of Lawino*. Kulingana na wahakiki alijaribu kudumisha sitiari wenye muundo mfupi na beti huru.

Katika utangulizi, Heron katika kitabu cha Song of Lawino (1972) alibainisha kuwa *Wimbo wa Lawino* si nyimbo kwa sababu hazikuimbika; hazingeweza kulinganishwa na nyimbo za Kiacholi hazingeweza kuwa ndefu kiasi cha kufikia kuwa kitabu. Nyimbo za Kiacholi zilijumuisha ubeti mmoja au ikizidi beti mbili zilizorudiwa na zilizoambatanishwa na ala za kimuziki. Aidha, tafsiri ya Kiingereza haikuwa na utoshelezi wa vina na mizani kama ilivyokuwa katika *Wer Pa Lawino*. Shairi hili lilikuwa Ombolezo kuhusu hisia za mwanamke mmoja mu-Acholi (Lawino) kuhusu ukengeushi wa mumewe (Ocol). Okot alimulika hali ya wananchi wa Uganda ambao wengine waliiga tamaduni za kizungu ilhali wengine walithamini mila na tamaduni zao.

Kulikuwa na mgogoro kati ya makundi mawili: Ocol aliwakilisha vikaragosi wa nchi za magharibi na mkewe aliwakilisha wenyeji ambao walibaki kuthamini mila na desturi za waacholi.Kila mara Ocol aliikashifu mienendo na tamaduni za waacholi kwa mfano, Ocol alimkashifu mkewe kila mara kwa kushikilia tamaduni za jamii yake. Wakati huo huo, mkewe alipambana kudumisha mila na desturi za jamii yake. Hata hivyo, Ocol alimpendelea mwanamke mwingine aliyekuwa amekengeuka kama yeye (Clementine). Hapa Okot alionyesha kwamba wale ambao walikuwa na mielekeo sawa ya maisha waliweza kuishi pamoja. Okot pia alikuwa anatuma ujumbe kwa wenzake ambao walitupilia mbali tamaduni zao na badala yake kuenzi tamaduni za kimagharibi.

Tulipopiga darubini mandhari ya hadithi, kule Uganda tulipata kwamba waacholi walikuwa wakishiriki katika kazi ya kuchunga ng'onbe na ukulima. Walikuwa wakiishi katika maisha ya mitala. Wakoloni waingereza walipofika nchini Uganda.katika miaka ya 1890 waliathiri pakubwa hali ya kijamii na kitamaduni ya waacholi. Wengine waliingizwa katika dini ya ukristo kama njia mojawapo ya kuendeleza ukoloni.

Viongozi wapya walichaguliwa na waingereza. Viongozi hawa walipata kukengeushwa kama Ocol. Waacholi walilazimishwa kupanda kahawa na pamba. Nyakati hizo, walinyanyaswa na wakoloni. Katika miaka ya 1960 baada ya uhuru athari za ukoloni zilipata kuonekana. Kulikuwa na kikundi cha waafrika waprotestanti ambao walisomeshwa na waingereza ili wachukue nyadfa za uongozi nchini humo.

Waafrika hao nao waliwakandamiza waafrika wenzao ambao walikuwa wameshikilia mila na desturi za jamii yao. Wakati huo nchi nyingi za kiafrika zilichukua mfumo wa kibepari. Matokeo yake yalikuwa ni udikteta. Okot alikuwa mmojawapo wa wasomi wa kiafrika ambao walipendekeza kuwa badala ya watu kukengeushwa walifaa wazienzi mila na tamaduni za jamii yao. Alikashifu ufundishaji wa kazi za magharibi katika vyuo vya Afrika.Kulikuwa na mada za ubishi katika kitabu cha *WimbowaLawino*. Mada hizi ziliangazia ukweli wa mambo nchini Uganda baada ya wakoloni hao kufika. Kwa mfano, Ocol anamchukulia Lawino kuwa mjinga kwa sababu hangeweza kucheza gitaa na alimchukulia mama mkwe wake kama mchawi.

Kulikuwa na sehemu ambazo zilionyesha Lawino akizienzi mila na tamaduni za jamii yake mifano ni ndoa, upishi na densi. Lawino alichukulia dansi za wazungu zilikiuka maadili kwani watu wa jamaa moja walishikana. Ocol kwa upande wake alionelea kuwa densi za waacholi zilikiuka maadili kwani wachezaji walikuwa uchi. Kwa mujibu wa Lawino, mitindo ya kizungu kuhusu urembo iliwafaa wazungu kuliko waafrika. Jambo hili lilikuwa ni tofauti na Ocol ambaye alimkejeli Lawino kwa kusalia kuwa mtamaduni. Ocol alithamini pesa zaidi na katu hakutaka kupoteza muda wake. Lawino kwa upande wake hakuthamini saa za wazungu. Aliamini kwamba waacholi waliweza kutekeleza majukumu yao bila kutumia saa ya kizungu.Suti za kizungu kwa mujibu wa Lawino zilionyesha hali ya kudhoofika kiafya.

Kadhalika, kulingana naye waacholi waliheshimu sherehe ya mazishi zaidi ikilinganishwa na wazungu. Lawino alizidi kuwakosoa wanawake waafrika waliotumia vipodozi na nywele bandia. Katika suala la uhuru, Lawino alishangazwa ni kwa vipi nchi ingekuwa huru na Ocol hangeweza kusikilizana na nduguye. Kuhusu mambo ya dini Lawino aliwakashifu mapadre ambao mienendo yao ilikiuka kanuni za dini. Lawino aliendelea kupendekeza dawa za kiacholi kuwa bora zikilinganishwa na za kizungu. Shairi lilifikia kikomo huku Lawino akiomba amani katika familia na katika jamii yake. Hata baaada ya kudhihakiwa na mumewe alizidi kuonyesha upendo na uaminifu kwake.

**1.2 Suala la Utafiti**

Imekisiwa kwamba, tafsiri zinazofanywa katika lugha ya Kiswahili zimevia. Utafiti huu ulichochewa na pengo za changamoto za kiisimu, matumizi ya lugha na isimu katika utafsiri wa *WimbowaLawino*, pengo ambalo halijajazwa. Utafiti huu ulinuia kuchunguza sababu zilizopelekea kuwe na changamoto za kiisimu, za kiujumi na za matumizi ya lugha katika kutafsiri ushairi wa *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa, tafsiri ya kitabu cha: *Song of Lawino* cha Okot P' Bitek.

**1.3 Madhumuni ya Utafiti**

i. Kubainisha kwa kutolea mifano changamoto za kiisimu zilizojitokeza katika ushairi wa: *WimbowaLawino*wa Paul Sozigwa.

ii. Kuonyesha jinsi changamoto za kiisimu zilivyoathiri matumizi ya lugha katika kutafsiri ushairi wa: *WimbowaLawino* wa Paul Sozigwa.

iii. Kufafanua jinsi matumizi ya lugha yaliathiri ujumi katika ushairi wa: *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

i. Kuna changamoto gani za kiisimu katika kutafsiri ushairiwa: *WimbowaLawino* wa Paul Sozigwa?

ii. Changamoto za kiisimu ziliathiriaje matumizi ya lugha katika kutafsiri ushairi wa: *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa?

iii. Matumizi ya lugha yaliathiriaje ujumikatika kutafsiri ushairiwa: *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yalinuia kuliendeleza stadi za lugha ya kiafrika (Kiswahili) kwa kuilinganisha na lugha ya Kiingereza hivyo kuchangia katika dhana ya utandarithi. Aidha, utafiti huu uliwanufaisha wasomi wanaotafiti kwa kutumia nadharia ya mseto ya kiisimu na mawasiliano.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti ulijikita katika kuonyesha changamoto za kutafsiri matini za kishairi .Utafiti uliangazia namna mtunzi alivyotafsiri mashairi kwa kuegemea kwa maswala ya kiisimu, ujumi na matumizi ya lugha.

Kazi hii ilijikita katika nadharia za kiisimu na mawasiliano ambapo katika isimu, viwango vya fonetiki, fonolojia, mofolojia na uchanganuzi wa sintaksia viliangaziwa.Yaani, uchanganuzi wa sauti za lugha mbili husika, uchanganuzi wa mifumo ya sauti za lugha mbili husika, uchanganuzi linganuzi na sintaksia katika lugha mbili husika. Katika nadharia ya mawasiliano, uhuru wa mfasiri pia uliangaziwa. Hapa maswala ya jazanda, nahau, sitiari na tamathali nyinginezo za usemi yaligusiwa. Hii ilikuwa ni pamoja na masuala ya kiisimu na kiujumi na jinsi yalivyoathiriana. Pia udhaifu wa mtafiti uliangazziwa. Utafiti huu ulizingatia kitabu cha Paul Sozigwa, *Wimbo wa Lawino* (1975) ambacho kilikuwa ni tafsiri ya kitabu cha Okot P' Bitek, *Song of Lawino* (1972).

### 1.7 Maelezo Ya Istilahi

*Anafora:*Hii ilikuwa ni mbinu ya kibalagha au kiusemi ambayo ilihusisha Kurudianeno au kundi la maneno katika vishazi au sentensi zinazofuatana. Katika shairi, urudiaji huwa katika sehemu za mwanzo mwanzo za Mishororo.Maneno haya yalikuza nia ya mshororo uliohusika pamoja na Muundo mzima wa tungo.

*Mita:* Mapigo au mizani

*Tafsiri:* Habari iliyohamishwa kutoka lugha chanzi na kuingizwa katika lugha Lengwa kwakutumia maneno ya lugha lengwa.

*Tafsiri ya neno kwa neno:* Hii ilikuwa ni tafsiri ya moja kwa moja kwakutumia. Mapangilio wa mofimu ya matini chanzi kubakiavilevile bila kujali muktadha.

*Tafsiri sisisi:* Hii ilikuwa tafsiri ambapo maneno yalifasiriwa pwekepweke lakini kulikuwa na kufuata mfumo wa kisarufi wa lugha lengwa.

*Tafsiri ya kisemantiki:* Hii ilikuwa ni tafsiri iliyoegemea kwenye lugha chanzi, yaani mwandishi.

*Tafsiri ya kimawasiliano:* Tafsiri hii ilimlenga msomaji kwa kutilia maanani tamaduni ya matini lengwa.

*Tafsiri ya kifonemia:* Sauti za lugha chanzi ziliundwa katika lugha lengwa na wakati huo huo maana ilihamishwa

*Tafsiri ya kimita:* Tafsiri hii ilisisitiza utoaji wa mahadhi ya kimuziki asili katika lugha lengwa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Walsh (2017) alisema kuwa,tafsiri ni kama sanaa inayohitaji wakati, jitihada, mazoezi ufahamu na tajriba. Tafsiri hulaumiwa kwa wingi wa kasoro zake kuliko kusifiwa kwa faida zake.Kutokana na kaida hii, ungetarajia watafsiri wafe moyo na kujitenga na shughuli za tafsiri. Hata hivyo, wameendelea kujitahidi kutafsiri zaidi.Katika sura hii ujumla na upekee wa tafsiri za kishairi ulichunguzwa. Kwanza tuliangalia mambo ya kijumla ya tafsiri. Mambo haya yalikuwa ni pamoja na; fasili ya ushairi, mashairi ya Kiswahili na tafsiri ya ushairi. Pili tuliangalia kipengee cha kiisimu kwa jumla, kipengee cha matumizi ya lugha na kipengee cha Ujumi. Tatu tulishughulikia misingi ya nadharia.

## 2.2 Fasili ya Ushairi

Flanagan (2018) alidokeza kuwa kuna fasili nyingi za ushairi sawia na washairi. Alisema ushairi ni ule unaotumia lugha ya sanaa kama vile sanaa ya marumaru; rangi iliyotapanyika kwenye turubai ya kuchorea lakini hapa mshairi hutumia maneno badala ya rangina turubai ya kuchorea ni hadhira. Nastasi (2013) katika makala kuhusu maana ya ushairi aliwanukuu washairi 20 walioeleza dhana ya ushairi. Fasili za ushairi zilikuwa kama vile:- " Ushairi ni rekodi ya wakati mzuri zaidi na wakati mzuri na kumbukumbu nzuri zaidi. Ni kioo kinachofanya kilichopotoshwa kuwa kizuri" na "Ni hisia za kubuni."

Troolin (2015) alieleza kuwa ili kuelewa ushairi lazima uangazie umbo na matini. Ili kuelewa matini ni vyema kutilia mkazo vipengee fulani kama vile:- anwani ya shairi, maudhui, toni, uteuzi wa maneno, mangilio wa maneno, tamathali za usemi, na sitiari. Umbo lashairi ulihusisha mkao wa nje na sauti zinazotumika. Donovan (2017) alidokeza kuwa utata katika mashairi nikuwa shairi moja yaweza kuwa na fasili zaidi ya moja kwa sababu ya matumizi ya sitiari, alama za kuakifisha na kuacha nafasi katika mishororo.

Adungo (2018) tarehe 30. Mwezi wa Mei, katika makala yake yenye mada "*Fasili mbalimbali za Dhana* '*Shairi'* " alimnukuu Gituma (2010) aliyemnukuu Abedi (1954: 1) katika kitabu chake "*Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani za Amri*" aliyesema kuwa shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lughaya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoelezea wazi kuhusu mawazo, hisi au tukio kuhusu maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala na muwala maalumu uliosheheni kanuni za utunzi wa mashairi.

Shairi ni tungo linalotiririsha taswira, mawazo na ujumbe kwa lugha nzito ya mkato, yenye mnato wa maana. Umbo la shairi hurejelea idadi ya beti zake. Hata hivyo, kila ubeti unafaa kuwasilisha ujumbe kamilifu unaowiana na maana ya shairi nzima.Fasili hii iliegemea upande wa wanamapokeo.

Maana ya ushairi kulingana na mawazo ya wanamapokeo wengine kama vile Shaaban Robert katika Massamba (1983: 55) anasema: Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Mwauliza wimbo, shairi na tenzi ni nini? Wimbo ni shairi ndogo, ushairi ni wimbo mkubwa na utenzi ni upeo wa ushairi. Mwauliza tena kina na ufasaha huweza kuwa nini? Kina ni mlingano wa sauti za herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti, na ufasaha ni uzuri wa lugha. Mawazo maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa shairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.

Naye abdilatifu Abdalla katika (Massamba 1983: 57) anasema kuwau Maatungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote bali ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye, wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyoofu, tamu na laini. Kutokana na maelezo ya waandishi hawa ushairi ni utungo wenye mpangilio fulani na wenye mahadhi ya kimuziki. Hapa kuliuwa na kanuni fulani ambazo zilizingatiwa. Wanamamboleo kama vile Mwai (1988: 5) walionesha kuwa washairi wa kisasa wanaeleza kuwa fasihi hubadilika katika umbo na maudhui na kwa hiyo ushairi wa Kiswahili sharti uruhusu mabadiliko yanayotokea katika ushairi huru.

Lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kusema, tumbuizi kwa masikio ya kuusikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ilivyokusudiwa (Mwai, 1988:44). Kutokana na maenezi ya lugha ya Kiswahili kutoka pwani ya Afrika Mashariki hadi bara, ushairi wa Kiswahili umeweza kuenea na kupata umaarufu miongoni mwa jamii za Afrika Mashariki. Kwa hivyo, watunzi wa ushairi wameweza kutunga tungo zao zinazoshirikisha utamaduni mpana wa Afrika Mashariki kutokana na umaarufu wa maenezi ya lugha ya Kiswahili (Babusa, 2005; Chacha, 1987).

Kwa mujibu wa Wamitila (2010) anasema ushairi ni sanaa inayotambulishwa na mpangilio maalumu wa sentensi au vifungu, mpangilio ambao una mdundo maalumu au ruwaza fulani inayounda wizani, lugha ya mkato na mafumbo pamoja na mpangilio usio wa kawaida wa vifungu fulani.

Ndumaro (2013) tarehe 20 mwezi wa Septemba katika makala yake ya " *Dhana na Dhima ya Ushairi wa Kiswahili*" aliwanukuu wataalam mbalimbali walioeleza maana ya ushairi. Wataalam hawa walisema kuwa ushairi lazima uguse hisi, lazima umsisimue yule anayeusema, kusoma na kuimba na yule ausikilizaye. Mayoka (1984: 3) alisema, "Ushairi ni mtungo wa kisanaa ulio na mpangilio maalum na lugha ya mkato ambayo ndani yake una vina, urari wa mizani na muwala maalum ambavyo kwa pamoja huwa na fani na maudhui yahusuyo hisia fulani au tukio juu ya maisha mtu au watu wa mazingira na wakati maalum." Hapa mtazamo wa Mayoka ulishabihiana na ule wa Wangari na Massamba ila alidokeza dhana ya fani na maudhui yaliyotumiwa kupasha ujumbe kumhusu mtu fulani katika mandhari na kipindi mahususi.

Kaviti (2005) alichunguza makosa ya kisintaksia yaliyojitokeza kwenye tafsiri za Makala magazetini. Alitumia nadharia ya tafsiri mawasiliano kwenye utafiti wake. Alionyesha upungufu uliopo kwenye makala zilizotafsiriwa. Alisisitiza umuhimu wa kusawazisha sintaksia ndipo maana ya ujumbe asilia umfikie msomaji. Hili lilitekelezwa kwa kutumia miundo ya kisintaksia inayokubalika. Alishauri kuwa muundo wa sentensi wa LL uongoze tafsiri.Alishughulikia vipengele kama vile virai, vishazi, dhamira na toni, njeo na hali. Kaviti alishughulikia tafsiri kwa kuzingatia vipengele vya kisint.

Kulingana na Flanagan (2018) Wordsworth alieleza ushairi kama,"Mafuriko ya hiari za hisia zenye nguvu." Flanagan pia alimnukuu Dickinson aliyesema, "Iwapo nitasoma kitabu na nihisi baridi katika mwili wangu, hakuna moto ambao unaweza kunifanya nihisi joto basi nitatambua kuwa huo ni ushairi" Waandishi hawa walitilia mkazo hisia zilizotokana na maneno aliyotumia mshairi.Kulingana na wanausasa, ushairi ulikuwa ni chombo huru ambao uliweza au haukuweza kuwakilisha dunia halisia lakini, uliumbwa katika lugha iliyobainishwa na mtandao wake tata wa marejeleo.Waliokuja baada ya wanausasa walitazama mashairi kama yalitumia nahau za kisasa na ambazo zilizojitosheleza.

Babusa (2005) aliyaainisha mashairi ya Kiswahili kimaudhui na pia kudhihirisha kwa kiwango fulani kuwa, kipengele cha muundo kiliweza kutumiwa katika uainishaji wa mashairi hayo. Kwa kuzingatia kipengele cha muundo, Babusa alibainisha sura mbalimbali zilizoibuka na aliyaweka mashairi hayo katika maumbo au bahari mbalimbali za ushairi. Kulingana na bahari hizo ni kwamba, ushairi wa Kiswahili unawakilishwa kwa miundo maalumu ya lugha kama vile uzingativu wa msamiati teule, sajili za lugha na lahaja. Hata hivyo, kilichobainika katika maelezo ya Babusa ni kwamba, umbo au muundo katika ushairi wa Kiswahili ulijibainisha zaidi kupitia kwa  uwasilishaji.

Kutokana fasili zilizotajwa hapo juu ni dhahiri kwamba, ushairi ulitekeleza majukumu ya sanaa. Yaani, uliwakilisha dhana ya dunia halisi, kupitia lugha yenye mvuto ili kusawiri au kuakisi uyakini wa maisha.Kulikuwa na matumizi ya mbinu kadhaa ili kutimiza malengo ya washairi katika kueleza maudhui. Hii ilikuwa ni pamoja na matumizi ya mbinu ya lugha na sanaa, toni, wizani, vina, ukiukaji wa kanuni za utunzi na mahadhi ya kimuziki kupitia mizani yenye kiimbo.

### 2.2.1 Mashairi ya Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili ulitokana na ushairi wa Kiarabu. Mashairi ya jadi yalinuiwa kuimbwa sio kusomwa tu.Kwa mujibu wa Donavan (2009) katika makala yake kuhusu mtazamo was ushairi wa Kiswahili, ufanifu wa mshairi ulitegemea uwezo wake wa kukidhi mahitaji ya jamii yake. Ili kutekeleza jukumu hili lazima ajihusishe na muktadha wake. Mshairi hutegemea matumizi ya tamathali za usemi ili hadhira yake ipate kuelewa ujumbe wake. Hata hivyo anapotumia tamathali hizi za usemi ikiwa ni pamoja na sitiari ujumbe huwa na maana fiche hivyo uelewaji utategemea hali ya kijamii na kisiasa ya jamii husika. Katika jamii ya waswahili wengi hujizatiti kutumia lugha kisanii na aghalabu wazungumzaji wengi huhukumiwa kutokana na umahiri wao wa kiisimu.

Aliendelea kudokeza kuwa wasomi wengi ambao si waswahili huchukulia ushairi wa Kiswahili kama ule “usiopendeza.” Ni muhimu kutambua kuwa majukumu ya ushairi wa Kiswahili sio wa umbuji tu bali ni kutekeleza majukumu mengine. Alisisitiza kuwa mashairi ya Kiswahili yawe ya kiarudhi au huru yaliweza kuchangia suala la ujumi. Wasomi hao walichukulia mashairi haya kuwa ya “kitamaduni’ na muundo wake wa “kikabila” au “asili”. Hali halisi ni kuwa mashairi ya Kiswahili yana majukumu ya kisasa. Aidha alisema kuwa katika mashairi ya Kiswahili umbo na matini huwa ni muhimu sana.

Hivyo basi mashairi anafaa azingatie vigezo fulani vya muundo ili kazi yake ionekane kuwa ya hali ya juu. Kupitia mitandao kumekuwa na mashairi mengi kutoka kwa washairi chipukizi. Hata hivyo, inasemekana kuwa mashairi mengi yanayochapishwa magazetini huwa ni chapwa kwa vile washairi hutilia mkazo sifa za arudhi badala ya matini yenye umantiki. Aliendelea kusema kuwa mashairi huru yamekuwa maarufu sana japo yamepingwa vikali na washairi wa Kiswahili ambao huchulia kwamba mashairi haya hupoteza dhana ya ujumi na yanatokana na athari za usomaji wa kigeni. Mjadala ulikuwa ungali ukiendelea hadi wa sasa.

Roy (2014) katika tasnifu yake kuhusu ushairi wa Kiswahili kuanzia karne ya 16 mpaka karne ya 20 alipochunguza nadharia kuhusu arudhi na bahari za kiashairi alionyesha maendeleo ya ushairi wa Kiswahili yalifuata mageuzo ya lugha ya Kiswahili. Kulingana naye istilahi nyingi za ushairi zilitokana na maneno ya kiarabu mathalan, arudhi, bahari, diwani, kina , mizani, shairi na ubeti. Akiwanukuu (Abedi,1954; Shariff,1988; King'ei, et al, 2001; Roy, 2013) alidokeza kuwa ubeti wa Kiswahili uliundwa na misingi minne: vina, mizani, mishororo na vipande. Aidha aliangazia bahari za mashairi kutokana na msingi. Hapa mashairi ya Kiswahili yaliainishwa kulingana na idadi ya mishororo kwa kila ubeti, vipande, vina na mizani.

Renatus (2017) katika makala yake " *Dhana ya Ushairi kama Ilivyofafanuliwa na Wataalamu Mbalimbali*"alisema kuwa utanzu wa ushairi uliwasilishwa kwa lugha ya maandishi au lugha ya masimulizi ulikuwa na mchango mkubwa katika kunufaisha au kustawwisha maisha ya binadamu kwa kuelimisha, kumsisimua, kutunza na kuendeleza lugha yake kama moja kati ya vipengee muhimu maishani mwake. Alimnukuu Mulokozi (1982) ambaye aliainisha ushairi wa Kiswahili katika tanzu mbalimbali kwamba, zipo kumbo kuu tatu ambazo ni ushairi wa kijadi, ushairi huru na ushairi wa kimaigizo. Aliwanukuu wataalam kama vile Mnyapala (1965), Shaban Robert (1958) pia wanamapinduzi na Kahigi (1982) pamoja na Topan (1974) ambao walilisitiza kuwa ushairi ni lazima uilenge jamii kwa kuibua hisia za jamii hiyo husika. Kulingana na wanausasa na wanamapinduzi hao ushairi ulitumia lugha maneno ambayo ni fasaha. Wataalam walioweza kuthibitisha kauli hii ni kama vile mwanamapinduzi Kezilahabi ambaye alisema ushairi huwa na uzuri wa maneno fasaha na mwanatamaduni Shaaban Robert alisema kuwa ushairi huwa na ufasaha wa maneno. Hata hivyo kulikuwa na migongano kadhaa wa kimtazamo wa wataalamu hawa kuhusiana na ushairi.

Wale wa kimapokeo walisisitiza sifa za kiarudhi  kama vile urari wa vina na mizani katika utunzi wa mashairi. Wanamapinduzi nao hakuona umuhimu wa sheria hizi za arudhi muhimu zaidi ilikuwa ni maudhui na wala sio fani. Wanamapokeo walisisitiza matumizi ya lugha ya mnato na ya mkato. Wanamapinduzi hawakutilia makazo suala hili katika kutoa maana ya ushairi, kulingana nao mashairi ni lazima yabadilike kutokana na wakati na mazingira. Alihitimisha kwa kusema kuwa kwa ujumla mashairi yoyote yale, yawe ya kimapokeo au ya kisasa ni mashairi tu ilimradi jamii inufaike kutokana na mashairi hayo kwa kusisimka, kuelimika, kufunziwa amali zake, kukuziwa na kuendelezewa lugha yake.

Kulingana na Paneli ya Kiswahili, Felix (2018) katika makala yenye mada " *Ainaza Mashairi*" alidokeza kuwa mashairi yanaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti. Aidha alieleza kuwa bahari za mashairi hutegemea na muundo wa shairi kwa kuzingatia vina, mizani, vipande na mpangilio wa maneno. alitoa mifano ya aina za mashairi kutegemea idadi ya mishororo katika kila ubeti kama vile:-

| Mishororo | Aina |
|---|---|
| 1 | Tatmina/ umoja |
| 2 | Tathnia/ uwili |
| 3 | Tathlitha/ utatu |
| 4 | Tarbia/ unne |
| 5 | Takhmisa |
| 6 | Tasdisa |
| 7 | Usaba |

Aliendelea kudokeza kuwa, bahari za mashairi ziliainishwa kulingana na mtindo wake, umbo lake na matumizi ya ;lugha. Walitoa mifano ya bahari za mashairi kama vile:-

**i.** **Utenzi-** Shairi ndefu lenye kipande kimoja katika kila mshororo.

**ii.** **Mathnawi-** ni shairi lenye vipande viwili ( ukwapi na utao) katika kila mshororo.

**iii.** **Ukawafi-** Ni shairi la vipande vitatu \(ukwapi, utao na mwandamizi) katika kila mshororo.

**iv.** **Mavue-** Shairi la vipande vine (ukwapi. Utao, mwandamizi na ukingo) katika kila mshororo.

**v.** **Ukaraguni-**Shairi ambalo vina vyake vya kati na vya mwisho hubadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine

**vi.** **Ukara-** Shairi ambalo vina vya kipande kimoja havibadiliki kutoka ubeti mmoja hadi

mwingine, lakini vina vya kipande kingine hubadilika.

vii. **Mtiririko-** Shairi ambalo vina vyake vya mwisho na vya kati havibadiliki kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

viii. **Mkufu/ pindu-**Shairi ambalo neno la mwisho au kifungu cha mwisho cha maneno katika ubeti mmoja hutangulia katika ubeti unaofuatia

ix. **Msuko-** Shairi ambalo kibwagizo au mshororo wa mwisho ni mfupi kuliko mishororo minineyo.

x. **Manduma-**Shairi ambalo kipande kimoja hutoa hoja, wazo ama swali, huku cha pili kikitoa jibu au suluhisho.

xi. **Malumbano-** Mashairi mawili ambapo mshairi mmoja hutunga shairi akijibu au kupinga urtunzi wa mshairi mwingine.

xii. **Ngonjera-**Shairi lenye wahusika wawili ambao wanajibizana.

xiii. **Sakarani-** Shairi lenye bahari zaidi ya moja.

xiv. **Sabilia-** Shairi lisilokuwa na kibwagizo au kituo( mshororo wa mwisho hubadilika kutoka ubeti hadi ubeti)

xv. **Shairi guni-**Shairi lenye makosa ya arudhi za shairi

xvi. **Shairi huru-**Shairi lisilozingatia sheria za ushairi.

### 2.2.2 Tafsiri ya Ushairi

Osman (2017) katika jarida la tafsiri alisema kuwa tafsiri ni utendaji wa kiakili ambao maana katika usemi wa kiisimu hutolewa kutoka lugha moja hadi nyingine. Yaani ni tendo la kupitisha usemi wa kiisimu kutoka lugha moja hadi visawe vya lugha nyingine. Hapa lugha inayotafsiriwa huitwa matini chanzi ilhali lugha inayowakilishwa hitwa matini lengwa. Aliendelea kusema kuwa mtafsiri anafaa awe na ujuzi katika lugha zote ili aweze kupitisha mwazo na maoni yaliyodhamiriwa na mwandishi .

Mwansoko na wenzake (2006) walieleza kuwa tafsiri ni uwasilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kutafsiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maaandishi katika lugha moja (lugha chanzi) na kuyaweka badala yake mawazo yanayolingana katika lugha ya pili (lugha lengwa). Tafsiri huhusiana na kuhamisha maana ya makala asilia hadi katika makala tafsiri kwa kuzingatia muundo wa semantiki. Tafsiri ina jukumu la kuhamisha maana inayopatikana katika matini chanzi na kuiwasilisha katika lugha pokezi, wakimnukuu (Catford, 1965).

Kutokana na maelezo hayo ni wazi kwamba tafsiri ni uhamishaji wa ujumbe ambao umeandikwa kwa lugha moja (lugha asili) na kuuwasilisha kwa maandishi ya lugha nyingine (lugha pokezi). Ujumbe unajijenga katika maana ya matini. Maana nayo hutegemea vigezo kama muundo na mtindo wa lugha, muktadha wa utamaduni, na hali ya mawasiliano. Hivi pia ni vikwazo vya tafsiri.

Kulingana na wataalamu hao Mwansoko na wenzake (2006) kulikuwa na aina nne za tafsiri, ambazo ni: tafsiri muundo, tafsiri sisisi, tafsiri wazi, na tafsiri huru. Tafsiri muundo ni tafsiri ya mofu kwa mofu, inayoandikwa bila kubadilisha mpangilio wa vipashio hivi. Tafsiri ya aina hii haijali sheria za kisarufi, muktadha wa utamaduni, wala hali ya mawasiliano. Tafsiri sisisi hurejelea neno kamili. Maneno hutafsiriwa pwekepweke bila kujali muktadha wa lugha au utamaduni, wala hali ya mawasiliano. Kanuni zingine za sarufi, hata hivyo, hufuatwa. Lawama kuu ya tafsiri sisisi imo katika hatari ya upotovu wa maana, ambao mara nyingi hutatiza uwasilivu katika ujumbe. Tafsiri wazi pia huitwa tafsiri maana kwa vile inalemewa kwenye maana zote za matini asili. Kila sentensi ya matini asili huwakilishwa jinsi ilivyo. Tafsiri ya aina hii pia huthamini sana miundo ya sarufi, hususan semantiki na sintaksia ya lugha asili. Wajibu wake mkubwa ni kuhakikisha kuwa kila maana ya matini asili imehamishwa. Matokeo ya tafsiri wazi ni mshindilio wa taarifa, ambao mara nyingi huwakilishwa kwa sentensi ndefu kuliko kiasi.

Kulingana nao, lawama kuu ya tafsiri wazi ni ukavu wake ukosefu wa ladha ya ubunifu na ugumu wa kueleweka. Tafsiri huru pia huitwa tafsiri mawasiliano. Hii ni tafsiri fasirivu inayojali zaidi mahitaji ya hadhira. Tafsiri inaandikwa kwa lugha nyepesi tena yenye uwasilivu wa hali ya juu. Ingawa tafsiri hii inazingatia ujumbe na sarufi ya matini asili, inathamini zaidi mitindo ya mawasiliano, tajiriba, na utamaduni wa lugha pokezi.

Japo ushairi ulihusisha vipengee vilivyotajwa hapo juu, kulikuwa na tashwishi na maswali iwapo utafsiri wake ulikuwa ni jambo lililowezekana. Kulikuwa na wale waliosema kuwa ni jambo lisilowezekana ilhali kuna wale ambao hawakukubaliana na kauli hii. Wapinzani wa tafsiri ya ushairi walitoa sababu zifuatazo:-Wakati mashairi hasa yale ya falsafa yalipotafsiriwa, tashtiti na hisia zilitafsiriwa katika lugha nyingine, mashairi haya hayakuwa tu tepetevu bali yaligeuka kuwa mashairi mapya katika lugha lengwa. Walisisitiza kuwa ushairi katika tafsiri ulipoteza vipengee vyake vya kimsingi. Mitazamo hii ilienda sambamba na imani kwamba ushairi ulipotea kabisa katika tafsiri.

Walichukulia kwamba tafsiri ya ushairi ilikuwa ni ngumu sana kwa sababu ya mpangilio wa sauti na hisi katika maana moja. Vermeer (2000) alisema kuwa hakuna matini chanzi iliyo na tafsiri moja tu ambayo ni sahihi na inayokubalika'. Hivyo basi kila tafsiri lazima itangaze *Skopos* yake – yaani ieleze nia yake. *Skopos* ya matini lengwa sio lazima ifanane na *Skopos*ya matini chanzi. Ni lazima nia au *Skopos* ya matini lengwa ifafanuliwe ndiyo tafsiri itekelezwe. Alisisitiza kuwa, mara tu mtu anapoijua nia ya tafsiri, mikakati mingine kama vile urekebishaji na uundaji upya wa matini utajileta wenyewe wakati wa kutafsiri. Nadharia ya ***S****kopos* inasaidia kuangalia matini lengwa. Kama matini, tafsiri haibainishwi tu na matini chanzi lakini hubainishwa pia na nia yake. Robert (1968) alidokeza kuwa ushairi ni sanaa ya vina, yenye ufasaha wa maneno machache au muhutasari wa mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhutasari, huvuta moyo kwa namna ya ajabu. Maneno hayo ya Shaaban Robert yanatuvuta kuangalia namna wataalamu wetu wa ushairi wa Kiswahili walivyotumia dhana na mitazamo yao kuuangalia utanzu huu wa fasihi.

Mutugi (2012) alichunguza changamoto zilizoibuka katika kutafsiri kauli za pronomino kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Alionyesha kwamba athari za tafsiri mbaya ilikuwa ni kupotoshwa kwa maana. Kwenye uchunguzi wake alisema tafsiri ilikuwa ni mradi uliohusu masuala kadhaa. Kila sentensi ilihusu uteuzi mwingi kuhusu habari zake. Hivyo basi, tafsiri ni mchakato wala si tukio. Kwa muhtasari alisema tafsiri ilihusisha maamuzi yakiisimu yaliyofanywa wakati wa kuhawilisha maana.

Uchunguzi huu ulitufaa kwa kuwa ameshughulikia kipengele mahususi cha kiisimu.Mawazo yake kuhusu umuhimu wa uteuzi katika kutafuta ulinganifu wa kipengele alichokichunguza yalitufaa.Kilichotafsiriwa ni maana. Maana ilibebwa na maneno ya lugha. Kuna tofauti baina ya maana ya maneno na sentensi na maana ya matumizi ya maneno au sentensi. Hii ina maana kwamba kuna maana ya kimuundo na maana amilifu. Maana ya kimuundo huzingatia maana ya maneno na sentensi huku maana amilifu ikizingatia matumizi yao.

Kutokana na maelezo haya maana amilifu ilikuwa na mashiko zaidi katika kutafsiri.Nyaga (2012) alishughulikia ulinganifu katika tafsiri ya fasihi akitumia *Usaliti Mjini* kama kielelezo. Alionyesha sura tofauti tofauti za ulinganifu na kueleza jinsi ulinganifu uliibua matatizo katika uibushi wa maana. Kazi hii ilitufaa katika kutathmini ulinganifu wa shairi hili katika Kiingereza na Kiswahili.

Uchunguzi wa Omboga (2006) ulihusu utathmini wa kinadharia wa fasihi tafsiri ya Kiswahili. Alitaja mbinu mbadala za kusoma, kufafanua na kutoa nadharia ya matini zilizotafsiriwa kwa misingi iliyo nje ya mifumo na miundo ya urasmi. Yapo masuala mengine kama ya kimatini, kimuktadha, kitamaduni na ya ufundishaji yaliyochangia matini chanzi kufikia matarajio ya hadhira lengwa. Alisisitiza kuwa upataji ulinganifu ulikuwa ni matokeo ya kitamaduni na historia yaliyochangia utunzi wa matini za kifasihi wala si usawa wa kiisimu. Alitumia mifano kutoka *Mabepari wa Venisi*, Utenzi wa *Kalevala* na *Barua Ndefu kama Hii*. Alisisitiza kuwa tafsiri ya shairi lazima ingekuwa na upungufu ambao ungeathiri sana fani kuliko maudhui.

Iwapo mtafsiri alitafsiri shairi kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi, lugha iliyotumiwa katika tafsiri ilikuwa nakala tu ya miundo ya tungo za kishairi ya lugha ya awali. Licha ya kulazimisha kuingiza kaida za ushairi za lugha ya kwanza katika lugha ya pili, maana ya shairi hilo katika lugha ya pili ilipotea. Sababu ni kwamba, lugha ya shairi la pili ilionekana kuwa butu. Kwa hivyo, kila lugha ilikuwa na kaida zake za kishairi. Hata hivyo, palikuwa na uwiano kati ya lugha moja na nyingine na kati ya tamaduni moja na nyingine. Uwiano huu uliwezesha pawe na uwezekano wa kutafsiri shairi kutoka lugha moja hadi nyingine. Tofauti kati ya lugha mmoja na nyingine na kati ya tamaduni moja na nyingine ndizo ziliibua haja ya kutafsiri. Lakini tofauti hizi pia zilizua utata katika tafsiri. Jambo hili halikumaanisha kuwa watu waepukane na utafsiri wa ushairi kwa sababu ushairi ulikuwa ni njia mojawapo ya kueleza hisia na mielekeo kuhusu masuala ya kilimwengu.

Kulingana na Mulokozi (2008) wanamsambao waliamini kuwa pale ambapo kufanana au uwiano baina ya lugha utatokea sababu ya msingi ya mfanano huo ni kuwa katika kipindi fulani hapo zamani jamii hizo ziliwahi kukutana kwa namna fulani na makutano hayo yalisababisha hali ya kuazimana baadhi ya mila na desturi.Kwa ujumla mawazo ya wafuasi wa nadharia hii waliamini kuwa utamaduni uliweza kusambaa kutoka katika jamii imara na maarufu tena yenye nguvu kuelekea katika utamaduni wa jamii iliyo dhaifu. Hivyo basi kutokana na mawazo ya wataalamu hawa ni kuwa fasihi simulizi ya kiafrika ilisambaa kutoka sehemu moja iliyostaarabika (Ulaya) kwenda sehemu nyingine ambayo haijastaarabika (Afrika). Kwa mfano ushairi wa simulizi wa Kiswahli ulitoka Uarabuni na Uajemi kuja Afrika na huko ndiko ambako kulionekana kuwa kumesataarabika kuliko Afrika na ndio maana ushairi huo ulileta huku Afrika (Mulokozi, 2008: 1973).

Wananadharia hii waliamini kuwa asili ya fasihi simulizi ya kiafrika ni ulaya, jambo ambalo hatukukubaliana nalo kwani kila jamii ilikuwa na fasihi yake na kutokea mfanano wa baadhi ya kazi za fasihi huenda kuliathiriana kwa namna fulani miongoni mwa jamii hizo.Mbinu za tafsiri ni hatua zilizopelekea kwenye suluhisho la tatizo la tafsiri.

Wataalam katika katika makala yao " *Tofauti kati ya Ukalimani na tafsiri*; *Kinatharia na Kivitendo*"wakitofautisha ukalimani na tafsiri walimnukuu Wanjala (2011) aliyesema kuwa ukalimani ni kuhawilisha ujumbe uliopo katika mazungumzo pamoja na uamilifu wake kutoka lugha chasili hadi lugha lengwa kwa kuzingatia isimu ya lugha husika, utamaduni na muktaadha katika jamii fulani. Kwa kutumia kigezo cha maana tofauti ya ukalimani na tafsiri ni kuwa, tafsiri ni taaluma ya uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa kwa kuzingatia isimu, muktadha na utamaduni.

Lengo kuu la makala haya lilikuwa ni kufanya uchunguzi wa kina juu ya mbinu zilizotumika kutafsiri maneno yaliyofungamana na utamaduni kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza. Malengo mahususi yalikuwa ni; kubainisha mbinu zilizotumika kutafsiri maneno ya kiutamaduni, kuibua mbinu iliyotumika zaidi kutafsiri maneno ya kiutamaduni katika matini za kitalii, kubainisha mbinu iliyofaa kutafsiri matini za kiutamaduni kutoka Kiingereza hadi Kiswahilina kubaini sababu ambazo zilisababisha kutumia mbinu hiyo zaidi ya mbinu zingine katika kutafsiri maneno ya kiutamaduni katika matini za kitalii.

### 2.2.3Kipengee cha Kiisimu

Balikumi (2017) katika makala yake "*Isimu- Kijue Kiswahili*" aliangazia dhana ya isimu na matawi yake. Kulingana naye isimu au " maarifa ya lugha"ni sayansi inayochunguza lugha.Isimu imegawika katika matawi mbalimbali kama vile:- fonetiki(kuhusu sauti zinazotolewa na binadamu), fonolojia( kuhusu mfumo wa sauti katika lugha fulani), mofolojia (kuhusu mfumo wamaneno), sintaksi (kuhusu mfumo wa sentensi) na semantiki( kuhusu maana).

Cruz (2017) Agosti tarehe 4, katika makala yake "*what is linguistics*" kuhusu maana isimu alidokeza kuwa kila lugha huwa ni uchangamano wa fahamu na uwezo wa kuwawezesha wasemaji wa lugha husika kuwasiliana na kuonyesha hisia mbalimbali na matamanio yao.

Aliendelea kusema kuwa isimu ni uchunguzi wa mifumo hii ya fahamu na huangazia umbo la mfumo wa fahamu, jinsi inavyopatikana, jinsi inavyotumika katika utoaji na uelewaji wa ujumbe na jinsi inavyobadilika kulingana na mapito ya wakati. Kulingana naye, wanaisimu hujihusisha na maswali kuhusu utaratibu wa lugha. Ni vipengee vipi vinafanana katika lugha zote za binadamu?

Ni kwa jinsi gani lugha hutofautiana na ni kwa kiwango gani lugha hutofautiana kimfumo, yaani tunaweza kupata ruwaza katika tofauti? Ni kwa vipi watoto hupata ufahamu wa lugha katika kipindi kifupi? Ni kwa vipi lugha hubadilika kulingana na mapito ya wakati na kuna mipaka kuhusu ni kwa vipi lugha hubadilika? Ni kwa vipi mifumo zingativu huchangia katika kuzalisha na kuelewa lugha? Aliendelea kusema kuwa upande wa isimu unaojishughulisha na umbo la lugha hugawika katika vikundi hivi: fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki.

Mbali na umbo la lugha kuna vipengee vingine vya lugha ambavyo huwakilishwa na matawi kama vile:- isimu historia, isimujamii, isimu nafsia, isimu ethnografia, upembuzi, isimu kokotozi na isimu nyurolojia. Aliongeza kusema kuwa isimu hiingiliana na masomo mengine kama vile:- falsafa,fasihi, ufundishaji wa lugha, saikolojia, sosholojia, patholojia ya usemi fizikia, elimu viumbe, sayansi ya kompyuta, kopyuta handisi na sayansi ya siha. Alihitimisha kwa kuangazia umuhimu wa isimu katika muktadha wa kiakademia ni kuendeleza ufahamu. Aidha wasomi wengi hutumia isimu katika ufundishaji wa lugha, patholojia ya usemi, tafsiri mashine, katika kutaja majina ya vitu na maumbo yote ya uandishi, uhakiki, na uchapishaji . Alitoa mfano wa aliyekuwa mwanafunzi wa chuo kikuu cha Carlifonia, Marc Okrand aliyetumia isimu kuvumbua lugha ya Klingon katika sinema ya *StarTrek.*

Kulingana na Wanjiru (2018) katika tovuti ya swahilihub.com.kwenye makala yenye mada, "*Isimu pamoja na matawi mbalimbali ya isimu katika Kiswahili*" alisema kuwa isimu ni taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na masuala ya lugha. Aliangazia sifa za isimu kama sayansi kwa kuangazia vipengee vya kadha wa kadha. Kuna matumizi sikisayansi na huitwa takwimu leksika. Kipengee cha Elimu viumbe katika isimu huchunguza maneno kutoka kinywani na vile yanavyotoka pamoja na yanakotoka. Maabara ya lugha hutumika katika kufanya uchunguzi wa lugha hasa katika nchi zinazoendelea. Kazi inayohusisha maabara bila shaka ni ya kisayansi.

Fizikia ni soma la sayansi ambalo hujihusisha na matumizi ya nguvu yoyote ile. Isimu pendekezi inapendekeza; kwa mfano, katika lugha mama Isimu elekezi hasa hutokea tunapotumia lugha ya pili. Kulingana na makala hayo isimu imegawanyika katika makundi mawili:Isimu pweke na Isimu tumizi. Isimu pweke ni tawi linalojishughulisha na jinsi sauti za lugha zinavyotamkwa. Isimu hii nayo ina matawi madogo kama vile fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki. Isimu tumizi ni tawi ambalo limegawika katika makundi madogo madogo kama vile isimu saikolojia,isimu historia na isimujamii.Isimu ni uchunguzi wa lugha kisayansi. Ipo taaluma kama falsafa ambayo nayo inaweza kujishughulisha na uchunguzi wa maswala ya lugha lakini si kwa kutumia vigezo vya kisayansi.

Wanaisimu huhakikisha kwamba wakati wa kutafiti na hatimaye kuwasilisha matokeo ya utafiti wao wanatumia vigezo vya kisayansi hatua kwa hatua. Kwanza huchunguza na kukusanya data. Halafu wanafanya ulinganisho kabla ya kuunda nadharia na kuzipima nadharia na kuzipima matukio yake. Baadaye hujiundia nadharia na kutoa kanuni ambazo zinapimika (MacMahon, 2009). Uchanganuzi wa kiisimu ulijumuisha: kiwango cha sauti, kiwango cha sauti za lugha mahsusi zilipowekwa pamoja kuleta maana, kiwango cha maumbo ya sauti hizi, maana mahsusi ya neno na kiwango cha matumizi ya lugha katika muktadha mahsusi.

Matukio ya kiisimu na ya kiakili yaliongozwa na mfumo mahsusi kulingana na mpangilio na maadili ya lugha mahsusi. Tulipata kwamba, lugha ilikuwa ni mfumo wa kitamaduni kwani ilikuwa ni kioo cha jamii na iliumba na ilibainisha matamshi na hisia za lugha husika. Iwapo lugha zote za binadamu zilikuwa na muundo, istilahi na maumbo mahsusi ilikuwa ni wazi kwamba ingekuwa vigumu kuhamisha kwa ukamilifu matini kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa.

Maswala yaliyopelekea kuwe na changamoto za kiisimu ni kama vile fonolojia ambayo ni tawi la isimu linaloshughulikia mfumo wa sauti za lugha mahsusi. Hapakuwa na lugha zozote mbili zilizokuwa na ufanano wa kifonolojia. Haikuwezekana kuunda upya sauti katika kazi iliyotungwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa ufupi, tofauti za lugha mbili hazikutokana tu na utofauti wa kifonolojia, bali pia zilitokana na mifumo ya sauti ya lugha mbili husika.

Pili, ni sintaksi ambayo ni tawi la Isimu lililoshughulikia kupanga na kuhusisha vipashio na maneno kisarufi. Hapakuwa na lugha zozote mbili ambazo zilikuwa na ufanano wa muundo wa kisintaksi. Ilikuwa ni vigumu kuunda upya sintaksi ya lugha moja katika lugha nyingine. Chomsky (1965) alitoa fasili ya sintaksi katika sentensi kwa kusema, "Ni taaluma ya kanuni na michakato ambapo sentensi huumbwa katika lugha mahsusi." Tulipata kuwa fonolojia ilitawala sauti ilhali sintaksi ilitawala muundo ambamo sauti fulani ingefaa. Isimu ya kisasa ilionyesha ya kuwa lugha asilia sio mkusanyiko wa vipengele, bali ni mifumo ambamo vipengele vyote vinahusiana kwa pamoja. Katika kipindi fulani mahsusi, mzungumzaji aliweza kutumia sauti, maneno mahsusi na namna ambavyo ziliunganishwa pamoja. Haya yalikuwa ni mambo ambayo mwanaisimu alieleza katika fonolojia, istilahi na sarufi (Sintaksi) ya kila lugha. Kila lugha iliweza kuwa na mfumo wake wa kipekee na sehemu za ruwaza za mifumo hii iliweza kuonyesha ufanano katika sehemu za mifumo ya lugha nyingine, hasa katika lugha ambazo zilikuwa na uhusiano wa kikaribu. Hata hivyo, lugha tofauti zikiitatua matatizo ya kuonyesha hisia na mawasiliano kwa njia tofauti. Kulikuwa na uwezekano wa kuhamisha maneno kulingana na jinsi yalivyohusiana katika sentensi (Fowler, 1966).

Lehmann (1978) alisisitiza tofauti ya kimsingi kati ya mpangilio wa kisintaksia wa mifumo ya kimawasiliano isiyokuwa ya kibinadamu. Alieleza kwamba sintaksia ni kipengee kikuu cha lugha ya binadamu. Miongoni mwa mifumo yote iliyotambulika kama ile ya nyuki, ndege, na wanyama wengine, ni mfumo tu wa binadamu ambayo sintaksia yake imeendelea zaidi. Hapa Fowler na Lehmann walitazama mfumo wa mawasiliano ya binadamu japo Lehmann alibainisha mfumo huo kati ya mifumo mingine ya wanyama wengine Kwa kawaida,  ilikuwa vigumu kuzielewa na kuzifasiri kazi za Chomsky kwa Kiingereza na ilikuwa vigumu zaidi zikitafsiriwa. Hivyo ziliishia kuwa na ugumu wa kutoa maelezo kupitia tafsiri za dhana nyingi za kiisimu. Zaidi ya hayo, makisio huenda yalitumiwa katika juhudi za kufikia zile tafsiri kamili au tafsiri zilizoridhisha. Jambo hili liliwalemea wanafunzi pamoja na walimu.

Kulingana na wanaisimu kama vile McIntosh na Halliday (1964) walisema, "Tunapojishughulisha na mfumo funge tunajihusisha na sarufi. Iwapo uteuzi ni wazi, tunajihusisha na uteuzi wa kileksia (istilahi) na sio wa kisarufi." Katika mashairi kipengee cha kiisimu kilidhihirika kupitia kipengele cha arudhi. Hapakuwa na lugha zozote zilizokuwa na sifa sawa za kiarudhi.

Namna tamko la silabi zilihesabiwa (Yaani, mahadhi ya kimuziki ya tamko) zilitofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kiasi cha tamko katika mfuatano wa silabi ulikuwa sawa hata pawe na idadi ngapi za mkazo katika tamko. Kila lugha ilikuwa na sifa yake ya kiarudhi. Kwa ujumla, kulikuwa na mbinu nyingi katika kutafsiri matini lakini sio mbinu zote ambazo zilitumiwa katika kutafsiri mashairi (Njogu, 1999). Hapa Njogu anatilia mkazo sifa za kiarudhi zinazobainisha lugha na jambo hili liliwafanya watafsiri kutumia mbinu mbalimbali.

Kutokana na maelezo ya wanaisimu hawa ni dhahiri kwamba katika kutafsiri hatufai kuchunguza suala la sarufi pekee bila kuangazia matumizi ya lugha katika maisha halisia. Kulingana na Lefevere (1975) kulikuwa na mbinu saba zilizotumika na wafasiri waingereza katika kutafsiri mashairi:Tafsiri ya kifonemia, tafsiri sisisi, tafsiri ya kimita, tafsiri kutoka mfumo wa beti hadi wa kinathari, tafsiri kwa kutumia vina, tafsiri huru na tafsiri ya kufasiri. Matokeo ya tafsiri ya kifonemia yalikuwa mazito kuelewa hasa kwa upande wa sauti na wakati mwingine baadhi ya sehemu na maana asili katika matini chanzi yalidondolewa.

Tafsiri sisisi haikumruhusu mtafsiri kutilia maanani maana asili, ilhali vishazi na sentensi ziliegemezwa katika lugha lengwa. Tafsiri ya kimita ilisisitiza utoaji wa mahadhi ya kimuziki asili katika lugha lengwa. Hii ni kwa sababu kila lugha ilikuwa na mfumo wake mahsusi wa msisitizo na matamshi. Matokeo ya mbinu hii ilikuwa ni tafsiri isiyofaa kwa kurejelea maana na muundo. Tafsiri kutoka mfumo wa beti hadi kinathari ulikuwa na athari kwa kuwa, ujumi wa shairi asili ulipotea. Tafsiri kwa kutumia vina ilisisitiza uhamisho wa vina kutoka shairi asili hadi tafsiri katika lugha lengwa. Matokeo yalifaa katika muundo wa nje lakini hayakufaa kisemantiki. Katika tafsiri huru iliweza kupata visawe sahihi katika lugha lengwa iliyokuwa na thamani ya kisanaa.

Kwa upande mwingine, vina na mahadhi ya kimuziki hazikuzingatiwa. Muundo wa nje ulikuwa tofauti na ule asili lakini kisemantiki ulikuwa ni sawa. Tafsiri za kufasiri zilikuwa za aina mbili: Tafsiri ya beti ambapo katika lugha lengwa, matokeo yalikuwa sawa kisemantiki lakini kimuundo ilikuwa ni tofauti na pili, tafsiri za uigaji ambayo ilikuwa tofauti lakini kichwa, mada na mwanzo wa shairi zilikuwa sawia na shairi asili.Kutokana na maelezo ya Lefevere (1975) tulipata kuwa alijaribu kusisitiza upya kuwa udhaifu wa mbinu za kutafsiri ushairi ulitokana na msisitizo uliopewa katika mojawapo ya vipengee vya kutafsiri. Mbinu za sisisi, za kimita na zilizingatia mahadhi ya kimuziki muundo wa shairi ilhali nyingine zilisisitiza utoaji wa maana sahihi katika lugha lengwa.

Maelezo yake pia yanashabihiana na yale ya Njogu kwamba kila mbinu ina upungufu ndio maana mbinu nyingi hutumiwa katika kutafsiri mashairi. Urari ulizua changamoto kwa sababu kila lugha ilikuwa na ruwaza yake mahsusi ya urari. Katika tafsiri za beti, kulikuwa na changamoto kwa sababu mashairi yote yalikuwa na maana nyingi. Haikuwa rahisi kutafsili hata maana ya kimsingi ya neno tamko kwa usahili. Kwa kawaida, maneno yalikuwa na mipaka isiyo dhahiri hivyo maana haikujitokeza wazi. Ili kuweza kutafsiri ushairi kwa njia mwafaka, wafasiri walifaa wawe washairi wa kutambua miundo ya kishairi katika lugha chanzi na lugha lengwa. Kadhalika, walifaa wawe na kiwango cha hisi katika kutafsiri ushairi katika mfumo wa beti  au wa kinathari.

Kulingana na Newmark (1981: 170-171), "Miongoni mwa tanzu zote za fasihi, tafsiri ni ya ushairi ndio ngumu zaidi." Kadhalika, changamoto zilizomkabili mtafasiri katika kujaribu kuiga matini chanzi zilihusisha umbo, mizani, maana na matumizi ya tamathali za usemi. Kwa kuwa sentensi ndiyo kipashio cha kimsingi cha fikira, kinachowasilisha kitu na kile kitu hicho hufanya, kilivyo, au huathiriwa nacho, basi sentensi ndiyo kipashio cha tafsiri. Kimsingi, unatafsiri ukizingatia sentensi, na katika kila sentensi, nia pamoja na kile kinachoitendekea nia hiyo ndiyo mambo ya kuzingatiwa kwanza.

Kupitia maelezo yake tulipata kwamba istilahi za tafsiri za kimawasiliano na kisemantiki ya kimawasiliano ilijaribu kuleta maana kama ilivyokuwa katika matini chanzi ili wasomaji wasiwe na ugumu wa kuelewa habari katika matini iliyotafsiriwa. Hapa, mtafsiri aliweza kuhamisha kwa wingi vipengele ngeni vilivyo katika matini chanzi hadi tamaduni ya lugha lengwa palipokuwa na haja. Tafsiri ya aina hii ilitumika mara nyingi katika matini ya ki-ubishi na ya kisayansi.

Medhat (2011) katika makala yake ya ukiushi wa kiisimu alidokeza kuwa katika kutafsiri ushairi hatuangazii tu mahadhi ya muziki hata mashairi huru huwa na sifa zake za kishairi. Alimnukuu Leech (1969) aliyesema kwamba kilichojenga shairi ni ukiukaji wa kiisimu. Alizua aina nane za ukiukaji: ukiukaji wa kileksia, ukiukaji wa kisarufi, ukiukaji wa kifonolojia, ukiukaji wa kigrafolojia, ukiukaji wa kisemantiki, ukiukaji wa  kilahaja, ukiukaji wa kisajili na ukiukaji wa kipindi cha historia. Ukiukaji wa kisarufi ulitokea wakati ambapo mshairi alizua maneno mapya. Ukiukaji huu ulichangia katika kuendeleza msamiati wa lugha husika.

Ukiukaji wa kifonolojia ulihusisha ukiukaji wa sauti na matamshi ya lugha mahsusi kimaksudi ili kudumisha mahadhi ya kimuziki. Ukiukaji wa kigrafolojia nao ulihusisha washairi ambao walikiuka kanuni za uandishi.

Ukiukaji huu uliathiri pakubwa mishororo ya shairi hivi kwamba haikulingana. Ukiukaji huu uliweza kuzua maana nyingine kando na maana halisi ya ubeti. Ukiukaji wa kisemantiki ulihusisha ukiukaji wa maana katika shairi kiasi cha kupoteza mantiki. Hivyo maana ya moja kwa moja iliathirika hivyo msomaji alitegemea uumbuji wa taswira ili apate kuelewa maana. Katika ukiukaji wa kilahaja mshairi alikopa maneno yaliyotokana na lahaja za kijamii au za kimaeneo. Ukiukaji wa kisajili ulihusisha matumizi ya sajili nyinginezo kando na sajili ya kishairi.

Ukiukaji uliohusiana na kipindi cha kihistoria ulihusisha matumizi ya maneno ya kale. Kutokana na maelezo haya tulipata kwamba aina hizi za ukiukaji zililitegemea aina ya shairi na lengo la mshairi. Catford (1965) alibainisha aina mbili za dhana ya matini kutotafsirika kwa matini ambapo dhana ya kwanza ilikuwa ya kiisimu na nyingine ya kitamaduni. Katika kiwango cha kiisimu, kutotafsirika kwa matini kulifanyika wakati ambapo hapakuwa na kisawe cha kileksia au kisintaksi katika matini lengwa. Jambo hili lilitokana na ukosefu wa kipengee cha hali ya kitamaduni katika tamaduni ya matini lengwa. Ilikuwa ni bayana kwamba kazi ya mtafsiri ilikuwa ni kutafuta suluhu ya shida hizi za kiisimu.

Katika mwalimuwakiswahili.com Novemba tarehe 23 (2017) makala yanayohusu tafsiri,waandishi walidokeza kuwa, changamoto katika shughuli ya kutafsiri hujidhihirisha katika vipengele vikuu vinne yaani maumbo ya sauti, maumbo ya maneno, miundo ya sentensi pamoja na maana. Harianto (2018) katika makala yake ya changamoto za kutafsiri ushairi alisema kuwa tunapoangazia changamoto za kiisimu lazima tuangazie uendaji pamoja wa maneno na maumbo ya kisintaksia ambayo si rasmi. Alitoa mifano katika maneno ya Kiingereza kama vile:- Waingereza husema “*makeaspeech*” na wala sio “*say a speech*” Aidha alidokeza kuwa muundo wa shairi huathiriwa na muundo wa sentensi ya lugha husika.

### 2.2.4 Kipengee cha matumizi ya lugha

Katika tovuti https://go.smartling.com. mwezi wa Juni, tarehe 2, mwaka wa (2017) katika chapisho lenye mada”*Common Challenges of Translation*” mhariri anasema kuwa tafsiri huhitaji uelewa wa sarufi na tamaduni ya jamii husika.

Aliendelea kusema kuwa tamthali za usemi huwa ni tata kutafsiri kwa vile maana si ya moja kwa moja. Jambo hili hupelekea kuwe na utata wa kutafsiri kimashine.

Alidokeza kuwa wachapishaji wanafaa kupunguza matumizi ya tamathali za usemi katika matini wanayodhamiria kutafsiri. Hata hivyo iwapo wanasisitiza kutumia tamathali hizo ni vyema wawe na ufahamu wa kutosha wa tamaduni za lugha husika. Watafsiri wamechunguza changamoto tano zinazowakabili watafsiri Katika kipengee cha utamaduni walisema kuwa lahaja huingiliana na lugha nyingi na huathiri matini. Aidha, kila lugha ina mfumo wake ambao huathiri tafsiri;kama lugha ni sahili pia tafsiri itakuwa rahisi.

Gessman (2017) tarehe 27 mwezi wa Oktoba katika makala yake, "*The Most Common Challenges with Translation*" alitoa mfano wa msemo wa msemo wa Kiingereza" *I've been feeling under the weather*" Kulingana na Buliba (2001) Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kiasili nchini Kenya. Asili yake ni pwani ya Kenya. Ni lugha ambayo imeenea kwa kasi barani Afrika na hata duniani kote. Nchini Kenya na Tanzania, Kiswahili ni lugha rasmi na ya kitaifa. Kiswahili ni lugha ya pekee yenye uwezo wa kutumika kama "Lingua Franca" ya bara hili.

Kutokana na kuenea kwake, lugha ya Kiswahili ni nyenzo muhimu ya kuiendeleza nchi kiuchumi.Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Lugha inaweza kuathiri na kuathiriwa na Lugha nyingine. Mfano, lugha ya Kiswahili imeathiriwa sana na lugha za Kiarabu, Kiingereza na hata lugha za Kibantu. Yawezekana pia kwa kiasi fulani ikawa Kiswahili kimeziathiri lugha hizo. Mifano wa maneno yenye asili ya Kiarabu ambayo yameingia katika lugha ya Kiswahili ni *kalamu*, *kitabu*, *daftari*, *adhabu*, *dhawabu*, *dhambi*, *dhahabu*, *sababu*,*aibu*, *laana*, *zina*, *dhima*, *wajibu*, *mahaba*,*sakafu*, *karibu*, *tafadhali*,*nafsi*, *roho*, *safari*, *salamu*, *amali*, *tabianasifa*. Mifano ya maneno yenye asili ya Kiingereza yaliyoingia katika Kiswahili ni *buku*, *peni*, *begi*, *kabati*, *rula*, *buti*,*bia*,*springi*, *stoonaskrubu*.

Kupitia maelezo haya ni wazi kuwa umuhimu wa lugha ni kama vile kuwasiliana ambapo lugha hutumika kupashana habari, kuunganisha ambapo lugha hupatanisha na kuleta uelewano miongoni mwa wanajamii.

Pia lugha hutumiwakutofautisha jamii moja na nyingine, kujenga jamii ambapo lugha huleta au huhimiza shughuli za maendeleo ya jamii, huleta amani na mshikamano katika jamii, kufundishia ambapo lugha hutumika katika kufundishia elimu, kutambulishaambapo lugha hutumika kutambulisha jamii ya watu fulani na chombo cha kuhifadhi na kueneza utamaduni. Hapakuwa na lugha zozote mbili ambazo zilikuwa na ufanano wa kiistilahi .Tulipata kuwa hata lugha ambazo zilikaribiana zilikuwa na dhoruba tofauti katika lugha tofauti.

Kulingana na Suryawinata (1982) miongoni mwa mbinu za kutafsiri zilizopendekezwa tafsiri za kimawasiliano na za kisemantiki ndizo zilikuwa bora zaidi. Sababu ni kwamba, mbinu hizi ndizo zilizosemekana kutimiza malengo makuu ya tafsiri: Iktisadi na usahihi. Hapakuwa na lugha zozote mbili ambazo zilishabihiana kimuundo. Sawa na miundo mingine ya kiisimu, ambazo zilikuwa na mizizi katika tamaduni na lugha mahsusi, iliegemea mipaka ambamo mtunzi alifanyia kazi kulingana na usuli wa tamaduni alimokulia na mahitaji ambamo amekulia na kulingana na mahitaji ya tamaduni yake. Maumbo ya kifasihi yaliweza kukubaliwa katika mipaka ya kiisimu na ya kitamaduni; ziliweza kubadilishwa na kuumbwa kufaa muktadha mpya. Lakini sawa na maelezo mengine ya tamaduni na lugha, hazikuweza tu kuhamishwa moja kwa moja bila kubadilishwa katika tamaduni mpya na mazingira mapya. Nadharia ya kutafsiri istilahi ilizuliwa na Kiingi K.B. ambaye alitaja vigezo vilivyoweza kutumika katika kutathmini fasiri ya istilahi.

Vigezo hivi vilikuwa vifuatavyo: *usahihi*, *uiktisadi*, *uzalishi*, *umataifa*, *uangavu*, *ustaara*, *utaratibu*, *ulinganifu* na *uhalisia*. Katika tafsiri, istilahi ilifaa kueleza istilahi asilia kisahihi. Kiiktisadi, ilikuwa muhimu istilahi isiwe na silabi nyingi katika tafsiri. Kwa upande wa uzalishi istilahi ilikuwa na maana iwapo iliweza kuzalisha maneno mengine. Katika kigezo cha umataifa, istilahi iliyokopwa kutoka maneno ambayo yamekopwa kutoka umataifa yalikuwa na umataifa zaidi. Kipengee cha uangavu nacho kilisisitiza kwamba istilahi ilipaswa ifae zaidi au iwe sahihi katika matumizi yake. Ustaara nao ulionyesha kwamba istilahi ilifaa ikidhi mahitaji ya watumizi.

Dhana ya ulinganifu nao ilisisitiza kwamba istilahi ilipaswa ikaribiane na utaratibu wa lugha husika. Uhalisia nao ulionyesha kwamba istilahi ilifaa ionyeshe ufaafu katika matumizi yake (Kuvuna, 1992). Maelezo haya yalidhihirisha kuwa mbinu nyingi zilihitajika ili kukidhi mahitaji ya kutafsiri.

Tafsiri za matini za kisheria pia ziliathiriwa na mambo mengine ambayo si ya kiisimu. Sheria na lugha ya kisheria zilifungamana na historia, ukuaji na tamaduni za mfumo wa sheria.

Mifumo ya kisheria ilikuwa na upekee wa kijamii. Kila jamii ilikuwa na mfumo tofauti wa kitamaduni, kijamii na kiisimu. Dhana za kisheria, mila za kisheria na utekelezaji wa sheria zilitofautiana kutegemea jamii husika. Sheria ya taifa fulani huwa ni mfumo huru wa kisheria ulio na istilahi zake, dhana zake na kanuni zake za uainishaji. Sheria hizi zilitofautiana kutoka taifa moja hadi nyingine. Jambo hili lilizua changamoto wakati wa kutafsiri kutoka mfumo mmoja hadi mwingine.

Newmark (1988: 94) alisema kuwa tamaduni ya jamii ilidhihirika kupitia virai,vishazi au sentensi ambazo zilikuwa na maneno ambayo yaliyohusiana na kategoria za kitamaduni kama vile dhana, mila na desturi na ekolojia. Tukiangazia ekolojia, tulipata kwamba Kiswahili kilizungumzwa kwenye nchi ya joto ilhali Kiingereza kilizungumzwa kwenye nchi ya baridi na msimu mfupi sana wa joto la wastani. Mswahili aliweza kubainisha misimu minne yaani, *kiangazi*, *vuli*, *masika* na *kipupwe*. Mwingereza naye aliweza kubainisha misimu minne:- *summer*, *autumn*, *winter* na *spring*. Hata hivyo, misimu hii haikuweza kushabihishwa katika lugha hizi mbili. Hii ni kwa sababu maneno yaliweza kupata vivuli chanya na hasi kutokana na athari za hali ya hewa.Kipengele cha dhana kilihusisha maneno mengi mapya yaliyotokana na uvumbuzi wa kisayansi na ubunifu wa kiteknolojia.

Maneno haya yaliingia katika utamaduni wa Kiswahili kila wakati. Ilikuwa ni vigumu kutafuta visawe vya maneno haya katika lugha ya Kiswahili. Tofauti za mila na desturi na imani ziliweza kuakisiwa katika tabia za ulaji, unywaji, mavazi, mienendo yao ya maisha katika masuala ya mapenzi, na ndoa. Katika ulaji, waswahili walikuwa na milo mitatu: kifungua kinywa, chakula cha mchana na chakula cha jioni. Kwa upande mwingine Kiingereza kilikuwa na : *breakfast*, *lunch*, *hightea*, *dinner* na *supper*. Kadhalika ilikuwa ni vigumu kupata majina ya vyakula na vinywaji. Kulikuwa na tofauti katika mavazi yaliyozua matatizo kadhaa ya kifasiri.

Kila kabila lilikuwa na majina mahsusi ya mavazi, ilikuwa ni vigumu kupata visawe vya mavazi haya katika tamaduni nyingine. Katika masuala ya mapenzi, utamaduni ya waingereza ulikuwa huru na wazi zaidi ukilinganisha na ule wa waswahili. Kisiasa, msamiati uliakisi mhemko na jazba hivyo ulikuwa ni vigumu kutafsirika.

Kidini matatizo ya kifasiri yalitokana na dhana ambazo zilikuwa marufuku katika jamii lengwa (Massamba, 1983). Maelezo ya Massamba yalishabihiana ya yale ya Sakareva kwa kuonyesha jinsi dhana ya utamaduni ulivyoathiri tafsiri.Utamaduni kulingana na Newmark (1988: 94) ulikuwa ni mkusanyiko wa mila na desturi za jamiiiliyotumia lugha moja mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Msamiati wa lugha kwa kiwango kikubwa ulijenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii ilimozungumzwa lugha hiyo. Hivyo maana za maneno yalikuwa ni kiungo au daraja madhubuti kati ya utamaduni na lugha katika tafsiri.

Kitabu cha *Wimbo wa Lawino* kiliandikwa kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiacholi kama *Wer pa Lawino* na kutafsiriwa katika Kiingereza na mwandishi mwenyewe wa matini chanzi. Tafsiri ya Kiingereza ina istilahi za Kiacholi ambazo hazina visawe katika lugha ya Kiingereza. Liyong (2001) alijadili kuwa tafsiri ya Okot (1972) haitafsiri istilahi za Kiacholi zihusuzo  mila, densi, ala za kimuziki na mimea. Sozigwa (1975) alipotafsiri shairi hili alihamisha baadhi ya istilahi hizi katika lugha ya Kiswahili ili kudumisha maana. Mfano mzuri ni istilahi zilizotumiwa katika vipindi fulani kama vile odunge( kipindi cha njaa), pot-kot (kipindi kabla ya mvua kuanza). Aidha kutokana na muktadha wa kitamduni wa lugha husika matukio ya kihistoria yalizua utata katika tafsiri. Hii ndio sababu mtafsiri alidumisha baadhi ya majina kama vile ya mapepo kama labeja na vifaa kama vile orak na otole ili asipotoshe maana.

Mtafsiri aliweza kuhusisha taratibu hizi za kutafsiri: Tafsiri sisisi, uhamishaji, utohozi, maelezo ya visawe, uainishaji, uchanganuzi wa vijenzi, udondoshaji, uongezaji, ufafanuzi, upanuaji na sinonimi.Katika tafsiri sisisi, mtafsiri alifanya tafsiri baina ya vitengo kutoka neno hadi vitengo vikubwa zaidi kama vile vishazi au virai. Katika utaratibu wa uhamishaji, mtafsiri alibadilisha neno katika  lugha chanzi moja kwa moja katika neno katika lugha lengwa kwa kurekebisha abjadi. Kadhalika yeye alirekebisha abjadi katika matamshi halisi ya matini lengwa. Hivyo, dhana ya utohozi iliibuka.Kadhalika, mtafsiri aliweza  kutafuta kisawe cha neno katika utamaduni wa matini lengwa. Iwapo ilikuwa ni jambo lisilowezekana, angetafuta kisawe cha utendakazi kwa kutoa maelezo katika matini lengwa na kumfanya atumie utaratibu wa maelezo. Wakati mwingine, mtafsiri aliweza kutoa maelezo ya kijumuishi katika matini lengwa hivyo kutumia mbinu ya uainishaji. Lakini iwapo angetoa kisawe kilichokuwa karibu na matini chanzi angekuwa akitumia utaratibu wa sinonimi.

Katika uchanganuzi wa vijenzi, mtafiti alitenga vitengo vya kileksia kutegemea maana moja na nyinginezo. Kadhalika, wakati mwingine, mtafsiri aliongeza maelezo kupitia matumizi ya mabano, vishazi au matumizi ya tanbihi au kudondoa maelezo ambayo hayakuwa muhimu katika matini lengwa. Taratibu hizi ziliweza kutumika kwa wakati mmoja. Mbinu hii ilijulikana kama uunganaji. Mtafsiri alifaa aanze na utaratibu wa kisawe cha kitamaduni kabla ya kutumia mbinu nyinginezo.

Iwapo maelezo fulani hayakuwa na umuhimu katika matini lengwa ilikuwa bora kwa mtafsiri kueleza umuhimu huo katika matini chanzi. Matumizi ya lugha yalifungamana na maudhui na yalihusisha tamathali za usemi kama vile:- Sitiari, taswira, anafora, chuku, tasfida, kinaya, metonimu, balagha, takriri-konsonanti, takriri-irabu, mchezo wa maneno, onomatopeya, tashbihi, na mchanganyiko wa maneno. Pia yalihusisha sauti, vina na mahadhi ya kimuziki, uhuishaji, tanakali za sauti, udondoshi na mshabaha wa irabu za shadda katika maneno mawili au zaidi. Mfasiri hangeweza kuzipuuza lakini angeweza kuzipanga kutegemea aina ya shairi.

Katika mwalimu wa Kiswahili.com tarehe 23 Novemba (2017) kwenye makala "*Changamoto za kitamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa wakati wa kutafsiri*"waandishi waliwanukuu wataalam Nida (1964) aliyenukuliwa na Mwansoko na wenzake (2006: 31) na Newmark (1988: 95) kudokeza vipengele vya kiutamaduni vilivyosababisha changamoto katika tafsiri. Wataalam hawa walibainisha changamoto hizi katika makundi matano yaani: ekolojia, violwa, mila, desturi, siasa na dini. Waandishi hawa nao walibaini kuwa kipengele cha kisiasa kilijitegemea na hakiwezi kuingizwa katika katika utamaduni hivyo waliangazia makundi manne.

### 2.2.5 Kipengee cha Ujumi

Hariyanto (2018) alidokeza kuwa mojawapo ya mambo yanayoleta changamoto katika tafsiri ni suala la ujumi. Kulingana naye, ujumi huhusiana na muundo wa shairi, tamathali za usemi kama vile sitiari na sauti. Alisema kuwa ujumi hubeba maana huru. Hii ina maana kwamba, mtafsiri akivuruga uteuzi wa maneno, mpangilo wa maneno na sauti yeye huharibu urembo wa shairi asili. Mawazo haya yalishahibiana na yale ya mwanaisimu.

Laura(2016) tarehe 23 mwezi wa Februari katika makala yake "*What makes Poetry Translation different"* alidokeza kuwa masuala kama vile umbo la shairi, misemo na nahau, sauti na athari za kitamaduni za jamii husika. Alisema changamoto kwa mtafsiri ni kuweza kupata visawe katika matini lengwa vinavyoshabihiana na kutekeleza malengo sawa kama ilivyo katika matini chanzi. Alihitimisha kwa kusema kuwa ni muhimu kuelewa umbo la shairi na mtindo na umahiri wa kutambua madhumuni ya mwandishi kabla ya kutfsiri. Aliorodhesha vipengee hivi ambavyo ni muhimu kuzingatia kabla ya kutafsiri: mshabaha wa irabu za shadda katika maneno mawili au zaidi, takriri, mahadhi ya kimuziki, toni na hali, mtindo na umbo.

Khatibi (2016) chapisho lake lenye mada "*Challenges of Literary Translation"*: *Kahlil Gibran's the Prophet as a case study* alichunguza ni kwa kiwango gani tafsiri hudumisha ujumi wa matini chanzi na alipata kuwa kwa kiwango fulani tafsiri hizo ziliweza kudumisha ujumi lakini tafsiri moja ilikuwa na ubunifu zaidi kushinda mwingine. Arberry (1945: 22) alichunguza ugumu wa kutafsiri mashairi ya beti. Alisawazisha tafsiri za wizani na wanasarakasi wa michezo ya sarakasi ya, "kumwezesha ndovu kutembea katika kamba iliyokazwa." Kadhalika, alisema kuwa, kati ya washairi waliosifika, Sa'di ambaye ni mwajemi ndiye alikuwa mshairi aliyeweza kufanya wengi waelewe zaidi tafsiri za mashairi bila kupoteza uhalisi na ujumi. Mojawapo wa utungo wake maarufu ulifahamika kama "*Oneness of mankind.*" Mtindo wake ulijumuisha matumizi ya tamathali za usemi kama vile mchezo wa maneno, sitiari na mdokezo. Kutokana na maelezo haya ugumu wa kutafsiri mashairi ya beti ulipunguzwa na matumizi ya tamathali za usemi katika lugha lengwa.

Cudden (1976) alisema kwamba, kilichofanya ushairi kuwa tofauti na tungo nyinginezo ni matumizi ya kiinimacho ambapo usiri ulidumishwa kuhusu ni kwa vipi maneno yalivyojiegemeza kwa mengine na jinsi yalivyofungamana kuhusiana kuleta maana. Haya yalitokana na matumizi ya wizani yaliyoleta mahadhi ya kimuziki. Kwa upande mwingine, miundo mingine ya ushairi ilikuwa ni dhahiri katika tamaduni, nyanja na lugha aliyoitumia mshairi.

Kwa hivyo, udumishaji wa umbo na yaliyomo katika utafsiri wa ushairi ulielekea kuwa ngumu zaidi.Maelezo ya Cudden yalionyesha kuwa ilikuwa vigumu kudumisha wizani katika kutafsiri. Kulingana na Newmark (1981) thamani za kiujumi zilitegemea muundo wa ushairi, sitiari na sauti.

Muundo wa ushairi ulijumuisha mpangilio wa shairi, asili, umbo na urari wa sentensi katika kila mshororo.Newmark (1988: 162) alichunguza mbinu za kutafsiri. Alidokeza kwamba tafsiri za fasihi, "...ni aina tata zaidi ya tafsiri." Kadhalika, "thamani ya ujumi hutegemea muundo wa shairi, sitiari na sauti." Utafsiri wa ushairi uliweza kusawazishwa na mtihani wa asidi wa kuonyesha changamoto za kazi hiyo. Tunapata maoni ya Newmark yalishabihiana na yale ya Cudden kwa misingi ya muundo na wizani ambazo huchangia utata katika kutafsiri.

Nyerere (1996) alipotafsiri vitabu mbalimbali, alitambua ushairi kama mbinu mwafaka ya kuwafikia watu. Alitumia mfumo wa tenzi katika kutafsiri bibilia ili ujumbe uweze kukaririwa, kuimbwa na hivyo kubakia akilini mwa wasomaji. Nyerere alitumia istilahi za kidini zilizolandana na tamaduni ya jamii lengwa. Weston (1965), katika makala yake ya '*Law in Swahili-Problems in Developing National Language'*aliangazia matatizo ya kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya sheria nchini Tanzania. Alijadili changamoto za kiisimu ambazo watafsiri wa sheria walikabiliana nazo wakati wa kutafsiri sheria. Changamoto hizi ni kama vile:- kutafsiri kutoka kwa mfumo mmoja wa kisheria hadi mwingine, kujaribu kufuata kanuni ya neno moja tafsiri moja, yaani neno moja liwe na tafsiri moja pekee na kwamba istilahi nyingi zilikuwa zimeundwa kutokana na nahau za Kiingereza.

Vilevile, alionyesha mikakati waliyotumia kukabiliana na changamoto hizi. Mikakati hii ilikuwa ni kama vile kunyambua maneno yaliyopo katika lugha ya Kiswahili ili kupata maneno zaidi, uundaji wa maneno, kutumia maneno ya kawaida na kuyapa maana za kisheria. Aidha, kuumba maneno mapya ambayo hayakuwepo na kuchukua maneno ya kawaida katika lugha na kuyapa maana za kisheria, kutafsiri kwa njia ya maelezo na kukopa maneno kutoka lugha zingine. Vilevile, alionyesha ufanisi walioweza kuupata katika harakati za kutafsiri sheria.

Ufanisi huu ulikuwa, japo kutafsiri sheria si jambo rahisi wataalamu waliweza kutafsiri matini za kisheria za kutumiwa katika mahakama za kimsingi na wakaweza kutafsiri matini zingine za sheria za nchi.Makala haya ya Weston yalikuwa ya thamani kubwa katika huu utafiti kwa vile yalituelekeza katika kutimiza malengo yetu ya utafiti.Suala lingine lililopelekea kuwe na changamoto ya ujumi lilikuwa ni kutafsiri toni ya lugha chanzi. Toni ilikuwa ni msimamo wa mshairi kuhusu ushairi wake:Iwapo dhamira ilikuwa ni kuchekesha, kutilia chumvi, kutoeleza kikamilifu au kuonyesha ukweli wa mambo. Mfasiri alifaa kudumisha uwazi katika toni.

Aina hii ya tafsiri ilikuwa ni bora katika maandishi ya kubuni, kama alivyodokeza Newmark (1988). Hivyo, mfasiri alikuwa ni mpatanishi kati ya mshairi na msomaji. Ilimlazimu mfasiri ajaribu kutafsiri kulingana na muktadha na ujumi wa matini chanzi.

Iwapo ushairi ulitafsiriwa, mizani yake ilibadilika toni yake ilivurugwa na kivutio au uzuri wake ulipotea. Mtazamo huu ulitokana na dhana kwamba kila lugha ilikuwa na muziki wake na mapigo ya mizani mahsusi ya kishairi. Matini ya ushairi yalikuwa na thamani ya mahsusi ya kiujumi na kihisia. Utendakazi wa kiujumi ulikuwa ni kusisitiza urembo wa maneno, mbinu za lugha na sitiari.

Kwa upande mwingine, utendakazi wa kihisia uliweka wazi fikra na hisia za mwandishi. Mtafsiri alifaa ajaribu kadri awezavyo kupitisha hivi vipengee mahsusi kwa msomaji wa lugha lengwa. Tofauti na tanzu nyinginezo za fasihi, katika ushairi, ujumi haukufikiwa tu kwa uteuzi wa maneno tu na mbinu za lugha kama ilivyo katika hadithi fupi au riwaya. Kulikuwa pia na matumizi ya vina, mizani, mahadhi ya kimuziki na misemo na maumbo ambayo hayakupatana na lugha ya kawaida. Kwa ufupi, mfasiri alihitaji zaidi ya kutafsiri kazi za kifasihi katika tanzu nyinginezo.Kutokana na maelezo haya ni wazi kwamba mtafsiri alifaa atumie nguvu zake kadri awezavyo ili msomaji aweze kuelewa shairi hilo. Mfasiri alifaa atafsiri maana kulingana na jinsi alivyodhamiria mtunzi. Kulikuwa na hatari ya kulazimisha usomi wa mtafsiri wa lugha chanzi katika kufasili. Mtafsiri alilazimika abainishe kati ya maana rejelezi na maana ya kishairi. Ilimbidi azue athari kama ilivyokuwa katika lugha chanzi.

Kwa jumla, lugha ilitambulishwa na hali ya matumizi ya lugha sanifu, lugha tendaji na lugha ya kiufundi. Vilevile lugha iliyotumika katika shairi huwa si wazi. Hii ni kwa sababu ya matumizi ya maneno ya kawaida lakini maneno haya huwa na maana ya kishairi. Hali hii huhitaji msomaji wa matini za kishairi awe na uelewa wa kishairi ili kuweza kubaini kinachorejelewa. Lugha sanifu ya shairi ni lugha ambayo huhusishwa uumbaji wa kanuni, kuzalisha kanuni hizi na kuzionyesha kanuni hizo, yaani ni lugha elekezi.

### 2.3 Misingi ya Nadharia

Mwansoko (2006) alisema kuwa nadharia za tafsiri ndizo msingi wa kazi zote za kifasiri. Ni maelekezo juu ya vipengele anuai vya kifasiri vinavyopaswa kuzingatiwa katika kazi ya kufasiri.

Nadharia za tafsiri zilichunguza mbinu zilizofaa kutumika kufasiri kwa ufanisi matini ya aina fulani mahsusi.Dhima muhimu ya nadharia za tafsiri zilikuwa ni kuonyesha mbinu za tafsiri zilizofaa kutumiwa kufasiria aina mbalimbali za matini. Vilevile nadharia zilitoa msingi, kanuni, sheria na vidokezo vya kufasiri matini na kuhakiki tafsiri, yaani matini zilizokwisha tafsiriwa. Nadharia pia zilielekeza jinsi ya kushughulikia vipengee vidogovidogo kama vile maana na umuhimu wa vistari, italiki na makosa ya tahajia. Sababu tatu kuu zlizopelekea kuanzishwa kwa nadharia za tafsiri.

(a) Wingi wa makosa (ya kimuundo, kimaumbo na kimsamiati) katika tafsiri zilizokwisha chapishwa. Ilikuwa ni nadra sana kupata tafsiri nzuri zisizo na makosa.

(b) Kuwepo kwa idadi kubwa na inayozidi kuongezeka ya asasi zilizojishughulisha na kazi ya tafsiri.

(c) Mfumko wa istilahi katika taaluma mbalimbali, hasa sayansi na teknolojia na haja ya kuzisanifisha ili kuwezesha tafsiri baina ya lugha moja na nyingine kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mwansoko (2006) alielezea ushairikama utanzu uliotafsiriwa sana kutokana na malengo makuu mawili; lengo la kuigizwa na lengo la kusomwa. Pia umefasiriwa sana kutokana na kwamba, ulikuwa ni utanzu mpya katika Afrika, hivyo wageni na wenyeji walitafsiri kwa lengo la kuutambulisha katika mazingira ya kiafrika. Vilevile umeonekana kutafsiriwa sana kutokana na urahisi wa lugha yake, kwani ushairi ulitumia maneno machache na yaliyoeleweka tena bila hata ya ufafanuzi wa kina kama ilivyo katika riwaya. Pia umefasiriwa sana kutokana na umuhimu wa maudhui yake ambayo yalijibainisha katika masuala mtambuko duniani kote. *Wimbo wa Lawino* umetafsiriwa sana kwa lengo la kukuza na kueneza lugha adhimu ya Kiswahili, ambayo haikuwa na machapisho mengi yahusuyo fasihi andishi.

Kwa upande wa lugha zilizojitokeza zaidi katika kufanikisha suala la tafsiri ya fasihi ya Kiswahili ni lugha ya Kiingereza, na Kiswahili; lugha ya Kiingereza imejitokeza sana katika tafsiri kutokana na kwamba, waingereza ni moja kati ya mataifa yaliyotawala sehemu kubwa ya dunia, na ndio taifa lililokuwa na dola yenye nguvu zaidi. Vilevile waingereza walishapiga hatua kubwa katika maendeleo ya fasihi wakilinganishwa na mataifa mengine. Pia hata lugha ya Kiingereza ni moja kati ya lugha kubwa duniani na inayofahamika na mataifa mengi (Beaugrande, & Dressler, 1981).

Lugha ya Kiswahili nayo ilionekana kutafsiriwa sana kutokana na hitaji la kuwa na machapisho mengi ya kifasihi ili kukuza na kueneza fasihi ya Kiswahili. Pia ni lugha inayokua kwa kasi na iliyoeleweka sana Afrika Mashariki ikilinganishwa na lugha nyingine.Pamoja na hayo yote, bado ilionekana kuwa, ushairi ni utanzu uliokabiliwa na changamoto nyingi zaidi katika kufasiri kutokana na kwamba, kwa kiasi kikubwa ushairi ulitumia lugha ya mkato na ya kisanaa zaidi yenye msamiati mgumu uliosheheni taswira, ishara, lahaja, tamathali za semi pamoja na misemo na mafumbo.

Hivyo basi, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kupotosha maana ya kifasihi pamoja na sanaa iliyomo katika utanzu huu.Licha ya hayo, vilevile ugumu ulisababishwa na kanuni za kiarudhi hasa katika mashairi ya kimapokeo kwani, ilikuwa ni vigumu sana kutafsiri ushairi huku ukizingatia urari wa vina na mizani bila kupotosha maana iliyokusudiwa. Hivyo basi, ili kuepuka changamoto hizo ingefaa sana mfasiri aliyefasiri utanzu huu awe mahiri kwa lugha zote mbili. Pia awe mtu mwenye upeo mkubwa katika uwanja huu na mwenye ujuzi mkubwa wa kutunga mashairi au naye awe kiasi fulani msanii. Hivyo haitamwia vigumu sana katika kuteua maneno mwafaka .

Kutokana na maelezo haya mfasiri alifaa awe mkwasi katika lugha zote mbili na awe na uzoefu wa kutathmini kazi ya ushairi. Leech (1969) alieleza kwamba baada ya kuangalia tathmini ya mapitio hayo,uchambuzi wa tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ulifanywa kwa mwongozo wa nadharia ya usawe wa aina matini.kulingana na Newmark (1982) matini yoyote ile ifasiriwe kwa kuzingatia aina yake. Hii ina maana kwamba, kazi iliyotokea ilifanana na matini chanzi. Vilevile mbinu ya "Ulinganishaji Matini" ilitumika katika kufanya uchambuzi wa kazi teule, kwani katika mbinu hii matini lengwa ililinganishwa na matini chanzi ili kubaini vipengele vya kifani na kimaudhui vilivyoongezwa, vilivyopunguzwa na vilivyopotoshwa.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya isimu (Isimu matini) na nadharia ya mawasiliano (uchanganuzi wa usemi). Mwelekeo wa kiisimu katika nadharia ya tafsiri ulizingatia maana, kisawe na uhamishaji na ilianza miaka hamsini iliyopita na kazi za Chomsky (1965) za Isimu muundo.Wengine kama, Leech (1969), Dijk (1972) na Beaugrande na Dressler (1981) waliendeleza nadharia ya isimu matini.

Hapa, ilitambulika kwamba, matini za kishairi zilikiuka kanuni za sarufi na maana na ilibidi kuwe na operesheni ya kimaandishi katika sauti sintaksi na maana. Operesheni hizi zilihusisha: ujumlishaji, udondoshaji na ubadilshanaji wa maneno. Katika tafsiri, changamoto za nadharia ya kiisimu zilikuwa ni matumizi yake ya usemi kiufundi. Hapakuwa na tafsiri iliyokuwa kamilifu hata kama palikuwa na matumizi ya visawe. Nadharia yao haitilii maanani tu matini,bali mwandishi na hadhira lengwa. Pia huchunguza thamani ya matini husika.

Walioendeleza nadharia hii kama vile Hariyanto (2015) aliandika makala yenye anwani,"*Text linguistics and Skopos Theory and their Application in Translation Teaching*" Alidokeza kuwa, isimu matini ni tawi la isimu linalojishughulisha na matini kama mifumo ya mawasiliano. Isimu matini hutilia maanani umbo la matini na muktadha wake, yaani jinsi ilivyotumiwa katika muktadha wa maingiliano na mawasiliano. Katika tafsiri alisema kuwa tafsiri sio tu shughuli ya kuchanganua matini asili uchanganuzi wa.sentensi baada ya sentensi usitiliwe mkazo bali mtafsiri, hadhira lengwa na lengo la mawasiliano.

Uchanganuzi wa usemi ulianza na kazi za Firth (1951) ambapo alidokeza maelezo kuhusu maana. Alisema kwamba, maana katika lugha yalidhihirika kupitia muktadha wake wa hali. Hata hivyo hakuhusisha umbo na maana. Uchanganuzi wa usemi ulichunguza ni kwa vipi matini iliwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi kwa msomaji. Walioendeleza nadharia hii ni kama vile:- Zhang (2015) katika makala yake yenye mada: "*Introduction to Discourse Analysis in Translation Studies*. Alimnukuu Palridge (2012: 1) aliyesema,katika tafsiri uchanganuzi usemi huangazia ruwaza ya lugha katika matini na hutilia maanani uhusiano baina ya lugha na muktadha wa kijamii na kitamaduni ambamo inatumika.

Nadharia hii ilichanganua jinsi lugha ilivyotumiwa sio katika kiwango cha neno na sentensi bali katika kitengo cha usemi. Lugha na na usemi zilichukuliwa kama vitendo vya kibinadamu vya kuwasilisha ujumbe katika muktadha mahsusi. Tulipata kwamba habari ziliwasilishwa katika kutuma na kupokea kwa njia mbali mbali lakini ilihusisha isimu. Hii ndio maana waandishi wengine walitambua uchanganuzi usemi kama isimu matini.

Beaugrande na Dressler (1981) walisema kwamba matini ilikuwa ni tukio la kimawasiliano lenye mihimili saba ya kimatini:

**Mshikamano**: Sehemu hii ilionyesha jinsi vipengee vya matini vimeunganishwa.

**Mwendelezowamshikamano**: Sehemu hii ilionyesha jinsi vipengee hivi vilihusiana na kuingiliana.

**Umakinifu**: Sehemu hii ilionyesha ni kwa vipi mtoaji ujumbe alivyodhamiria kuwasiliana ili malengo yake yatimizwe.
**Ukubalifu**: Sehemu hii ilionyesha ukubalifu wa matini kwa msomaji ( Je, ataielewa matini? Kwa kiwango kipi? Sehemu hii ilitegemea mwendelezo na mwendelezo wa maana ya matini.
**Ujulishaji**: Sehemu hii ilionyesha kiwango cha mawasiliano: kilichotarajiwa / hakikutarajiwa, kilichojulikana / kile ambacho hakikujulikana.
**Muktadha**: Sehemu hii ilionyesha kile kilichofanya matini ieleweke. Yaani, ilieleza madhumuni ya matini.
**Uhusianokatiyamatini**: Sehemu hii ilionyesha ni kwa kiwango kipi matini ilitegemea ufahamu wa matini nyingine iliyosomwa.Kipengele cha kwanza cha mshikamano kilifanya kazi ya kujumuisha matini kileksia na kisemantiki ili kujenga umoja wa matini.

Katika mawasiliano sintaksia ilikuwa na kazi ya kujenga ruwaza za matini kijuu juu. Yaani, matini ilikuwa na mshikamano iwapo vipengee vya kijuu juu vya matini vilikuwa vimeunganishwa kwa kufuata utaratibu fulani. Jambo hili liliwezekana kupitia ishara tano za mshikamano: marejeo, vibadala, udondoshaji wa maneno,viunganishi na mshikamano wa kileksia. Mshikamano ulifanya mwendelezo wa mshikamano kuwa dhahiri kiisimu. Kwa ufupi, mshikamano ulikuwa matokeo ya tafsiri.Mwendelezo wa mshikamano ulikuwa kipengele cha pili. Mwendelezo huu wa maana ulihusisha mpangilio wa mawazo na mahusiano ya matini ilikuwa imeshikamana na matini kijuu juu. Mwendelezo huu wa maana ndio ulikuwa msingi wa mwendelezo wa mshikamano. Msingi huu ulitokana na upangaji wa dhana na mahusiano yaliyoelezwa pamoja na mwonolimwengu wa mpokeaji ujumbe. Katika tafsiri, kipengele hiki kilihusisha ni kwa vipi matini ilipata kueleweka na wasomaji kupitia mpangilio wa matini, uhusiano na uelewano wa mawazo na dhana. Mwendelezo huu wa maana ulipokatizwa, madhumuni ya mawasiliano katika matini yalipata kuathiriwa.

Kwa ufupi, mwendelezo wa mshikamano ulikuwa ni fasiri ya matini kwa upande wa msomaji. Umakinifu na ukubalifu ulihusisha ni kwa vipi ujumbe ulitolewa kwa misingi ya mshikamano na mwendelezo wa mshikamano. Hii ilikuwa na pamoja na matumizi ya vitendo neni vya Grice. Hii ni kwa mujibu wa Maaitah (2017) katika makala yake "Pragmatics". Mwandishi wa matini alifaa ahakikishe kuwa matini yake ilichangia madhumuni fulani na msomaji apate kuikubali matini hiyo. Hata hivyo, haikuwa lazima kwa mpokeaji habari kuamini maelezo mahsusi ya matini hiyo. Alifaa atambue aina ya matini aliyothamiria mtuma ujumbe na madhumuni ya matini hiyo.Kipengee cha ujulishaji kilihusishwa na matini

ambapo matukio katika mfumo wa lugha yoyote ile yalifaa yawe ya kuarifu. Kazi ya mtafsiri hapa ilikuwa kumhusisha msomaji na taarifa katika matini. Tofauti za kileksia na kisintaksia katika lugha mbili zilipelekea kuwe na mabadiliko katika mpangilio wa usambazaji wa maelezo katika tafsiri.

Wakati mwingine, ilimlazimu mtafsiri kutumia tanbihi au kutoa maelezo zaidi ili apate kujulisha msomaji.Kipengee cha hali nacho kilionyesha ni kwa vipi madhumuni ya mawasiliano yalivyohusishwa na hali. Kulikuwa na kuhusisha matini na muktadha wa kiisimu jamii. Hapa wakati na mahali mahsusi ya uandishi wa matini chanzi ziliathiri tafsiri. Ilimbidi mtafsiri kubadilisha hali katika matini lengwa huku akidumisha utendakazi na madhumuni ya matini chanzi.Kipengee cha mwisho kijulikanacho kama uhusiano kati ya matini kilionyesha matini ambayo ilikuwa na sifa sawa na matini nyinginezo.

Kipengee hiki kilihusisha masuala yaliyowawezesha wasomaji kubainisha sehemu za matini nyinginezo katika matini husika. Msomaji hapa alikuwa na matarajio fulani kuhusu ufaafu wa matini hiyo. Kwa mujibu wa ruwaza za kiulimwengu. Mtafsiri alifaa adumishe masuala ya kisemantiki, kisintaksia na kipragmantiki katika tamaduni ya matini lengwa. Kwa muhtasari vipengee katika mawanda madogo na makubwa vilichunguzwa. Hivi vilikuwa ni: vipengee vya kiisimu (mpangilio wa maneno, vishazi, n.k), vipengele vya ziada vya kiisimu (wakati, mahali, umbo, njia ya uwasilishaji na umbo la matini) na vipengele kama vile uakifishaji, toni, mtuo, nyanja na vitendo neni.

Hivyo basi, utafiti huu ulihusisha masuala ya isimu matini katika nadharia ya isimu na uchanganuzi wa usemi katika nadharia ya mawasiliano. Katika Isimu matini mtafiti aliongozwa na vigezo hivi:

i. **Umbo** (Muundo wa kisintaksi)

ii. **Yaliyomo** (Mwendelezo wa maana)

Nadharia ya mawasiliano ilifaa hasa katika kudokeza kwa uwazi masuala ya kitamaduni ambayo hayakuweza kuelezwa kwa kutumia nadharia ya kiisimu. Utafsiri mwafaka ulibainika pindi tu mtafsiri angefasiri tamaduni ya jamii husika. Hapa nadharia ya mawasiliano ilijaza pengo la kukidhi mahitaji ya tamaduni katika tafsiri. Katika tafsiri kulikuwa na aina tatu za tofauti za kitamaduni:

i. Migogoro halisi kutokana na maelezo ya kitamaduni yasiyotambulika.
ii. Migogoro ya kirasmi kwa sababu kila tamaduni ilikuwa na sintaksia mahsusi na matini mahsusi.
iii. Migogoro ya kisemantiki kutokana na mahusiano mahsusi ya tamaduni.

Mtafiti alikuwa na jukumu la kuonyesha mawasiliano baina ya wasomaji katika lugha chanzi na lugha lengwa. Umbo, yaliyomo na maana zilihusiana katika tamaduni mahsusi lakini zilkuwa tofauti katika tamaduni tofauti.

Nadharia ya mawasiliano (uchanganuzi wa usemi) ilifaa zaidi kujumuishwa na nadharia ya kiisimu (isimu matini) katika ushairi kwani, ushairi ulikuwa ni utaratibu wa kazi za usemi na sio maneno. Hapa masuala ya muktadha yalitiiliwa maanani.

Katika tafsiri miktadha iligawika katika mawanda matatu:

i. **Muktadhawakitamaduni** – Nje ya lugha
ii. **Muktadhawahali**- Nje ya lugha
iii. **Muktadhawakiisimu** (ushiriki wa matini) – Ndani ya lugha

Kulikuwa na uhusiano wa karibu kati ya lugha na muktadha. Muktadha uliamuliwa na ulijengwa na uteuzi wa lugha mahsusi. Kwa upande mmoja lugha ilichukuliwa kama mfumo, vipengee vyake vya kileksia na kategoria zake za kisarufi zilihusiana na muktadha wake wa kitamaduni. Kwa upande mwingine, matini mahsusi na vipengele vyake vilihusiana na muktadha wake wa hali.

Muktadha wa utamaduni ulihusiana na utanzu, muktadha wa hali ulihusiana na rejesta na ushiriki wa matini ulihusiana na usemi wenyewe.Matini katika lugha tofauti iliweza kuwa na visawe katika vitengo tofauti (kamili/ kiasi kutokana na muktadha wa kisemantiki wa sarufi ya kileksia) na tofauti katika kategoria za neno kwa neno, vishazi kwa vishazi na sentensi kwa sentensi. Hili lilipelekea kupotea kwa dhana mbalimbali katika tafsiri (Suala la ujumi). Hii ni kwa vile mtafsiri alijiuliza ni mambo yapi adumishe na ni yapi adondoe. Hivyo mtafsiri alilazimika kuegemea katika muktadha wa kitamaduni na muktadha wa hali. alifanya hivi kupitia lugha (Suala la matumizi ya lugha) kwani lugha iliakisi tamaduni kupitia masuala kama msamiati, sintaksia na jinsi dhana zilivyopangwa (Suala la isimu). Kwa muhtasari rejelea kielelezo cha dhana:-

**2.4 kielelezo cha dhana**

**ISIMU MATINI**
(umbo na yaliyomo)
Mfuatano wa kitaratibu
Utofauti wa kiisimu katika lugha mbili

→

**UCHANGANUZI USEMI**
(lengo na ukubalifu)
Utofauti wa kimtindo kati ya lugha mbili

→

**HALI KATI YA MAANDISHI**
(masuala ya kitamaduni jamii)Masuala ya ujumi

**Jedwali 1: Kielelezo cha kidhana**

| | | |
|---|---|---|
| Vipengele vya uchanganguzi<br>1. Muundo wa sauti na maneno mahususi<br>2. Maumbo tofauti ya silabi<br>3. Sentensi kamilifu (mishororo) | Utofauti wa kimtindo<br>1. Uteuzi wa lugha<br>2. Utendaji wa usemi (marudio ya silabi sitiari,kinaya n.k) | Muktadha<br>1. Hali ya kitamaduni jamii<br>2. Utendakazi<br>3. Maana-mfuatano wa utaratibu (jinsi mishororo inahusiana kuleta athari-ujumi) |

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sehemu hii ilihusisha vipengee vifuatavyo: muundo wa utafiti, kikundi lengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data. Utafiti huu ulijumuisha masuala ya kiuthamano katika uchanganuzi elezi wa matini. Mkabala wa kiulinganishi ulizingatiwa kwa kurejelea vitabu viwili: *Song of Lawino* (Okot P' Bitek) kama matini chanzi na *Wimbo wa Lawino* (Paul Sozigwa) kama matini lengwa.

### 3.2 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Babbie (1992) muundo wa utafiti ni mpango na mpangilio wa hali katika ukusanyaji wa data pamoja na uchanganuzi.Naye Willis (2017) kwenye chapisho lake wenye mada"*How to Define Research Design*" anasema kuwa muundo wa utafiti ni jinsi mtafiti ameweka pamoja suala la utafiti kujibu maswali.Sehemu hii ilitoa maelezo kuhusu ni kwa vipi data zilikusanywa na kuchanganuliwa. Sehemu hii ilisaidia kujibu maswali ya utafiti.

Hapa mtafiti aliongozwa na maswali ya utafiti.Muundo wa utafiti ulikuwa ni uchanganuzi elezi. Uchanganuzi elezi hutumiwa kuchanganua kuwepo na maana na mahusiano ya maneno na dhana katika matini kisha kueleza matokeo kuhusu ujumbe, waandishi, wapokezi ujumbe na hata utamaduni na kipindi cha matini husika. Utafiti huu ulichunguza changamoto za kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi katika kutafsiri ushairi kutoka Kiingereza "*Song of Lawino*" hadi Kiswahili "*Wimbo wa Lawino.*"

Mtazamo wa utafiti huu ulikuwa wa kiuthamano, wa kimaelezo kwa kulinganisha na kulinganua mashairi ya Kiingereza na Kiswahili na pia kwa kutazama muktadha ambamo maneno yalitumika kulingana na maswali ya utafiti. Kwanza mtafiti alibainisha maswali ya utafiti na malengo ya utafiti . (Rejelea sura ya kwanza sehemu ya 1.3 na 1.4 ). Kisha mtafiti alipitia maandishi ili apate ufahamu wa dhana na matini ya ushairi. Katika kupanga muundo wa utafiti, mtafiti ndiye alikuwa mhusika mkuu wa kukusanya data.

### 3.3 Kikundi Lengwa

Kikundi lengwa kilihusiha mashairi kumi na tatu katika wimbo wa Lawino ambapo mtafiti aliteua vipengee vya kiisimu, vya matumizi ya lugha na vya kiujumi. Hapa vipande vya mashairi kutoka matini asili na matini pokezi vilitumika kufafanulia maelezo. Data iliwasilishwa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

### 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni kiwakilishi cha kipande cha kikundi kinachoitafitiwa na mtafiti ili aweze kupata maelezo na kutoa muhtasari (Gay, et al.,2006). Cherry (2018) katika chapisho lake kwenye mtandao wenye mada"*Sample Types and Errors in Research*" alisema kuwa sampuli ni kitengo cha idadi kinachotumiwa kuwakilisha kikundi chote kizima. Sampuli haikuchaguliwa kiholela bali ilikuwa ya kimakusudi na ilizingatia maswali ya utafiti kwa kuzingatia vipengee vya kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi. Mtafiti alitumia vitabu viwili, " *Song of Lawino*" na "*Wimbo wa Lawino*."Mtafiti alishughulikia mashairi yote kumi na tatu katika usampulishaji. Hapa idadi ya sampuli haikuathiri umuhimu au thamani ya utafiti kwa sababu hakuna mwongozo wa kubaini idadi halisi ya sampuli katika utafiti wa kiuthamano. Sampuli ilibadilika kulingana na kiwango na aina ya kipengee kilichotafitiwa. Usampulishaji uliendelea hadi mahali ambapo maelezo mapya yaliyokusanywa yalionekana kukolea. Usampulishaji ulihusisha mgao uliowakilisha idadi nzima ya kilichotafitiwa.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Data iliyokusanywa ilikuwa ni vipengele vya kiisimu, vya matumizi ya lugha na ujumi kutoka mashairi katika kitabu, Wimbo wa Lawino cha Sozigwa (1975), ambacho ni tafsiri ya Song of Lawino cha Okot P' Bitek (1972). Data za msingi na zile za upili zilitumika katika utafiti. Data za msingi zilitolewa moja kwa moja kutoka kitabu cha wimbo wa lawino (Okot P' Bitek) kama matini chanzi na *WimbowaLawino* (Paul Sozigwa) kama matini lengwa. Data hizi zilibukia masuala ya kiisimu, matumizi ya lugha na Ujumi. Data za upili nazo zilikusanywa kwa kusoma maktabani. Mtafiti alijikita katika kusoma vitabu, tahakiki, makala na majarida mbalimbali kuhusu tafsiri kwa jumla. Mbinu ya utafiti ilikuwa uchanganuzi elezi wa matini. Mtafiti alisoma vitabu viwili teule. Pia utafiti wa maktabani ulitumiwa katika kupata yale ambayo yamekwisha fanywa kuhusu mada na pia yahusuyo nadharia zilizotumika katika utafiti.

Aidha, mtafiti alitumia vyombo vya utafiti kama vile majarida ya utafiti, makala na tasnifu zilizoandikwa kuhusiana na tafsiri halafu alitumia mtandao ili apate maelezo zaidi kuhusu tafsiri. Baada ya kusoma aliteua vipengele vya kiisimu, vya matumizi ya lugha na vya ujumi katika mashairi mahsusi. Alifanya hivi kwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa kabla ya kutoa kauli yake kutokana na uchanganuzi wa matini. Zana za utafiti zilikuwa ni kalamu na karatasi. Mtafiti alitumia kalamu na karatasi kuandika data mbalimbali alizozipata katika utafiti wake. Mtafiti alikuwa akisoma kwa makini vitabu teule kasha kudondoa sifa alizohitaji kulingana na maswali ya utafiti.

### 3.5.1 Utaratibu wa Kukusanya Data

Utaratibu wa kukusanya data kutokana na sampuli ni mchakato unaotumiwa kuteua vipengee vya idadi inayolengwa kwa njia ambayo inawakilisha sifa mahsusi ya ya idadi jumla(cohen et al., 2000) Utaratibu ulikuwa ni kama ifuatavyo:-

**a.** Kusoma mashairi yote kumi na tatu kwa Kiingereza na Kiswahili

**b.** Kukusanya sampuli kwa kubainisha changamoto za kiisimu kwa kutumia nadharia ya isimu matini ambapo kulikuwa na mihimili saba ya kimatini: Mshikamano, mwendelezo wa mshikamano, umakinifu, ukubalifu, ujulishaji, muktadha na uhusiano wa matini. Mtafiti pia alifuata mikakati ya Leech (1969) kubainisha ukiukaji wa kiisimu kwa kubainisha ukiukaji wa kigrafolojia, kifonolojia, kileksia, kisarufi, kisemantiki, kilahaja, kisajili na ukiukaji wa kipindi cha kihistoria.

**c.** Kubainisha changamoto za matumizi ya lugha (Tamathali za usemi,imani,thamani, taasisi, misimu na majina, ngoma, mavazi, nyimbo, vifaa, ala za kimuziki, ekolojia, flora na fauna) na ujumi (kwa kurejelea masula ya kiisimu na matumizi ya lugha) kwa kutumia nadharia ya mawasiliano.

**d.** Kufasili na kutathmini matokeo kwa kutoa maelezo na kutumia majedwali na kulinganisha mashairi haya mawili kwa kubainisha changamoto za kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi. Uchanganuzi wa kiuthamano ulitumika zaidi kutoa maelezo.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alidondoa sehemu ambazo mtafiti alihitaji katika mashairi kumi na tatu (vipengee vya kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi). Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kufafanua na kubainisha iwapo masuala ya kiisimu, kiujumi na matumizi ya lugha yaliathiri tafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Uchanganuzi wa matini ulianza na uchunguzi wa umbo la shairi. Masuala kama vile muundo wa shairi, beti, uakifishaji na aina ya shairi.

Pia mtafiti alichunguza sauti katika shairi. Hapa masuala ya mahadhi ya kimuziki yalipigwa darubini kwa kutilia mkazo uradidi wa konsonanti, vokali, usambamba, shadda na kiimbo. Kadhalika, maneno yaliyotumika yalichunguzwa na mtafiti alionyesha ni maneno yapi yaliyodondolewa, kuongezwa, kubadilishwa na jinsi yalivyoathiri utafsiri. Mtafiti pia alitazama sifa za kiisimu kama vile vitendo neni, tashbihi, istiari na mwisho alitazama vipengee vya ujumi kama vile toni na uteuzi wa maneno kama vile maneno ya kitamaduni katika kuleta ujumbe. Aidha mtafiti aliangazia baadhi ya udhaifu wa mtafsiri.

### 3.6.1 Mbinu za kuchanganua data

Data zilichanganuliwa kwa kutumia vigezo vya maswali ya utafiti. Mifano ya uchanganuzi wa changamoto za kiisimu:Katika kiwango cha utambuzi wa umbo kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojia uliohusisha utofauti wa idadi ya mishororo na alama za uakifishaji, hapa ujumi uliathiriwa kama ifuatavyo: Rejelea kiambatisho 1 na 2A.

| MATINI CHANZI | MATINI LENGWA | MATOKEO |
|---|---|---|
| 1.***My husband's tongue is bitter***<br>**Aina**: Huru | 1.**Ulimi wa mume wangu ni mkali**<br>**Aina**: Huru | Ilidumishwa |
| **Muundo**: Ruwaza sahili | **Muundo**: Ruwaza sahili | Ilidumishwa |
| Ubeti 1: Mishororo 14 | Ubeti 1: Mishororo 15 | Haikudumishwa |
| Ubeti 3 : Mishororo 4 | Ubeti 3: Mishororo 5 | Haikudumishwa |
| Ubeti 5:Mishororo 4<br>**Uakifishaji**: Ubeti 1<br>. (1) , (3) ;(1)<br>Ubeti 3<br>, (2) ! (2) | Ubeti 5: Mishororo 7<br>Ubeti 1<br>(3) , (2) (1)<br>Ubeti 3<br>, (2) ! (1) ; (1) | Haikudumishwa<br><br>Haukudumishwa<br><br>Haukudumishwa |

Mfano wa ukiukaji wa kifonolojia ili kuleta mahadhi ya kimuziki (Rejelea kiambatisho 2-A

| | |
|---|---|
| Kiingereza | |
| Konsonanti | Mifano |
| /n/ | **N**ow, i**n**herited, au**n**t, so**n** |
| **/s/** | **s**tupidity, **s**pite, **s**on, thing**s, s**ay |
| Vokali | Mifano |
| /a/ | Husb**a**nd, **a**nd, **a**unt |
| /e/ | m**e,** b**ee**n, b**e**cause l**e**ft |
| Kiswahili | |
| Konsonanti | Mifano |
| /s/ | **s**a**s**a |
| /n/ | u**n**a**n**idharau |

Hapa takriri konsonanti na takriri irabu zimetumika kupamba lugha ya shairi ili iweze kuvutia kwa msomaji au msikilizaji. Pia inaleta mlingano wa sauti unaoibua athari za kimuziki zinazovutia au pia kusisitiza ujumbe. Hata hivyo mahadhi ya kimuziki yaliathiriwa katika tafsiri kwa sababu ya tofauti za sauti na mifumo katika lugha hizi mbili; kwa kiasi fulani idadi za mishororo ilikuwa ni tofauti.

Mfano wa ukiukaji wa kisarufi kutokana na uradidi wa maneno:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| **Youare** now a man | Sasa **wewe** ni mtu mzima |
| **Youare** not a dead fruit | **Wewe** si embe mbovu |
| **HesaysIam** rubbish | Anasema **mimini** takataka |
| **HesaysIam** primitive | Asema **mimini** mshamba |

Ukiushi wa kisintaksia na kisarufi pia ulijitokeza kwa kudondoa kiunganishi ambacho kingetumika na pia kwa kutumia mifano zaidi ya moja kurejelea kitu kimoja.Angesema 'anasema mimi ni takataka na mshamba' badala ya kurudia 'anasema.' Aidha, kudondoa kiambishi 'na' katika mshororo wa nne wa tafsiri ya Kiswahili kuliathiri uradidi uliodhamiriwa kusisitiza ujumbe katika matini chanzi.Pia hapa kuna ukiushi wa kifonolojia ambapo kiambishi 'na' kimedondolewa katika neno 'asema" Alifanya hivi ili kupamba lugha ya ushairi. Aidha ukiushi wa kileksia ulitokea wakati alipotoa kisawe cha '***dead fruit'*** kuwa 'embe mbovu'.

Alitumia neno '**embe'** ili aweze kuifikia hadhira lengwa ambao walikuwa na uzoefu wa kula embe ikilinganishwa na matunda mengine .Mtafsiri angesema **tundabovu** ili kudumisha maana asili.

Katika kuchanganua changamoto za matumizi ya lugha kulikuwa na maneno ambayo yaligeuzwa maana yao ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Hapa kulikuwa na ukiushi wa kisemantiki kupitia tamathali za usemi ambazo zilifungamana na tamaduni za waacholi.

Hizi mbinu zililazimishwa katika tamaduni ya matini lengwa.Wakati mwingine ilimbidi mtafsiri kutumia tanbihi ili kutoa maelezo zaidi au pia alijaribu kutafuta visawe au kudondoa maneno hayo. Changamoto ya matumizi ya lugha yaliathiri pia thamani ya tamathali hizo za usemi katika matini lengwa.

Kwa kuangazia sitiari kwenye anwani :

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| The ***Graceful*** Giraffe cannot Become a Monkey | Hawezi twiga kuwa nyani (Kiambatisho 2-E) Dhana ya Graceful ilipotea katika matini lengwa hivyo kuathiri thamani ya sitiari hiyo. Mtafiti angetumia neno "**mwenye neema"** kudumisha maana asili. |

Katika kuchanganua changamoto za ujumi ukiushi wa kisajili ulijitokeza kwa matumizi ya sajili ya siasa katika kiambatisho 2-K ubeti wa nne,maneno kama **uhuru** na **amani** yalitumika. Hata hivyo shairi hili lilikuwa na mashiko zaidi kwa hadhira ya matini chanzi kwani mfumo wa kisiasa uliwalenga waganda ambao walifahamu zaidi vyama va '**Democratic Party'** na **Uganda Peoples Congress'**hivyo iliathiri jazba aliyonuia mshairi wa matini chanzi kwa hadhira yake katika kipindi hicho cha kihistoria. Hapa ujumi uliathiriwa. Japo aliweza kudumisha umbo la shairi huru hakuweza kudumisha idadi ya miishororo hivyo kuathiri muundo wa shairi. Toni pia ilibadilika alipojumuisha mshororo wa kwanza na wa pili.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DATA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii iliangazia matokeo ya utafiti huu kulingana na maswali ya utafiti. Iliangazia matokeo ya kiisimu, matumizi ya lugha na matokeo ya ujumi. Baada ya kusoma na kuchanganua vitabu viwili teule ambavyo ni *Wimbo wa Lawino* cha Sozigwa (1975), ambacho ni tafsiri ya *Song of Lawino* cha Okot P' Bitek (1972) mtafiti alipata matokeo kulingana na kubainisha vipengele vya kiisimu, vya matumizi ya lugha na ujumi kutoka mashairi katika vitabu hivyo.

### 4.2 Kubainisha Changamoto za Kiisimu

Balikumi (2017) alisema kuwaIsimu ni sayansi inayochunguza lugha kama mfumo wa sauti, ambao huwasilisha maana, huku ukitawaliwa na sheria za kisarufi. Lazima maana iwasilishwe pia ikubaliwe na wenyeji wa lugha. Naye Okere (2018) aliangazia changamoto za kiisimu katika ushairi kwa kuangazia aina mbalimbali za ukiushi kama ilivyoelezwa na leech (1969) kama vile ya kigrafolojia, kisintaksia na kileksia.Katika kiwango cha utambuzi wa umbo tulitalii shairi kwa misingi ya grafolojia (maandishi) na fonolojia (matamshi). Grafolojia ilihusisha kanuni zote za uandishi. Kimaandishi tulipata kwamba lugha hizi mbili zilikuwa tofauti kwani kila lugha ilikuwa na mfumo wake. Lugha ya Kiingereza ilikuwa ya mfumo funge ilhali ya Kiswahili ilikuwa ya mfumo wazi.Kadhalika, Kiswahili tofauti na Kiingereza kilikuwa ni lugha ambatanishi. Lugha ya Kiingereza ilifuata mfumo wa unyumbuaji. Jambo hili lilipelekea kuwe na athari katika wizani au mita hivyo muundo wa mishororo ulibadilika katika baadhi ya beti.

Mtafsiri alidumisha umbo la mashairi ambao ulikuwa huru. Kulikuwa na udumishaji wa mistari mishata (isiyokamilika) na mistari kifu (iliyokamilika) katika tafsiri. Rejelea kiambatisho 2-A hadi M. Kwa kurejelea kiambatisho 2-A: Mkao wa fonti katika shairi la matini chanzi yaKiingereza ulikuwa tofauti na ule wa Kiswahili. Idadi ya mishororo katika shairi la Kiingereza ilikuwa ni kumi na nne na Kiswahili kumi na tano. Katika uakifishaji kulikuwa na utofauti ambapo shairi la Kiingereza halikuwa na alama ya kipumuo na kituo mwishoni mwa mishororo miwili ya kwanza. Hata hivyo katika Kiswahili kulikuwa na alama hizo mwishoni mwa mishororo hiyo. Katika kipengele cha vina, shairi la Kiingereza lilikuwa na urudiaji katika vina vya mwisho katika mishorori ya kwanza, tano, sita, nane na tisa vikiishia na –me (rejelea kiambatisho 2-A na kiambatisho 3).

Katika Kiswahili ruwaza hii ilibadilika na badala yake kulikuwa na uradidi katika mishororo ya nne, tisa, kumi na mbili na kumi na tatu ambapo uradidi ulikuwa mwanzoni mwa mishororo hiyo. Kwa ujumla kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojia ambapo katika shairi la Kiingereza kingo za mishororo katika upande wa kushoto hazikuwa sambamba kama ilivyokuwa katika tafsiri ya Kiswahili.Kando na sifa hizi, kulikuwa na pia sifa za kiisimu za lugha ya shairi. Sifa hizi ziliweza kubainishwa kama sifa za kileksia, kisintaksia, kipragmatiki na kimtindo. Sifa moja bainifu ya kileksia ya lugha ya shairi ni msamiati changamano na wa kipekee uliopatikana katika lugha hizi tofauti. Sifa hii ya kiisimu ndiyo iliyoonekana sana katika lugha ya kishairi kama lugha ya kiufundi. Msamiati wa kishairi katika kila lugha ulikuwa mpana mno.

Kwa sababu ya tofauti za mifumo ya lugha, istilahi nyingi za shairi katika lugha moja hazikuambatana na istilahi katika lugha nyingine. Sifa hii ilileta tatizo la ulinganifu wa kiistilahi jambo ambalo lilikuwa tatizo kubwa katika kutafsiri. Katika kila msamiati wa kishairi kulikuwa na upekee ambao haukulinganakatika lugha hizi mbili. Sifa muhimu ya sintaksia ya lugha ya shairi ilikuwa ni mtindo wa uandishi ulio rasmi na usiohusishwa na mtu maalumu. Kulikuwa na upekee wa kisintaksia katika kila lugha ya shairi. Kwa mfano, Kiingereza kilitumia miundo changamani, usemi taarifa, vishazi vihusishi na vikanushi vingi. Hivyo tafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine iliyo na miundo tofauti ya kisintaksia ilileta changamoto.

### 4.2.1 Kiwango cha sauti katika lugha husika

Hariyanto (2018) alidokeza kuwa mojawapo ya mambo yanayozua utata katika kutafsiri ni sauti na muundo wa shairi. Fonolojia ni mfumo wa sauti za lugha mahsusi. Taaluma ya fonolojia ilizingatia muundo, sifa na ruwaza za sauti zilivyotumika katika mfumo wa sarufi bayana na lugha kwa jumla. Tafsiri fonolojia iliwakilisha sauti na ruwaza za sauti za lugha asili kwa zile linganifu za lugha pokezi.Katika utafiti huu, lugha mbili zilihusishwa yaani: Kiingereza na Kiswahili.

Katika kiwango cha sauti tofauti kati ya lugha hizi mbili ni kwamba sauti /q/ na /x/ zilipatikana katika lugha ya Kiingereza na asilani katika lugha ya Kiswahili. Kifonolojia, Kiingereza kilikuwa na muundo wa silabi funge tofauti na Kiswahili, kiasilia muundo ulikuwa wazi.

Katika kiwango cha sauti ni wazi kwamba lugha hizi mbili zilikuwa na mifumotofauti. Jambo hili lilipelekea kuwe na utofauti wa kiarudhi. Arudhi ilisimamia muundo, maumbo, na mahusiano mwafaka wa vipashio vya sauti vilivyozidi foni.

Ruwaza za sauti ziliathiriwa hivi kwamba mdundo wa shairi ulibadilika. Mdundo huu ulisaidia kujenga mahadhi ya kimuziki. Kwa mfano, katika shairi la kwanza: Ulimi wa mume wangu ni mkali na *My husband's Tongue is Bitter* (Rejelea Kiambatisho 2-A ubeti wa 1) kulikuwa na uradidi katika kiwango cha neno, konsonanti, vokali na silabi ambazo hazikudumishwa katika tafsiri.Katika kiwango cha sauti na silabi, kulikuwa na ukiukaji wa kisarufi ambapo sauti zilirudiwarudiwa ili kupamba shairi na kusisitiza ujumbe na katika kiwango cha neno kulikuwa na ukiukaji wa kisintaksia.Ulinganifu wa Konsonanti ulikuwa katika maneno yafuatayo:

| Konsonanti | mifano |
|---|---|
| */n/* | *N*ow, I*n*herited, au*n*t, so*n* |
| */s/* | *s*tupidity, *s*pite, *s*on, thing*s*, *s*ay |
| */m/* | *m*e , Ia*m*, co*m*pare, ho*m*estead |
| */d/* | husban*d* , *d*espise, *d*o, an*d* |
| */b/* | *b*ecause, *b*aptized, *b*een |
| */p/* | stu*p*idity, com*p*are, *p*u*pp*y, des*p*ise |
| */t/* | no*t*, li*tt*le, pi*t*, lef*t*, insul*t*, le*tt*er |

Ulinganifu wa irabu ulikuwa kama ifuatavyo:

| Vokali | Mifano |
|---|---|
| */a/* | Husb*a*nd, *a*nd, *a*unt, *a* |
| */e/* | m*e*, b*ee*n, b*e*caus*e*, l*e*ft |
| */i/* | desp*i*se, rubb*i*sh, p*i*t, w*i*th |
| */o/* | *of, no, compare, not* |
| */u/* | *you, stupidity,* |

Katika tafsiri, ulinganifu wa konsonanti ulikuwa kama ifuatavyo:

| Konsonanti | Mifano |
|---|---|
| */m/* | *m*u*m*e, ukase*m*a, *m*wana, *m*aha*m*eni |
| */n/* | u*n*a*n*idharau, u*n*asema, *unan*itukana |

| | |
|---|---|
| */sh/* | *shangazi, shule, unanilinganisha* |
| */s/* | *s*a*s*a, una*s*ema, uki*s*ema, *ghas*ia, *s*ababu |
| */ch/* | *ch*ifu, unani*ch*eka |
| */ng/* | sha*ng*azi, unanili*ng*anisha |
| */z/* | shanga*z*i, za, sikubatizwa |

Ulinganifu wa vokali ulikuwa kama ifuatavyo:

| Vokali | Mifano |
|---|---|
| */a/* | W*a*ngu, s*a*s*a*, k*a*bis*a*, s*a*b*abu* |
| */e/* | mum*e*, *ewe*, |
| */i/* | jaan*i*, *chifu*, nam*i*, mahamen*i* |
| */u/* | *u*kisema, *u*nasema, sabab*u*, h*u*na |

| Maneno yaliyorudiwa | Ruwaza |
|---|---|
| 1) *Now you* despise *me* | (Mshororo wa 1) Kurudiwa rudiwa kwa neno |
| Konsonanti /n/, /w/ / *y* / | Kurudiwa rudiwa kwa konsonanti |
| Vokali / *o* / na /*u* / | Kurudiwa rudiwa kwa vokali |
| 2) *Me* | Kurudiwa rudiwa kwa neno |
| Konsonanti / *m* / | Kurudiwa rudiwa kwa konsonanti |
| Vokali / *e* / | Kurudiwa rudiwa kwa vokali |
| 3) With the *rubbish* in the *rubbish* pit | ( Mshororo wa saba) Kurudiwa rudiwa kwa neno |

Katika Kiswahili sauti za ruwaza hizi zilibadilika mfano:-

| | |
|---|---|
| *i.* *Sasa unani*dharau | Kurudiwa rudiwa kwa neno |
| /-*sa*- / | Kurudiwa rudiwa kwa silabi |
| Konsonanti / *s* / | Kurudiwa rudiwa kwa konsonanti |
| Vokali /-*a*-/ | Kurudiwa rudiwa kwa vokali |
| *ii.* Unani- | Kurudiwa rudiwa kwa viambishi |
| / U-/ | Kurudiwa rudiwa kwa silabi |
| /-na-/ | Kurudiwa rudiwa kwa silabi |
| /-ni-/ | Kurudiwa rudiwa kwa silabi |

| | |
|---|---|
| /-n-/ | Kurudiwa rudiwa kwa konsonanti |
| /-a-/, /-i-/ | Kurudiwa rudiwa kwa irabu |
| *iii.* Takataka za jaani. (Mshororo wa 8) | Hapa mtafsiri hakudumisha urudiaji wa neno *rubbish,* badala yake alitumia kisawe cha taka ambacho kilikuwa ni *jaa* |

Tofauti hizi pia zilipelekea kuwe na athari katika kiimbo na shadda. Mdundo wa shairi ulibadilika hivi kwamba mahadhi ya kimuziki yakaathiriwa.

Tukirejelea shairi la kwanza: *Ulimiwa mume wangu ni mkali.* na *My husband's Tongue is Bitter.* ( Kiambatisho 2-A)tukiangazia shadda katika neno la kwanza:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| '*Hus'band* | 'Mume(Ubeti wa 1 mshororowa1) |
| *'comp'are* | Unanilinga'nisha( Ubeti wa 1 mshororo wa 5) |
| *'insult* | unanitu'kana(Ubeti wa 1 Mshororo wa 10) |
| *'ash* | ma'gadi(Ubeti wa 5 mshororo wa 3) |
| *'Laugh* | unani'cheka(Ubeti wa 5 mshororo wa 11 ) |

Jambo hili liliathiri dhana ya usambamba kwa kiasi fulani na mrejeosabiki katika umbo la shairi. Hapa pia mahadhi ya kimuziki hayakudumishwa: Tulipata kwamba mishororo ilifupishwa au kurefushwa katika lugha lengwa.

Leech (1969) alisema kuwa usambamba urudiaji wa maumbo ambapo vipengee vya ugeukaji hujitikeza. Hii hapa ilikuwa mifano ya usambamba: (Kiambatisho 2- A ubeti wa 3 na wa 5).

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| ***You are no** waman* | **Sasa wewe** ni mtu mzima (Ubeti wa 3 mshororo wa 2) |
| ***You are no** waman* | **Sasa wewe** ni mtu mzima ( Ubeti wa 3 mshororo wa 2) |
| ***You are not** a dead fruit* | **Wewe si** embe mbovu,( Ubeti wa 3 mshororo wa 3) |
| ***Stop** despising people* | **Acha** kudharau watu (Ubeti wa 5 mshororo wa 1). |

| | |
|---|---|
| ***Stop*** *treating me like saltless ash* | **Acha** kunifanyia visa kama makapi ya magadi ( Ubeti wa 5 mshororo wa 3) |
| ***He says Iam*** *rubbish* | **Anasema mimi ni** takataka (Ubeti wa 8 mshororo wa 1 ) |
| ***He says Iam*** *primitive* | *Asema mimi ni* mshamba ( Ubeti wa 8 mshoro wa 4) |
| ***He says my*** eyes *are* dead | **Asema** macho **yangu** yamekufa ( Ubeti wa 8 mshororo wa 6) |
| ***He says my*** ears *are* blocked | **Asema** masikio **yangu** yameziba (Ubeti wa 8 mshororo wa 8). |

Hapa mtafsiri alitumia maneno mengine katika baadhi ya tafsiri ilhali visawe vipo katika lugha ya Kiswahili kwa mfano anatafsiri "*dead fruit*" kama " embe mbovu" badala ya "tunda bovu". Aidha kisawe cha "ash" ni "majivu"

Hii hapa ilikuwa mifano ya mrejeosabiki: Kiambatisho 2- B

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| ***She looks like*** a witch | **Anafanana** na mchawi ( Ubetiwa 9 mshororo wa 4) |
| ***Like*** *someone who has lost his head* | **Kama** mtu aliyepandwa na kichaa (Ubeti wa 9 mshororo wa 5) |
| *We all suffer from a little* ***jelousy*** | Wote tunao **wivu** kidogo moyoni (Ubeti 11 mshororo wa 4) |
| ***It*** *catches you unawares* | **Wivu** unakujia ghafla (Ubeti 11 mshororo wa 5) |
| ***It*** surprises people | **U**nawashangaza binadamu (Ubeti 11 mshororo wa 6) |

Katika shairi, matumizi ya vidokezi (Maumbo yaliyowakilisha vitu vilivyotajwa) yaliathiri kiimbo katika tafsiri kwa mfano:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| ***His*** **eyes** grow large | **Macho** yanamtoka (Kiambatisho 2-A |

| | |
|---|---|
| | ubeti 13 mshororo wa 1). Katika tafsiri hii neno "yake" lingetumika kama kisawe cha "his" |
| ***Ocol'seyes*** *resemble those of the Nile Pearch* | **Macho ya Ocol** yanafanana na macho ya kitoga samaki wa mtoni. Kiambatisho 2- A ubeti 13 mshororo wa 3) |

Hapa mtafsiri alitoa ufafanuzi zaidi kuhusu neno *kitoga*. Ufafanuzi huu haukuwa katika matini chanzi. Huenda alibaini kuwa hadhira lengwa huenda isitambue kitoga kuwa aina ya samaki. Mifano mingine ya vidokezi:

| | |
|---|---|
| *He is in love with a* ***modern girl*** | Anampenda **mwanamke wa kisasa** (Kiambatisho 2- B ubeti 3 mshororo wa 2) Hapa mtafsiri alitafsiri neno "girl" kuwa "mwanamke" badala ya "msichana" hivyo kuipotosha hadhira lengwa. |
| *The name of the* ***beautiful one*****!**<br>Is ***Clementine*** | Jina lake **msichana huyo mzuri**<br>Ni **Clementine**<br>(Ubeti 3 mshororo wa 3 na wa 4).<br>Hapa kisawe cha " beautiful" kinafaa kiwe "mrembo" badala ya mzuri. |
| ***The woman with whom I share my husband***<br>*It is the sight of Tina* | **Huyo mwanamke tunayeshirikiana naye mume**<br>**Tina** ameharibika<br>(Ubeti 10 mshororo wa 3 na 6). |

Hapa aliipotosha hadhira lengwa kwa kutoa kisawe cha "*sight*" kuwa "ameharibika" badala ya "mtazamo." Mathieu (2015) alidokeza kuwa mtafiti anaweza kusuluhisha matatizo yake ya kileksia kwa kurajelea kamusi, benki za istilahi au kutumia sinonimi.

Udondoshajimaneno pia ulichangia katika kuathiri mahadhi ya kimuziki. Kulikuwa na ukiukaji wa kisintaksia.Hii hapa ilikuwa baadhi ya mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Her lips are red-**hot*** | Midomo yake myekundu (Kiambatisho 2- B ubeti 4 mshororo wa5) |
| *Listen Ocol my **old** friend* | Sikiliza Ocol rafiki yangu. (Kiambatisho B ubeti 24 mshororo wa kwanza). Hapa katika matini lengwa dhana ya "old" ingefidiwa kuwa "zamani |
| Is bitter like the roots of *the lyonno **lilly*** | Ulimi wa mume wangu ni mchungu kama mizizi ya mchunga (Kiambatisho A ubeti 11 mshororo wa 2 na 3). Hapa kisawe cha "lily" katika Kiswahili ni "yungiyungi" |

Maneno ya kibadala yaliyotumiwa katika tafsiri pia yaliathiri mahadhi ya kimuziki na pia kulikuwa na ukiushi wa kileksia. Hii hapa ilikuwa baadhi ya mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Only recently I would play | Nilikuwa nikicheza zeze la **kikwetu** |
| On ***my*** bow-harp | ( Kiambatisho B ubeti 2 mshororo wa 3 na 4) . Hapa badala ya kusema "zeze la kikwetu" angesema " zeze langu." |
| *Get tin gready for the **midnight dance*** | Anayejitayarisha kwenda **kuwanga** ( Kiambatisho 2- B ubeti 3 mshororo wa 19 ) |
| *The thing is good on **pink** skin* | Hiyo inawafaa wenye ngozi **nyekundu** (Kiambatisho B ubeti 6 mshororo wa 3) |
| *Like **earth** tremors* | Kama tetemeko la |

| | |
|---|---|
| | **nchi**(Kiambatisho B ubeti 11 mshororo wa 6). Neno "ardhi" lingefaa zaidi badala ya "nchi" |
| *Ocol **rejects*** | Ocol **hapendi** (Kiambatisho 2- B ubeti 6 mshororo wa 1). Kisawe cha "*rejects*" katika Kiswahili ni "hukataa" na wala sio " hapendi". Hapa mtafiti alikuwa na udhaifu |

Kasi ya shairi ilipata kubadilika katika baadhi ya mishororo hivyo kuathiri mawimbi ya sauti. Katika shairi la pili: *The Woman With Whom I Share My Husband* / MwanamketunayeshirikianaMume ( Kiambatisho 2-B) ubeti wa pili kulikuwa na matumizi ya kipumuo katika mshororo wa pili na matumizi ya alama hisi katika mshororo wa tatu wa Kiingereza. Katika tafsiri ya Kiswahili hapakuwa na matumizi ya kipumuo katika mshororo wa pili na katika mshororo wa tatu, mtafsiri alibadilisha alama hisi na badala yake alitumia alama ya kituo. Kasi ya shairi ilipunguka kwa kiasi fulani. (Rejelea Kiambatisho 3 kwa mifano zaidi.)

### 4.2.2 Kiwango cha Maneno

Katika kitengo cha mshikamano, tulishughulikia athari katika tafsiri katika vipengele vifuatavyo: Uradidi, uradidi usio kamili/ sinonimi, usambamba, katafora, udondoshaji wa maneno, vibadala na uundaji wa maneno mapya.Kulikuwa na urudiaji uliodumishwa katika vitengo mbali mbali vya maneno. Kulikuwa na ukiushi wa kisintaksia. Hapa mshairi alikuwa anataka kusisitiza ujumbe. (Rejelea Kiambatisho 2- C):

**Nomino**

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Girl* | Msichana (Ubeti 8 mshororo 1 na 2) |
| *Fish* | Samaki ( Ubeti 21 mshororo 3 na 5) |
| *Dung* | Mavi (Ubeti 31 mshororo 2 na 3) |
| *Women* | Wanawake (Ubeti 19 mshororo 1 na 5) |
| *Wanaume* | Men (Ubeti 19 mshororo 4 na 5 ) |

**Viwakilishi**

Kiwakilishi ni aina ya neno linaloweza kutumika badala ya nomino. Aina za viwakilishi ni kama viwakilishi vioneshi au viwakilishi vya kuonesha, viwakilishi vya nafsi ambavyo vipo vya aina tatu; amba -viwaakilishi nafsi huru -viwakilishi –nafsi viambata -viwakilishi –nafsi rejeshi, viwakilishi vya kuuliza/viwakilishi viulizi ambavyo huashiriwa na mofu /kiambishi {-pi} ambavyo katika tungo hutanguliwa na kiambishi ngeli cha jina husika.

Pia viwakilishi vya urejeshi ambavyo vinajengwa na shina amba- pamoja na vipande vidogo vidogo kama –ye-, -o-, -cho- -vyo-, -lo-, -po-, -mo-, -ko- na kadhalika ambavyo vinachaguliwa kulingana na ngeli ya majina yanayorejeshwa navyo, viwakilishi vya idadi: Viwakilishi hivi hutuarifu kuhusu idadi ya nomino hiyo huweza kuwa kamili (halisi) au ya jumla, viwakilishi vya pekee: Hivi ni aina ya vivumishi vya pekee kuwakilisha nomino. Hufuata sheria za upatanisho za nomino zinazowakilishwa.

Viwakilishi vya A-unganifu ambavyo huundwa kwa kihisishi cha A-unganifu kusimamia nomino iliyomilkiwa, inayochukuwa nafasi fulani katika orodha au nomino ya aina fulani kihisishi a-unganifu huandamana na nomino kuunda kirai husishi ambacho husimamamamahali pa nomino. Viwakilishi vya sifa ambayo huchukua nafasi ya nomino katika sentensi. Katika tafsiri ya Kiingereza kulikuwa na uradidi wa viwakilishi nafsi huru. Hata hivyo, katika tafsiri ya Kiswahili uradidi ulikuwa wa viwakilishi nafsi viambata. Aidha, katika baadhi ya mishororo, uradidi wa viwakilishi haukudumishwa hivyo kuathiri mahadhi ya kimuziki.

Kulikuwa na ukiushi wa kisarufi. Mifano kwa kurejelea Kiambatisho 2- A ubeti wa 1:*My husband's tongue is bitter*/ ulimi wa mume wangu ni mkali-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Now **you** despise me* | Sasa **u**nanidharau |
| *Now **you**...* | Sasa **u**nanipuuza... |
| ***You** insult me* | ***U**nanitukana |
| ***You** laugh at me* | ***U**nanicheka |
| ***You** say | ***U**nasema |
| ***I** have inherited* | .**ni**merithi |
| ***I** have not been to school* | **Si**kuwahi kwenda shule (kapa) |
| ***I** have not been baptized* | Wala kubatizwa (kapa) |

| | |
|---|---|
| ***He*** says... | ***A***nasema... |
| ***He*** no longer... | hana haja nami (kapa) |

**Vivumishi**

Kulikuwa na aina kadhaa wa kadhaa za vivumishi vya sifahutoa sifa za nomino /kiwakilishi cha nomino. Vivumishi vya kumiliki ni vivumishi vinavyoonesha kuwa kitu fulani kinamilikiwa na mtu au kitu kingine.Vivumishi vioneshi huonyesha mahali au upande kitu kilipo. Vivumishi vya aina hii hujengwa na mzizi {h} kwa vitu vilivyopo karibu na mzizi {le} kwa vitu vilivyo mbali. Vivumishi vya kuuliza ni vivumishi ambavyo hufafanua nomino kwa kuuliza habari zake. Hujibu swali: “gani?ipi? ngapi**?”**Kulikuwa na uradidi wa vivumishi vimilikishi katika tafsiri. Hata hivyo uradidi huo haukuwepo katika baadhi ya mishororo, hivyo kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojia.

Hii hapa ilikuwa ni mifano: Kiambatisho 2- D

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| ***My*** *breasts*. | Matiti **yangu** (Ubeti 3 mshororo wa 2) |
| ***My*** *neck* | shingo **yangu**( Ubeti 3 mshororo wa 5 ) |
| ***My*** *breasts* | *Maziwa* ***yangu***( Ubeti 4 mshororo 3) |
| ***My*** *good manners* | *Adabu* ***yangu***( Ubeti 14 mshororo wa 2) |
| ...***your****waist* | ...kiunoni (kapa) |
| ...***your****arms* | ...mikononi (kapa) |

**Vitenzi**

Kitenzi ni neno linaloeleza jambo lililotendwa au lililotendeka. Kitenzi pia huarifu lililofanyika au lililofanywa na kiumbe hai chochote kinachoweza kutenda jambo. Kulikuwa na uradidi wa vitenzi katika matini chanzi na matini lengwa. Hata hivyo, mtafsiri alibadilisha vitenzi vingine katika matini lengwa hivyo kuathiri dhana ya msisitizo maana.Hapa palikuwa na ukiukaji wa kisemantiki.

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| ***Takecare*** | **Angalia (**kibadala**)** |
| ***Takecare*** of *your tongue* | ...**jihadhari** ulimi wako |
| ***Becareful*** *what your lips say* | **Angalia** neno (kibadala)(Kiambatisho A ubeti 2 mishororo ya 3, 4 na 5) |
| ***Hesays*** terrible things... | **Mumewangu** hunitukana...(kibadala) |

| | |
|---|---|
| ***Hesays*** I am rubbish | **Anasema** mimi ni takataka(Kiambatisho 2- A ubeti 7 mshororo wa 2 na ubeti wa 8 mishororo wa 1 na 4 ) |
| *He is in love with a modern **girl*** | Anampenda **mwanamke** wa kisasa |
| *He is in love with a **beautiful** girl* | Anampenda msichana **mzuri**(Kiambatisho B ubeti 1 mishororo ya 2 na 3) |

**Vielezi**

Kulikuwa na uradidi wa vielezi katika matini chanzi. Hata hivyo katika tafsiri baadhi ya uradidi huo haukudumishwa. Mtafsiri pia alibadilisha vielezi vingine na kutumia vielezi mbadala. Pia hapa dhana ya msisitizo iliathiriwa. Hii hapa ilikuwa ni mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *But only **recently*** | Lakini **miakamichache tu** |
| *Only **recently**...* | **Miakamichachetu** iliyopita (Kiambatisho2- B ubeti wa 2 mishororo ya 1 na ya 3)<br>Katika Kiswahili, kisawe cha “recently” ni “karibuni” na wala sio “miaka michache tu” |
| *At the **homestead** of the Hoe chief* | **Nyumbani** kwa chifu wa jembe (Kiambatisho2- K ubeti 2 mshororo wa 5) |
| *The new parties have split the **homestead*** | Vyama hivyo vipya vimegawa ndugu na **nyumba**(Kiambatisho K ubeti 10 mshororo wa4) |
| *Those in the **countryside*** | Wale walio ***vijijini*** (Kiambatisho K ubeti 45 mshororo wa 1) |
| *They return to the **countryside*** | Wanarudi **vijijini** (Kiambatisho 2-K ubeti 49 mshororo wa 1 na wa 2.) |

**Vihisishi**

Katika matini chanzi kulikuwa na urudiaji wa vihisishi. Hata katika tafsiri kulikuwa na uradidi huo japo mtafsiri alidondoa alama hii katika baadhi ya mishororo na hivyo kuathiri toni na kasi ya shairi. Aidha, baadhi ya maneno katika mishororo yalidondolewa hivyo kuathiri jazba ya mwandishi katika matini chanzi. Aidha, kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojia katika baadhi ya mishororo.

Hii hapa ilikuwa mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *And they fear the* ***deadly*** *ojebu taboo*! | Na wanaogopa miiko ya ojebu(Kiambatisho 2-K ubeti13 mshororo wa 11) . Hapa neno deadly halikutafsiriwa na kisawe ni “angamizi” katika Kiswahili |
| *Of our homestead!* | Na wanaogopa miiko ya ojebu(Kiambatisho 2-K ubeti13 mshororo wa 11) . Hapa neno deadly halikutafsiriwa na kisawe ni “angamizi” katika Kiswahili |
| *Like a hyena’s den!* | Kama ndani ya shimo la fisi (Kianbatisho2- C ubeti 25 mshororo wa tatu) ( Alama hisi haikudumishwa) |
| *Than mine!* | Kama yangu**.** (Kiambatisho 2-D ubeti wa 14 mshororo wa 8) (Alama hisi haikudumishwa) |
| *And it goes*! | Na inakwenda.(Kiambatisho2- G ubeti 4 mshororo wa 2) |

**Viunganishi**

Viunganishi ni maneno, kikundi cha maneno au kiambishi chenye kuunganisha maneno, kirai, kishazi au sentensi.Dhima ya kiunganishi ni kuunga vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa kisarufi.Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki wakati wa kutafsiri baadhi ya viunganishi. Tulipata kwamba viunganishi vingine vilibadilishwa na ilhali vingine havikutafsiriwa hivyo kuathiri maana katika lugha lengwa.

Hivyo basi kulikuwa na ukiukaji wa kisintaksia na kisemantiki. Hii hapa ilikuwa mifano ya uradidi katika viunganishi:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| ***And*** *say I have inherited* | Ukisema nimerithi ( kapa )<br>(Kiambatisho 2 -A ubeti wa1 mshororo wa 3) |
| ***And*** *it looks so pale* | Uso ukaonekana mweupe (kapa)<br>(Kiambatisho 2- B ubeti wa 3 mshororo wa 16) .<br>Hapa kisawe cha "pale" ni "umekwajuka" na sio mweupe. |
| ***And*** *I have not been baptized* | **Wala** sikubatizwa ( kibadala)<br>(Kiambatisho A ubeti 1 mshororo wa 14) |
| ***It*** **is** ***not right*** *that* | **Haifai** tena (kibadala)<br>(Kiambatisho 2- A ubeti 4 mshororo wa 3) |
| ***That*** *he trusted me completely* | Alisema alinipenda kabisa (kapa)<br>(Kiambatisho 2- B ubeti wa 2 mshororo wa 8) |
| ***Because*** *she is cold, weak, clumsy* | hana joto, mnyonge na *wala* hakuchangamka (kapa)<br>(Kiambatisho 2- B ubeti 24 mshororo wa 8) |
| ***Because*** *their roots reach deep into the soil* | Mizizi yake ni mirefu<br>Iliyoingia ndani arthini (kapa)<br>**(**Kiambatisho 2- B ubeti 28 mshororo wa 10) |

**Uradidi usio kamili**

Katika kitengo cha mwendelezo wa mshikamano, tulipoangazia dhana tulipata ya kwamba, neno moja au sentensi moja haikutosha kumfanya msomaji apate kuelewa maana. Ilimbidi msomaji apate kurejelea maelezo yaliyotangulia au asome mishororo iliyofuata katika matini. Kulikuwa na ukiukaji wa kisintaksi kwa vile shairi lilikuwa huru, hivyo basi kulikuwa na matumizi ya mistari mishata. Ilimbidi mtafsiri atumie maneno mbadala katika kutafsiri baadhi ya maneno ili apate kuifikia hadhira yake.

Hii hapa ilikuwa baadhi ya mifano:Kiambatisho 2- H:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| *I am ignorant* | Anasema silijui Neno Jema |
| *Of the goodword* | Iliyomo katika |
| *In the* ***Clean*** *Book* | Kitabu **kitakatifu** |

(Ubeti wa 1 mishororo 1-3).

Hapa mtafsiri wa Kiingereza alifanya tafsiri sisisi na kudumisha neno "clean" kama ilivyokuwa katika tafsiri ya Kiacholi.

Hata hivyo, katika tafsiri ya Kiswahili mtafsiri alitumia tafsiri ya mawasiliano ili aweze kuifikia hadhira lengwa hivyo akatumia neno "kitakatifu"

| | |
|---|---|
| *Because he says **Jok** is in my head* | Kwa sababu anasema<br>Nina **shetani** kichwani mwangu<br>(Ubeti wa 2 mshororo wa 3) |
| *Maria the **Clean** Woman* | Maria **mtakatifu** |
| Mother of the ***Hunchback*** | Mama wa **Mungu** |
| *Who spoils things* | *Sisi***wakosefu**<br>(Ubeti wa 16 mishororo 1-3). |

Katika tafsiri hii mtafsiri wa Kiingereza alidumisha tashtiti katika lugha ya Kiacholi kwa kutumia neno "*Hunchback*". Alitumia tanbihi kueleza maana ya " hunchback kuwa ni jina la pepo linalosababisha kifua kikuu cha uti wa mgongo na hivyo kusababisha kibyongo. Hata hivyo mtafsiri wa Kiswahili hakudumisha tashtiti na badala yake akatumia"mtakatifu" kama ilivyo katika ombi la "Salaam Maria" ambalo ni maarufu kwa wakatoliki. Hapa kulikuwa na udhaifu wa kudumisha tashtiti

Katika uchanganuzi wa maneno tulipata kwamba kulikuwa na maneno ambayo yalipata kuhusiana na kukumbushana. Mambo haya yalidhihirika pia katika tafsiri kwa mfano:-

*God: Good word- Clean book-Clean Ghost (Ubeti wa 1)*

Mungu: Neno Jema- Kitabu kitakatifu- Roho mtakatifu

*Church: Pray- Cross- Catholic- Priest- confession-Protestant-Christened-Baptized*

(Ubeti 15:3,4:9,10:3,4:8,11:3,5:3)

Kanisa: utuombee- alama ya msalaba-kikatoliki- wanawake wa kizungu, watawa -maungamo- waprotestanti- kubatizwa

*Songs: drums- dance- dancing- shaking their waists-Singing- rhythm- arena*

(Ubeti 27 mishororo:4:1:3:4:11

Nyimbo: ngoma- mchezo- wakicheza- wakitikisa viuno vyao- mdundo- ngomani

Kulikuwa pia na matumizi ya msamiati uliokubalika ulimwenguni kama vile:-

| | |
|---|---|
| *Pray, God, church, class* | Utuombee, Mungu, kanisa, darasa |

(Ubeti 16:11, 1:6,10:3,16:2).

Hata hivyo, katika kiwango cha maneno (msamiati) tulipata kwamba kulikuwa na kuchanganya ndimi. Katika matini chanzi mwandishi alichanganya Kiingereza na Kiacholi. Sababu ni kwamba alikuwa ametafsiri shairi hili kutoka lugha ya Kiacholi. Masuala ya kitamaduni jamii hayangeweza kutafsiriwa. Mwandishi wa Kiswahili naye alichanganya maneno ya Kiswahili na ya Kiacholi kwa sababu hiyo hiyo. Kutokana na hayo tulipata kwamba maneno haya hayakuwa na mashiko kama ilivyokuwa katika lugha chanzi. Hapa kulikuwa na ukiukaji wa kilahaja na ukiukaji wa kisarufi.Kwa mfano katika shairi la kumi na tatu:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Let them prepare the Malakwang' Dish* | Hebu wakutengenezee chakula cha malakwang (Kiambatisho 2-M). |

Wasomaji wa Kiswahili wanajiuliza "*malakwang*" ni chakula cha aina gani? Hapa mwandishi alikuwa anataka kuchochea wasomaji wake wabainishe maana kutokana na maelezo ambayo yaliyotolewa kwamba *Ocol* arejelee tamaduni za Kiacholi. Mbali na chakula kulikuwa na maneno mengine ambayo yalilazimishwa katika lugha lengwa. Mifano ni mizizi ya *Ombwoye (ubeti 2:1)*, ngoma ya *nanga (ubeti17:9)*, na *alyeka(ubeti 16:2)lurono (ubeti3:2), lukut(ubeti3:5)* na *lacucuku(ubeti 17:6)* ambazo zilikuwa ni shanga za Kiacholi. Hivyo kulikuwa na ukiukaji wa kilahaja katika matini chanzi na pia katika matini lengwa.

Kulikuwa pia na ukiukaji wa kisarufi ambapo mwandishi alivumbua maneno mapya katika matini chanzi hivyo mtafsiri alilazimika kudumisha maneno yayo hayo au kutafuta msamiati mbadala katika matini lengwa. Hii hapa ilikuwa ni mifano:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Or burnt like the **Kongoni*** | Au ameungua kama **Kongoni**. |
| | (Kiambatisho 2-B ubeti 8 mshororo wa 8) |
| *Mother of the **hunchback*** | Mama wa **Mungu** |
| *Full of **graciya*** | Uliyejaa **neema** |
| | (Kiambatisho2-H ubeti 16 mishororo ya 10 na 12) |

Aidha kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki katika tafsiri. Ukiukaji huu uliathiri maana kama ilivyokuwa katika matini chanzi. Ukiukaji huu ulijitokeza Tukirejelea mfano katika Kiambatisho 2-A :

| | |
|---|---|
| *You are not a **dead fruit*** | Wewe si **embe mbovu** |
| *Ocol* **rejects** | *Ocol* **hapendi** |
| | *(Kiambatisho B ubeti wa1 mshororo wa1)* |
| *You saw my **hairstlyle*** | Uliona **nywele** zangu |
| | *(Kiambatisho E ubeti wa 6 mmshororo wa 2)* |
| *And as the **fragrance*** | Kama **harufu** ya... |
| | *(Kiambatisho 2- E ubeti wa 19 mshororowa 1)* |

Katika tafsiri hii dhana ya “*hairstyle*” inafaa iwe “mtindo wa nywele” Katika lugha ya Kiswahili. Aidha dhana ya “*fragrance*” inafaa iwe “harufu nzuri” kwani “harufu” ni neno la kijumla. Pia,tulijiuliza iwapo *embe* ni kisawe cha *fruit* na iwapo kisawe cha *dead* ni *mbovu*. Lakini alifanya hivi ili kuwafikia walengwa wake kwa kutoa maana mahsusi.Kadhalika, mtafsiri alipotafsiri shairi kulikuwa na ukengeushi mwingine wa kisemantiki kwa mfano alipotafsiri kichwa cha shairi la pili:*The woman with whom i share my husband* /Mwanamke tunaye shirikiana Mume (KiambatishoB) maana ilipotoka. Tulipata kwamba dhana ya ‘*kushirikiana’* haikuleta athari katika hadhira lengwa. Ilitarajiwa kwamba mtafsiri angesema ‘*mke mwenza* kwani dhana ya kuwa na wake zaidi ya moja ilikubalika katika jamii ya waswahili tofauti na jamii ya waacholi na waingereza. Katika shairi lili hili alibatilisha tafsiri ya: *the woman with whom i share my husband* kuwa: Huyo mwanamke *hawala* yamumewanguna pia *Anayechangia naye mwanamume*. Hata hivyo mshairi alikuwa anataka kudumisha hali ya tashtiti kaika shairi hilo. Pia tulipata kwamba alipotafsiri ‘*my husband’* kuwa ‘*mume’* katika anwani alipotosha maana kwani neno ‘*mume’* lilikuwa la kijumla tofauti na ‘*my husband’* lililokuwa bayana. Hapa pia mshairi alikuwa anataka kudumisha hali ya dhihaka.

Katika kiwango cha utaratibu wa kuambatanisha dhana tulipata ya kwamba katika matini chanzi kulikuwa na utangulizi kuhusu madhumuni ya shairi hili ambapo mwandishi alisema kwamba alikuwa anataka kuonyesha ni kwa vipi wasomi waafrika walivyokuwa wamekengeuka kiasi cha kudharau mila na desturi za jamii yao.

Mwandishi huyo pia alitutajia wahusika wakuu: *Lawino* na *Ocol* alipokuwa akidokeza anwani ya shairi: *Wimbo wa Lawino*. Mambo haya yalimwezesha msomaji kutabiri kitakachofanyika kutokana na kumbukumbu za maelezo yaliyokuwa katika utangulizi. Vilevile, anwani za mashairi na ubeti wa mwisho katika kila shairi ziliwasaidia wasomaji katika kutambua msimamo wa mwandishi. Hata hivyo katika tafsiri ya shairi tulipata kuwa, hapakuwa na utangulizi kuhusu shairi lenyewe na pia wahusika, hivyo basi mwendelezo wa maana ulikatizwa kwa kiasi fulani kwa wasomaji wa matini lengwa.

Katika kiwango cha vielelezo tulipata ya kwamba msomaji katika matini chanzi alitimiza malengo yake ya kuelewa matini kupitia muundo uliodokezwa na mwandishi. Mwandishi alifuata utaratibu fulani ili kuhusisha madhumuni yake na ufahamu au kumbukumbu za msomaji kuhusu matini hiyo. Jambo hili lilidhihirika (isipokuwa hapakuwa na utangulizi) pia katika tafsiri ya matini hiyo. Ili kudhibitisha kauli hiyo kulikuwa na utambuzi wa vithibiti viini: Katika shairi la kumi na mbili: *My husband's House is a Dark Forest of Books* / *Nyumba ya Mume wangu nimsitu mkubwa wa Vitabu*:Kiambatisho 2-L

**Dhana za kimsingi:**

*1)Vifaa:* Books, dark glasses, papers, desk /Vitabu, miwani ya jua, meza, karatasi.

*2)Mahali:* Ndani ya nyumba.

*3) Tukio:*Lawino alieleza kuhusu vitabu vingi vya mumewe Ocol

*4)Kitendo:* Lawino alidokeza ukengeushi wa mumewe na aliwaomba watuwa ukoo wake wapate'kuomboleza' kifo chamumewe.

**Dhana za kisekondari:**

1) *Hali:* Wasomi watamaduni

2) *Ajenti:* Lawino

3) *Mhusika*: Ocol

4) *Waathiriwa*: Wasomaji

5) *Mahusiano*: Mume – mke

6) *Matokeo*: Athari hasi ya ukengeushi wa wasomi

7) *Mandhari na wakati*:

Kupitia utangulizi katika matini chanzi tulipata ya kwamba mwandishi alichochewa na mambo yaliyofanyika Uganda katika miaka ya sabini, Tulipopiga darubini ubeti wa kwanza, vitenzi vilivyotumika vilikuwa katika wakati uliopo: Listen/sikilizeni. *Icry*/ Ninalia.

Hata hivyo katika ubeti wa pili nyakati ilibadilika na kuwa katika wakati uliopita: *was still wooing me*/alipokuwaakiniposa.Kupitia lugha iliyotumika kulikuwa nn usasa: *Books*/ vitabu. Matumizi ya lugha na vivumishi yalidhihirisha mandhari: *My husband's house*/ Nyumba ya mumewangu (vivumishi) *is a dark forest of books*/ nimsitumkubwawavitabu (Sitiari). Hata hivyo tamathali nyinginezo za usemi kama vile tashbihi hazikubainishwa katika tafsiri kutokana na istilahi za kiacholi ambazo hazikuwa za kutafsiriwa: Rejelea ubeti wa 6: *Like the poistem*/ Kamashinalamti *(mshororo wa 3)*, *Like the ororo snake*/ kamanyokawahatari.(mshor oro wa 8).*Msogezo*: Jambo hili lilitendeka kule Uganda ambapo wasomi wengi walipuuza mila na desturi za jamii na badala yake wakaenzi tamaduni za ughaibuni.Mfano wa pili ulikuwa katika shairi la kumi na moja:*The buffaloes of Poverty Knock the People Down* / Mbogo wa Umaskini Huwaangusha Watu *(Kiambatisho2- K)*

**Dhana za kimsingi:**

*Vifaa*: Vyama, makabila

*Mahali*: Sokoni ( Jukwaa la siasa)

*Tukio*:  Kulikuwa na uhasama baina ya Ocol na nduguye kuhusu msimamo wa kuhusu makabila

*Kitendo*: Lawino anawadhihaki Ocol na nduguye waliokuwa wanahubiri amani kwa wanachama wao ilhali wao wenyewe walikuwa na uhasama kati yao.

**Dhana za kisekondari:**

*Hali:*Uhurudhidiyaamani

*Ajenti:* Lawino

*Mhusika:* Ocol na nduguye

Waathiriwa: Wasomaji

*Mahusiano:* Vyama vya kisiasa, waprotestanti na wakatoliki

*Matokeo:* Uhasama baina ya wanachama wa vyama viwili na baina ya wakatoliki na waprotestanti

*Mandhari na wakati:* Uganda katika miaka ya sabini. Istiahi kama vile independence/ Uhuru vilidhihirisha usasa. Mandhari ya siasa yaliendelezwa na majina ya vyama na jazanda: *The buffaloes of poverty knock the people down*/*Mbogo waumaskini huwaangusha watu*(Kiambatisho 2-K).

*Msogezo:* Kulikuwa na mchipuko wa vyama katika miaka ya sabini kule Uganda

Tulipata kuwa mtazamo wa isimu ulikuwa muhimu kwa sababu zifuatazo: Masuala ya kiisimu yalikuwa muhimu kutambua jinsi lugha husika zilikuwa zimepangwa hasa kwa upande wa kuimarisha istilahi.Sababu hii ilipelekea kuwe na changamoto katika matumizi ya lugha katika tafsiri, kwa mfano, kulikuwa na matatizo ya kutafsiri semi, nahau, mafumbo na hata visawe. Umilisi wa kiisimu pekee haukutosha katika tafsiri. Masuala ya utamaduni pia yalichangia katika usahihi wa mawasiliano.Katika kitengo cha kusudi tulipata ya kwamba, katika matini chanzi madhumuni yalikuwa ni kumjuza msomaji kuhusu athari za ukengeushi miongoni mwa waafrika wasomi.

Hata hivyo, tulipozingatia kanuni nne za vitendo neni za Grice tulipata ya kwamba kwa kiwango fulani tafsiri iliathirika:- Katika kiwango cha kiasi matini chanzi matini ilikuwa na kiwango cha ujulishaji kumwezesha msomaji kupata kuielewa shairi hilo. Kulikuwa na utangulizi ambao uliwaongoza wasomaji kutambua usuli wa shairi hilo na pia wahusika. Hata hivyo mwandishi alikuwa amechopeka istilahi nyingi za lugha ya kiacholi. Jambo hili liliwaathiri tafsiri na wasomaji katika matini lengwa.

Hii hapa ilikuwa baadhi ya mifano ya maneno yaliyohusiana na tamaduni za kiacholi na yaliyozua utata wa kutafsiri:

1) Dhana

a) Imani

Ilikuwa ni vigumu kuhamisha imani kutoka tamaduni moja hadi nyingine. Katika matini lengwa kulikuwa na matumizi ya neno *Jok* (Kiambatisho 2-F ubeti 29 mshororo wa 8)ambaye alikuwa ni shetani. Neno hili lilikuwa na mashiko katika tamaduni ya waacholi kuliko ya waswahili. Kulikuwa pia na neno *Jogoo wa mvua (ubeti wa 8 mshororo wa 4).*Japokulikuwanamaelezokatika tanbihi neno hili lilifungamana na tamaduni ya waacholi. Mti wa *Okango (kiambatissho M ubeti 14 mshororo wa 2)*ulikuwa mti mtakatifu katika tamaduni ya waacholi. Jambo hili lilikuwa ni tofauti na waswahili. Pia neno *Pagak* (Kiambatisho J)lilikuwa na mashiko zaidi katika tamaduni ya waacholi.

b)Asasi za kijamii Kulikuwa na matumizi ya majina ya kiacholi ambayo yalikuwa na mashiko zaidi katiika tamaduni hiyo. Kupitia tanbihi tulihamasishwa kwamba neno *Odure (Kiambatisho2-Fubeti 35 mshororo 1)* lilikuwa ni jina la mzaha la wavulana wadogo waliopenda kukaa-kaa wakati mama alipopika. Jina hili lilitokana na mvulana mmoja aliyekuwa na jina hilo ambaye uchi wake uliiungua kwa moto wa jiko.

Kadhalika, kulikuwa pia na matumizi ya majina ya kiacholi: Majina ya huzuni kama vile *Alobo*, *Abur*, *Ayiko* na *Woko(Kiambatisho 2-H ubeti 63 mshororo wa 2)*. Majina ya mizimu kama vile *Apiyo* na *Acen (kiambatisho H ubeti 61 mshororo wa 1)*. Majina ya miti: *Oywelo, lucoro (Kiambatisho 2-F ubeti 34 mshororo wa1)*. Majina ya ndege kama vile: *Okwik(Kiambatisho2-H ubeti wa19 mshororo wa 4)* Makabila kama vile *Acoli*, *Lango*, *madi* na *lugbara(Kiambatisho K (ubeti wa 5mishororo ya 3,4na 5).*

c)Thamani

Waacholi walithamini *boga*, Chakula cha *malakwang(kiambatisho2-M ubeti wa 3 mshororo wa 3)*, mbegu za *labikka(ubeti wa 6 mshororo wa1),* mizizi ya *Lurono(ubeti wa 3 mshororo wa 3)* na *Lukut(ubeti wa 3 mshororo wa 5)*

d)Mila na desturi

Kulikuwa na miiko ya *Ojebu* mapigano ya mkuki, mchezo wa kung'anganiana, kujipaka mafuta ya mti ya *labwor-omor (kiambatisho 2-E ubeti wa 15 mshororo wa 4)* , kuchemsha mafuta ya panya pamoja na miti yenye harufu ya *Lakura* na *Atika*.(Kiambatisho 2-E ubetiwa 21 mshororo wa 6)

e) Muziki, vyombo vya kale na sanaa

Muziki, mchezo wa kuwinda wa *lawala(kiambatisho2-D ubeti wa 20mshororo wa4),* mkuki wa *alwiri*, densi za *jok,* wachezaji wa *nanga (kiambatisho 2-Mubeti 17 mshororo wa 8)*,njuga za*lacucuku (ubeti17 mshororo wa 6)*

f)Ekolojia: Miti ya *lapena* na *Olim*, mbegu za *labikka*, mizizi ya *lurono* na *ombwoye.(Kiambatisho2-M ubeti wa7 mshororo wa 5,ubeti wa 6 mshororo wa 1,ubeti wa 3 mshororo wa 3 na ubeti wa 2 mshororo wa 1).* Kupitia jinsi matini ilivyotafsiriwa, kulikuwa na dhana ya ukweli kupitia majina halisi ya wahusika yaani Ocol na Lawino. Aidha kulikuwa na istilahi za kiacholi na nyimbo za kiacholi. Kulikuwa pia na matumizi ya tanbihi kueleza msamiati tata wa kiacholi kama vile: *Makapi ya magadi (2-A ubeti wa 5 mshororo wa 4)*-haya na faida yoyote na hutupwa njiani, *Pagak (kiambatisho 2-J)*-kule ambako mtu akienda harudi, kuzimuni*)*, *Lawala(Kiambatisho2-Dubeti 20 mshororo wa 4)*-lawalanimchezowakuwinda, *Jogoo wa mvua (Kiambatisho2-Fubeti wa 8 mshororo wa 4)*-Inaamini waku wa ngurumo na radi husababishwa na ndege mkubwa wa rangi ya kahawia*)*.Hata hivyo katika tafsiri mtafsiri aliamua kutoa ufafanuzi na pia kutumia istilahi zilizoeleweka katika lugha pokezi.

Kwa mfano badala ya kutumia tanbihi katika neno *Cooro(Kiambatisho2-Dubeti wa 20 mshororo wa 5)* alitumia neno *bao*. Katika kiwango cha mahusiano kulikuwa na mwendelezo wa matukio katika matini chanzi. Istilahi zilizotumika zilihusiana kulingana na usemi wa mhusika. Katika tafsiri pia kulikuwa na mwendelezo wa maana ijapokuwa hapakuwa na utangulizi, jambo ambalo lilikatiza mwendelezo huo wa maana.Katika kiwango cha namna kauli ya mwandishi na jinsi alivyoakisi usemi wa wahusika wake ilielezwa kwa mapana sana katika matini chanzi na pia katika matini lengwa. Kwa mfano katika shairi la pili (Kiambatisho 2-B): *The woman with whom I share my Husband*/ Mwanamketunayeshirikianamume, maumbile ya Clementina yalielezwa kwa mapana na marefu.

Aidha katika shairi la tano(Kiambatisho 2-E): *The Graceful Giraffe Cannot Becomea Monkey*/ *Hawezi Twiga kugeuka kuwa Nyani* dhana ya *nywele* imeelezwa kwa mapana na marefu. Tulipoangazia kaida za utunzi wa mashairi ilikuwa ni dhahiri kwamba shairi hili lilikuwa ndefu sana hivi kwamba liligawika katika sehemu kumi na tatu. Hapa kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojiia na ukiukaji wa sajili. Kama mashairi mengine huru shairi hili lilikuwa limegawika katika beti kadhaa na hapakuwa na urari wa vina na mizani. Japo maneno yaliyotumiwa na mtafsiri yalionekana kuwa wazi na sahili katika umbo la nje, kulikuwa  na maneno mengine ya kitamaduni ambayo yalikuwa na maana matilaba. Mtafsiri hakutumia tanbihi katika baadhi ya maneno hayo na hili lilisababisha wasomaji kutopata maana kikamilifu kama ilivyokusudiwa.

Katika kiwango cha ukubalifu tulipata ya kwamba wasomaji wa matini chanzi walipata kuikubali matini hiyo kutokana na maelezo yaliyodokezwa kwenye utangulizi. Hata hivyo ruwaza hiyo haikufuatwa katika tafsiri hivyo kulikuwa na pengo lililoachwa na mtafsiri hakuanza na utangulizi. Kadhalika mhusika Lawino alikuwa akitoa malalamishi yake kuhusu Ocol na wasomaji hawakuwa na budi kuikubali kauli yake. Hapakuwa na nafasi kwa wasomaji kutoa msimamo wao kuhusu malalamishi ya Lawino.

Istilahi nyingi za kiacholi pia zilitinga mawasiliano kwa wasomaji wa jamii lengwa. Wasomaji walipata kujiuliza maswali kama: Chakula cha *malakwang* kilikuwa cha aina gani? Watu wa  *Payira* walikuwa ni watu wepi? *Orak* ilikuwa ni ngoma ya aina gani? *Odye* na *Lacomi* zilikuwa ni mavazi ya aina gani?

Hata hivyo, muundo wa shairi na maelezo ya mwandishi katika matini chanzi na matini lengwa yaliweza kufanikisha mawasiliano kiasi cha wasomaji kuelewa ujumbe wa mwandishi.

Katika kiwango cha ujulishaji tulipata ya kwamba kutokana na utofauti wa kileksia na kisintaksia katika Kiingereza na Kiswahili kulikuwa na mabadiliko katika usambazaji wa maelezo. Ilimbidi mwandishi wa matini chanzi atumie tanbihi katika kufafanua baadhi ya istilahi za kiacholi. Mwandishi wa matini lengwa pia alituumia tanbihi na wakati mwingine alilazimika kufafanua au kutoa kisawe cha neno katika matini lengwa ili aweze kuwafikia walengwa wake. Kwa muhtasari:-

Aina ya matini: *Fasihi*

Kitengo: *Shairi*

Mada: Wimbo wa Lawino

Utaratibu wa ujulishaji:

*Utaratibu wa kwanza waujulishaji*: Sheria za kisarufi zilikuwa wazi Japo katika tafsiri alama za uakifishaji zilibadilika katika baadhi ya mishororo.

*Utaratibu wapili waujulishaji*: Muundo wa nje wa matini katika matini chanzi na matini lengwa ulituwezesha kuelewa matini.

*Utaratibu wa tatu wa matini*: Kulikuwa na msamiati ambao haukutambulika katika matini chanzi na matini lengwa. Iliwabidi waandishi wote watumie tanbihi, sinonimi na ufafanuzi. Hata hivyo, sio maneno yote yaliyoweza kunukuliwa kulikuwa na mengine ambayo yaliachwa, hivyo kuvunja mwendelezo wa maana.

Mifano ya ajenti:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| As *the fishermen* hook the fish | kama mvuvi anavyomchoma samaki ndoana |
| Sifa bainifu | hapakuwa na sifa bainifu |
| Andpull *them* upmercilessly | Aka- *m*- tupa mchangani bila huruma |
| Kurejelea samaki wengi | kurejelea samaki mmoja |

Katika kiwango cha muktadha tulipata ya kwamba katika matini chanzi kulikuwa na kiwamgo fulani cha kuhusisha usemi na muktadha wa hali na mahali. Kupitia utangulizi wasomaji walipata kutambua hali ilivyokuwa kule Uganda katika miaka ya sabini baada ya wakoloni kung’atuka na mielekeo ya wasomi kuhusu tamaduni zao na zile za ughaibuni.Hata hivyo, katika tafsiri muktadha wa hali na mahali ulikuwa tofauti na ule wa matini chanzi.

Jambo hili lilifanya kuwe na mabadiliko fulani kwa kufuata taratibu fulani za tafsiri kama vile:udhahirishaji, ufupisho na ubadilishanaji wa mpangilio wa matini.

Mabadiliko haya yalisababishwa na mahitaji ya mwandishi wa matini lengwa kutaka kudumisha madhumuni na utendakazi wa matini katika muktadha wake mpya. Hii hapa ilikuwa ni mifano ya taratibu hizi katika shairi la nne, *Blew Like a Horn Among the Payira* /Jina langu lilivuma kama Parapanda miongoni mwa Watu wa Payira.*(kiambatisho 2-D)*

Udondoshaji:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *And I played on **my** bow-harp* | Nami nilijua kupiga **kizeze** *(ubeti wa 5 mshororo wa 5)* |
| With ***elephant*** grass | Kiliezekwa vizuri kwa **manyasi** *(ubeti wa 9 mshororro wa 3)* |
| ***Colourful** ten- stringed **lion** beads* | Mitungo kumi ya **nene**shanga *(ubeti wa 10 mshororo wa 2)* |

Udhihirishaji:

| | |
|---|---|
| 1)*Whatisallthis?* | Upuuzi gani huo?(ubeti wa 15 mshororo wa1) |
| *2)*Like *beggers* | Kama maskini **wanaaomba barabarani** *(ubeti wa 18 mshororo wa 1)* |
| *3)You cannot sing a **solo*** | Huwezi **kuanza wimbo** *(ubeti 21mshororo wa2)* |
| *4)I was bright* | **Mwenye akili** nimechangamka *(ubeti wa 1mshororo wa 3)* |

Maneno mbadala:

| | |
|---|---|
| *1)You saw me when I was **young*** | Uliniona nilipokuwa *msichana* *(ubeti wa 6 mshororo wa 4)* |
| 2)*Thesonofthebullwept* | Mwana wa dume alilia (ubeti wa 6 mshororo wa 7) |
| *Formewithtears* | Akatoka machozi kwa ajili yangu (ubeti wa 6 mshororo wa 7) |

| | |
|---|---|
| 3)*Whose mother has **stayed long*** | Mamaye yuko katika shamba la ufuta. (ubeti wa 6 mshororo wa 110 |

Maneno yaliyochopekwa:

| | |
|---|---|
| *1)Like house flies* | Kama **kundila** nzi (ubeti wa 16 mshororo wa 4). |
| 2) I sang *sweetly* | Nilijua kuimba *vizuri(ubeti wa 14 mshororo wa 1)* |
| 3)You loved my giraffe tail bangles | Ulizipenda bangili zangu *zilizosongwa* kwa usinga wa twiga. (ubeti wa 8 mshororo wa1) |

Muktadha wa hali:

Nyanja: Siasa

Kulikuwa na mchipuko wa vyama vya kisiasa.

Utaratibu: Kulikuwa na uhasama kati ya Ocol na nduguye kuhusu siasa. Lawino alishangazwa ni kwa vipi ndugu wawili wanawasihi wanachama wao wawe na amani ilhali wao wenyewe walikuwa ni mahasimu. Namna: Muktadha wa Isimu. Katika matini chanzi lugha ilikuwa rasmi. Lugha ilifanya kazi ya kuwafahamisha wasomaji kilichojiri kisiasa katika miaka ya sabini nchini Uganda. Lugha ilifungamana na muktadha wa tamaduni ya jamii lengwa. Hata hivyo, katika tafsiri , muktadha ulikuwa tofauti. Jambo hili liliathiri pakubwa jazba aliyokuwa nayo mwandishi wa matini chanzi (Kiacholi) katika matini lengwa. (Kiingereza na Kiswahili). Hii hapa ilikuwa ni mifano ya jinsi lugha ilvyotumiwa kupasha habari kuhusu siasa kwa njia ya tashtiti na kiwango cha athari katika muktadha wa lugha lengwa .

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *And the forced labour system* | ...mpango wa manamba (kiambatisho 2-K ubeti wa 6 mshororo wa 13) Tafsiri ya Kiswahili kwa muktadha wa wasomaji waswahili wakenya kwani neno *manamba* lilifahamika kama *utingo*. Hapa kulikuwa na ukiushi wa kihistoria ambapo msamiati huo ulitumika katika kipindi cha ukoloni. |

| | |
|---|---|
| 2.*They reject the* ***famine relief*** *granaries* | **Msaada wakutengenezea** maghala **ya chakula chanjaa** *(kiambatisho K ubeti wa 6 mshororo wa 12)* Katika muktadha wa Kiswahili tafsiri ya *famine relief* iliwakanganya wasomaji kani walijiuliza chakula cha njaa kilikuwa chakula cha aina gani? |
| 3.*There was* ***homicide*** *between them* | Utadhani **wamepasuana uchawi**. (kiambatisho K ubeti wa 11 mshororo wa 4). Katika Kiswahili kisawe cha“homicide” ni “mauaji ya binadamu”. Hapa dhana ya *homicide* ilibadilika kuwa *uchawi*. Wasomaji wa Kiswahili walijiuliza iwapo uchawi wa aina yoyote huleta maafa |
| 4.And they fear the deadly Ojebu taboo | Na wanaogopa miiko ya Ojebu(kiambatisho K ubeti 11 mshorororo wa 10). Katika muktadha wa waswahili miiko ya Ojebu haikuleta athari kama ilivyokuwa katika matini chanzi(Kiacholi) |
| 5. *Collect the Odir and Ocienne insects* | Wana wa kukusanya **wadudu** |
| And they roast the Odir and Ocienne | wanawakaanga na kuwala(kiambatisho K ubeti wa 31 mshororo wa 7) Mtafsiri hakubainisha aina ya wadudu katika matini lengwa hivyo, kulikuwa na pengo la mawasiliano. Mtafsiri wa Kiingereza alidumisha majina ya Kiacholi nah ii pia iliwakanganya |

wasomaji wa Kiingereza.

6.He is like a ***newly eloped*** girl Kama msichana ambaye *Ndiye wa kwanza atoroshwe (kiambatisho H ubeti wa 10 mshororo wa 2)* Tafsiri ya "*newly eloped*" haikuleta athari kama ilivyokuwa katika matini chanzi.

Sifa hizo ziliwawezesha wasomaji kubainisha katika matini nyingine sifa walizotarajia kutegemea ufahamu wao wa matini nyinginezo. Yaani mambo haya yalihusisha matarajio yao kuhusu matini husika. Wasomaji walitarajia shairi liwe moja, kinyume na matarajio yao, shairi hilo lilikuwa limegawika katika sehemu kumi na tatu. Kadhalika wasomaji hawakutarajia beti za tafsiri kuwa ndefu kuliko matini chanzi.

Kupitia athari zilizotokana na istilahi za kiacholi, wasomaji hawakutarajia istilahi hizo kuhamishwa katika matini lengwa pasi na ufafanuzi zaidi. Hata hivyo, kulikuwa na istilahi za kiacholi ambazo ziliweza kufafanuliwa kupitia tanbihi na picha. Wasomaji pia walitarajia pawe na mazungumzo kati ya wahusika wakuu, yaani Ocol na Lawino. Badala yake, Lawino ndiye alisimulia kuhusu wahusika wote, hivyo wasomaji wengi walielekea kumuunga mkono. Iliwezekana kutambua mandhari kupitia, lugha iliyotumika, vitenzi, vivumishi na taswira kutokana tamathali za usemi.

### 4.3 Kubainisha Changamoto za Matumizi ya Lugha

Adiel naAhmed (2016) walinukuu nadharia ya Lotman iliyosema kuwa hakuna lugha inayoweza patikana bila kuangazia muktadha wa kitamaduni na hakuna tamaduni inayopatikana bila kuangazia muundo wa lugha asili (Lotman 1978:211-32).Hivyo watafsiri wanafaa watilie maanani suala la utamaduni katika matini chanzi na jinsi inavyohamishwa katika matini lengwa. Matatizo haya yanategemea pengo la kiisimu na kitamaduni kati ya lugha mbili au zaidi husika (Nida, 1964: 130).

Changamoto za kiisimu zilipelekea kuwe na changamoto za matumizi ya lugha. Lugha moja yaani Kiingereza haikuweza kubeba tamaduni nyingine yaani ya Kiacholi na ya Kiswahili. Matumizi ya lugha yaliambatana na mila na desturi ya kijamii. Msamiati ulifungamana na utamaduni. Usahihi wa matumizi ya lugha ulifungamana na misingi ya kijamii.

Tafsiri iliathiriwa na matumizi ya lugha kwa misingi ya ekolojia, violwa, mila na desturi siasa na dini. Matatizo ya kutafsiri semi, nahau visawe na mafumbo yalizuka katika nadharia ya kiisimu. Kwa vile tafsiri iliegemea upande wa mawasiliano, nadharia ya mawasiliano ilifaa zaidi kukidhi ufinyu wa kiisimu. Katika utafiti huu, matokeo yafuatayo ya matumizi ya lugha yaliangaziwa:

### 4.3.1Tamathali za Usemi na Mbinu za Sanaa

Adiel na Ahmed (2016) waliangazia aina tatu za sitiari: zile ambazo zina aina sawa au hali sawa ya kiramani, Zile ambazo zilikuwa na hali sawa ya kiramani lakini kileksia zimetumika kwa njia tofauti na zile ambazo hazina hali sawa kiramani. Jambo hili lilipelekea mtafsiri kutimia mbinu kadhaa kutegemea changamoto.Tamathali za usemi zilihusisha maneno ambayo yaligeuzwa maana yao ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Sanaa ilikuwa ni ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha mawazo kupitia lugha. Katika tafsiri tulipata kwamba tamathali hizi na mbinu za sanaa zilipata athari kwa sababu ya utofauti wa muktadha. Kulikuwa na tamathali za usemi na mbinu za sanaa ambazo zililazimishwa kutoka tamaduni ya matini chanzi hadi matini lengwa. Wakati mwingine ilimbidi mwandishi kutumia tanbihi ili kuwafikia walengwa wake. Wakati mwigine alilazimika kutafuta kisawecha neno katika lugha lengwa.

Tukirejelea shairi la kwanza mwandishi alitafsiri taswira kupitia tashbihi, tashtiti, sitiari tashihisi na jazanda. Hii hapa ilikuwa ni mifano:Kulikuwa na tashbihi iliyofungamana na tamaduni ya waacholi. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki na wa kilahaja pale ambapo mtafsiri alishindwa kupata visawe katika matini lengwa. Hii hapa ilikuwa ni mifano ya tashbihi:-

*My husband's tongue is bitter like the roots of the* ***lyonno lily****. /* Ulimi wa mume wangu ni mchungu *kama* mizizi ya ***mchuga***.(Kiambatisho 2-A ubeti wa 11 mshororo wa 2 )Hapa mwandishi alitafuta kisawe cha *lily*. Alitatizika kupata kisawe cha *lyonno*.

Mifano mingine katika ubeti huo ni:-

*Hot like the penis of the bee* /Unawasha kama mwiba wa nyuki (mshororo wa 3),

*Like the* ***sting*** *of the kalang*/kama mwiba wa sungusungu(mshororo wa 4),

**Deadly** *like the spear of the buffalo hornet*/unaumiza kama mwiba wa nyigu mkubwa (mshororo wa 6),

***Ferocious** like the poison of the barren woman*/unafoka kama sumu ya mwanamke tasa. Katika Kiswahili kisawe cha “ferocious” ni “ kali” na mtafsiri alitumia neno nyingine mbadala.
Aidha, sitiari pia ilifungamana na tamaduni ya jamii husika.Utamaduni ulihusu maswala mengi ya maisha ya jamii. Hapa tulifikiria zaidi falsafa za maisha, zilivyoenezwa kupitia matumizi ya lugha na fasihi.

Ngano na tanzu zingine zafasihi ni hifadhi za tamaduni za lugha zake. Tunapotafsiri fasihi, tunafuma baadhi ya vipengele vya utamaduni wa lugha asili kwa utamaduni wa lugha pokezi. Mtafsiri alitatizika kupata baadhi ya visawe vya sitiari katika matini lengwa. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki na wa kilahaja mtafsiri alipodumisha baadhi ya sitiari hizo zilizokuwa zimefungamanishwa na tamaduni za waacholi na waingereza. Alilazimika kudondoa maneno fulani hivyo thamani ya sitiari katika lugha chanzi iliweza kupotea. Wakati mwingine alipuuza visawe ambavyo vilikuwepo katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuendeleza udhaifu. Tukichukua mfano wa kichwa cha shairi la tano: *The **Graceful** Giraffe Cannot Become a Monkey* / Hawezi Twiga  kuwa Nyani (Kiambatisho2-E); dhana ya *Graceful* ilipotea katika matini lengwa. Mifano mingine ya sitiari ambazo hazikuwa na mashiko katika matini lengwa ni katika anwani zifuatazo:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *The Mother Stone Hasa Hollow Stomach* | Jiwe-mama Lina Shimo Tumboni ( Rejelea Kiambatisho 2-F). |
| *Buffaloes of Poverty Knock The People Down* | Mbogo Wa Umaskini huwaangusha Watu (Rejelea kiambatisho 2-J). |
| *My husband’s House is a Dark Forest of Books* | Nyumba ya Mume wangu ni Msitu  Mkubwa wa Vitabu    (Rejelea kiambatisho L) |

Kila jamii ilikuwa na jazanda iliyotumiwa kwa uzoefu kiasi cha kueleweka vizuri na wanajamii husika. Jazanda ilipohamishwa kutoka tamaduni moja hadi nyingine, maana haikukolea vizuri katika jamii lengwa ambayo haikuwa na uzoefu wa kuitumia. Lawino alijaribu kuonyesha ya kuwa hatuwezi kubadilika na kuwa kama watu wengine.  Alirejelea jinsi Ocol alikuwa amebadilika kiasi cha kutaka kuwa kama mzungu. Alipendekeza kuwa Ocol alifaa arudi awe kama alivyokuwa hapo zamani.

Katika shairi la kumi na tatu:Let them prepare the Malakwang' Dish/*Hebu wakutengenezee chakula cha malakwang* (Kiambatisho 2-M) kaina za vyakula na sehemu za mwili za wanyama kijazanda. Tulipata kwamba mifano iliyonukuliwa ilikuwa ya tamaduni ya waacholi hivyo haikuwa na mashiko katika tamaduni ya waswahili.

Hii hapa ni mifano mingine ya baadhi ya jazanda zilizopoteza thamani katika matini lengwa:-
*The pumpkin in the old homestead must not be uprooted/* mboga ulioota mahameni usidiriki kuung'oa*(Kiambatisho2-B ubeti wa 26 mishororo ya 3 na 4)* .Hapa *the pumpkin* liliashiria boga mahsusi. Katika jamii ya waacholi boga iilichukuliwa kama chakula muhimu sana tofauti na jamii ya waswahili. Mtafsiri alibadilisha *boga* kuwa *mboga* hapakuwa na athari katika matini lengwa. Pia katika sura ya nane (Kiambatisho 2-H): -
*I am ignorant of the Good Word in the Clean Book* / Silijui Neno jema lililomo katika Kitabu kitakatifu.Neno *clean* lilikuwa limetumika kijazanda kumaanisha takatifu.
Katika tafsiri mtafsiri hakudumisha neno hilo na badala yake akatumia neno *takatifu* kwa hivyo jazanda hiyo haikuwa na mashiko katika lugha lengwa.

Kila tamaduni ilikuwa na njia yake ya kukejeli kupitia tashtiti, hivyo katika tafsiri kulikuwa na athari fulani japo haikuwa kama ilivyokuwa katika matini chanzi. (ya Kiacholi na ya Kiingereza) Matini chanzi ilikuwa inawalenga waacholi. Ilipotafsiriwa muktadha ulibadilika. Kwa mfano katika sura ya pili: -
*The Woman With Whom I Share my Husband/Mwanamke tunayeshirikiana mume*/ (Kiambatisho 2-B). Katika jamii ya kiafrika kuna dhana ya mume kuwa na kimafa au mke wa pili tofauti na jamii ya waingereza.

Kupitia tashbihi: *Or burnt like the* ***kongoni****/ au ameungua kama* ***kongoni***. (kiambatisho2-B ubeti wa 8 mshororo wa 10).Tashtiti hii ina mashiko sana katika matini chanzi ya Kiacholi na sio katika Kiingereza na Kiswahili. Lawino alifafanua maudhui ya ukengeushi kupitia kwa mwanamke aliyependwa na mumewe. Urembo wake Clementina ulielezwa kwa njia ya tashtiti. Hata hivyo wasomaji wa lugha lengwa walitatizika kuelewa maana ya neno *kongoni*. Aidha kejeli haikudumishwa katika shairi la: *I am Ignorant of the Good Word in the Clean Book/*Silijui Neno jema lililomo katika Kitabu kitakatifu katika ubei wa 16. (Rejelea kiambatisho 2-H) Katika matini chanzi kulikuwa na kukejeli dini la Kikristo na haukudhihirika katika maombi ya 'Maria' mama wa Mungu. Hapa kulikuwa na ukiushi wa kileksia ambampo msamiati tofauti ulitumika ili kuwafikia walengwa wa Kiswahili.

Takriri ilifungamanishwa na tamaduni ya lugha husika.Takriri zilitumika kuleta mahadhi fulani ya kimuziki na pia kuleta dhana ya usambamba.Iwapo mtafsiri alilazimisha baadhi ya takriri hizo takriri hizo zilikuwa za kishenzi.Kulikuwa na ukiukaji wa kisintaksi kutokana na takriri hizo.

Hii hapa ilikuwa ni mifano ya takriri za kishenzi:-

Kiambatisho 2- J

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| | Ubeti 75 mishororo ya: |
| ***You*** *do not resist* | Hukatai (5) |
| ***You*** *must not resist*. | Usikatae. (6) |
| ***You*** *can not resist* | Huwezi kukataa (7) |
| | Ubeti wa 58 mishororo ya: |
| ***Even if*** *his ears are dead* | **Hatakama** masikio yake yameziba (4) |
| **Even** ***if*** *the world has boxed him* | **Hatakama** angefungiwa na dunia (5) nzima |
| ***Even if*** *his legs are dry like firewood* | **Hatakama** miguu yake imekauka kamakuni (6) |
| | Ubeti wa 43 mishororo ya: |
| ***And*** *throat trouble and eye sickness* | Magogole na magonjwa ya macho (9) |
| ***And his*** *ears have pus* | Masikio yake yavuja usaha (10) |
| ***And his*** *legs have ulcers* | Na miguu yake ina vidonda (11) |
| ***And his*** *loin-string is loose* | Naye dhaifu, kakondeana (12) |
| | Kiambatisho 2-I, ubeti wa 16 mishororo ya: |
| **Theclay** for moulding Skyland | **Udongo** wa kutengenezea mbingu (3) |
| **Theclay** for moulding earth | **Udongo** wa kutengenezea nchi (4) |
| **Theclay** for moulding the moon | **Udongo** wa kutengenezea mwezi (5) |
| **Theclay** for moulding the stars | **Udongo** wa kutengenezea nyota (6) |

Katika Kiswahili ilikuwa vigumu kupata kisawe cha "*the*" kuashiria kitu mahususi.

Aidha, misemo na nahau zilifungamanishwa na tamaduni ya lugha husika.

Wasomaji hawakupata athari kama ilivyo kuwa katika matini chanzi mtafsiri alipohamisha baadhi ya misemo na nahau za matini chanzi.Hii hapa ilikuwa baadhi ya misemo na nahau zilizolazimishwa kutoka matini chanzi hadi matini lengwa:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Time is money | Muda ni fedha<br>(kiambatisho 2- G ubeti wa 21: 9) |
| Who has ever prevented<br>The cattle from the salt lick? | Nani aliyeweza kumzuia ng'ombe<br>asirambe chumvi?<br>(Kiambatisho H ubeti 37:3-4) |

Kinaya kilifungamanishwa na mila na desturi za jamii, hivyo ilipohamishwa hadi matini lengwa ilipoteza thamani kutokana na utofauti wa muktadha.Kinaya kilikuwa kinawalenga wasomi katika jamii ya waacholi na jinsi walivyokuwa wamekengeuka katika kipindi fulani. Wasomaji katika lugha lengwa hawakupata athari kama ilivyokuwa kwa wasomaji katika matini chanzi. Katika kiambatisho2-B ilikuwa ni kinaya kwamba Lawino hakuwa anamwonea gere Clementina. Alikuwa amekasirika tu na Ocol ambaye alipendelea kuwa na mwanamke aliyemshinda umri. Aidha urembo wake ulielezwa na Lawino kwa njia ya tashtiti. Tulipata kuwa Lawino alipendelea tamaduni za kiacholi zidumishwe.

Kinaya ni kwamba, Ocol alipendelea kuwa kama wazungu. Ilikuwa ni kinaya kwamba, hata baada ya Lawino kudhihakiwa na Ocol, bado Lawino alimsihi arudi katika njia za Kiacholi.Pia alimwomba Ocol amruhusu apate kumsifu (Kiambatisho 2-M).Ilikuwa ni kinaya kwamba Ocol hakupenda tamaduni za Kiacholi ilhali yeye alikuwa ni mu-Acholi. Kadhalika, urembo, mavazi, saa, misimu, densi, vyakula, na stovu za Kiacholi zilikinzana na zile za Kiingereza na za Kiswahili. Aidha, Ocol alikuwa ni msomi japo Lawino hakuwa amepata kisomo. Ocol alipendelea lugha ya Kiingereza kuliko ya Kiacholi ambayo alisema ilikuwa ni ya kishenzi.

Katika kipindi hiki nchini Uganda, wasomi wengi walikuwa wamekengeuka. Hadhira hii ilipata mguso zaidi ikilinganishwa na waingereza na waswahili. Kinaya kilionekana kupitia mawazo ya Lawino kuhusu wanasiasa kama mume wake na nduguye mume wake waliokuwa wakihubiri uhuru na amani japo nyumbani walikuwa ni mahasimu. (Kiambatisho 2- K). Katika kipindi hiki vyama vingi vya kisiasa vilikuwa vimechipuka.

Katika matini chanzi majina ya vyama hivyo vilitajwa na makabila yaliyokuwa yakizozana wakati huo yalitajwa, hivyo wasomi katika matini chanzi walipata mguso zaidi kuliko wale wa matini lengwa.

### 4.3.2 Imani, thamani na taasisi

Tamaduni ya jamii ya kiacholi ilihamishwa kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Wakati mwingine ilimbidi mtafsiri kutoa ufafanuzi zaidi kwenye tanbihi, kuhamisha istilahi hizo, kudondoa istilahi hizo au kutoa maneno mbadala katika matini lengwa. Kama mtafsiri wa Kiingereza mtafsiri wa Kiswahili alidumisha istilahi za kiacholi huku akitumia tanbihi kutoa fasili katika baadhi ya istilahi. Hata hivyo hakuweza kutoa maelezo yote ya istilahi za kiacholi hivyo kulikuwa na udhaifu. Hii hapa ilikuwa ni mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Like* ***Labeja***, ***the jok*** **of** ***Alero*** | Kama **Labeja**, **Shetani wa Alero** (Usultani wa Mashetani) .(Kiambatisho 2- C ubeti 21: 2) |
| *And caught the* ***rain-cock*** | Na kumnasa **jogoo wa mvua** (Inaaminiwa kuwa ngurumo na radi husababishwa na ndege mkubwa wa rangi ya kahawia.). (Kiambatisho 2- F ubeti 8:6) |
| *The* ***rain-cock*** *prepares afeast* | **Jogoo wa mvua** huandaa karamu (Huyu ni mtu, kohani wa mvua anayeongoza tambiko za kuomba mvua).(Kiambatisho 2-G ubeti 39:11) |
| *And when it is* ***JokOmara*** | Na kama ni **Omara**(Kiambatisho 2- J ubeti 27:1) |
| *Or* ***Odude*** or ***Ayweya*** | ***Odude*** au *****Anyweya***(Kiambatisho 2- J ubeti 27:3) |
| *When* ***jok Rubanga*** | Kama **shetaniRubanga** (Jina la Mungu wa kikristo katika |

| | |
|---|---|
| | lugha Lwo ni **Rubanga**) (Kiambatisho 2- J 27: 5) |
| *Or **jokOdude*** | Au *shetani Odude* (Kiambatisho 2- J 27: 7) |
| *The last safari to**Pagak*** | Safari ya mwisho kwenda **Pagak** (kuzimuni),<br>(Kiambatisho 2-J –anwani) |
| *Let them prepare the* ***malakwang*** dish | Hebu wakutengenezee chakula cha **malakwang**<br>(Kiambatisho 2-M- anwani) |
| *The **Oput- drinking peace making ceremony*** | Utadhani **tambiko za pombe zakuleta suluhisho** hazijafanyika<br>(Kiambatisho K ubeti 11:7) |
| *As they fear the deadly **ojebu** taboo* | Na wanaogopa miiko ya *ojebu*<br>(Kiambatisho2-K ubeti 11:10) |

**4.3.3 Misimu na majina**

Mtafsiri alilazimika kuhamisha misimu na majina ya Kiacholi ambayo hayakuwa na mashiko katika tafsiri ya Kiingereza na matini lengwa (Kiswahili). Wakati mwingine alipuuza visawe ambavyo viko katika lugha ya Kiswahili.Wakati mwingine alitoa ufafanuzi, kudumisha istilahi hizo au kuzidomdoa.Hapa kulikuwa na ukiukaji wa kilahaja. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki alipojaribu kubadilisha maneno hayo na visawe katika matini lengwa

Hii hapa ilikuwa ni mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *In* a *windy **storm*** | Wakati wa *upepo* (neno “storm” ni dhoruba) |
| *During the **Ager** period* | Majira yaitwayo **Ager**<br>(Kiambatisho 2- G ubeti 44:1) |
| *The period is called **Poto-kot*** | Majira hayo huitwa **Poto-kot**<br>(Kiambatisho 2-G ubeti 45:5) |
| *The period is called **Odunge*** | Majira hayo huitwa **Odunge**<br>(Kiambatisho 2- G ubeti 47:4) |
| *Iscalled **abalo-panga*** | Huitwa **Abalo-Panga** |

| | |
|---|---|
| | (Kiambatisho 2- G ubeti 48:5) |
| ***Okang*** *Was born in the beginning* of the dry *season* | **Okang** alizaliwa mwanzo wa kiangazi (Kiambatisho G ubeti 56:1) |
| *Liste my father comes from* ***Payira*** | Baba yangu anatoka **Payira**(Kiambatisho 2-E ubeti 4:2) |
| *My mother is a woman of* ***Koc***! | Mama yangu mwanamke wa **Koc**! (Kiambatisho 2- E ubeti 4:3) |
| *From the mouth of the* ***Oyitino*** *River* | Kutoka Mtoni (Kiambatisho 2- I ubeti 13 :2). |

**4.3.4 Ngoma, mavazi, nyimbo, vifaa, vyakula na ala za kimuziki**

Majina ya ngoma, mavazi, vifaa na ala za kimuziki yalitafsiriwa jinsi yalivyokuwa katika matini chanzi ya Kiacholi na tafsiri yake ya Kiingereza.. Wakati mwingine, ilimbidi mtafsiri atafute visawe au adondoe istilahi za Kiacholi katika matini lengwa ili aweze kuifikia hadhira yake. Hii hapa ilikuwa ni mifano:-

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| *The ‘****get-stuck*** *dance drums* | *Ngoma* (Kiambatisho 2-H ubeti 23:1) |
| *Who fears grinding the* ***kabir*** *millet* | Aogopaye kazi ya kusaga mtama (Kiambatisho2- C ubeti 8:4) |
| *Resembles the* ***alwiri*** *spear* | Na mkuki aina ya *alwiri* (Kiambatisho 2-E ubeti 21:6) |
| *You do your hair with* ***akuku*** | Nywele zako unazipaka **masizi** (Kiambatisho 2-E 14:2) |
| *Who plays the* **nanga** | Anayepiga **zeze**(Kiambatisho E) |
| *Bring the* ***lacucuku*** *rattles* | Leta na **lacucuku** (Kiambatisho2- C Ubeti 9:2) |
| *Call the* ***nanga*** *players* | Waite wachezaji wa *nanga* (Kiambatisho E 39:5) |
| *You hear* **Otole** *dance drums* | Utasikia ngoma za **Otole** (Kiambatisho G ubeti 51:1) |
| *It means the* ***moko*** *dance* | Ngoma iitwayo **moko** (Kiambatisho G ubeti 54:3) |
| *At the* ***Orakdance*** | Waliokatika***ngoma*** |

| | |
|---|---|
| | (Kiambatisho G 20:1) |
| *At the* ***ogododance*** | Na mwanamke aringaye **ngomani** |
| | (Kiambatish G28:3) |
| *A young man wears the* ***odye*** *and* ***lacomi*** | Mvulana anavaa **odye** na **lacomi** |
| | (Kiambatisho C ubeti 10:1) |
| *As well as* ***waragi*** | pamoja na **gongo** |
| | (Kiambatisho C ubeti 17:3) |
| *With* ***lugoro*** *and* ***ober*** | Kama **lugoro** na **ober** |
| | (Kiambatisho C ubeti 25:9) |
| *Is* ***lawala*** *not a game*? | ***Lawala*** *si mchezo, na* **bao** *si mchezo*? |
| Is *cooro* not a game? | (Kiambatisho D ubeti 20:6:7) |
| *Is cooked with* ***Lakura*** *or* ***atika*** | pamoja na miti yenye harufu***Lakura*** na ***atika*** |
| | (Kiambatisho E 17:3) |

**4.3.5 Ekolojia: Flora na fauna**

Flora ilihusisha mimea yote ya kiacholi au ya kipindi maalum. Fauna ilihusisha mkusanyiko wa wanyama wote katika mazingira ya Kiacholi. Majina haya pia yalihamishwa kutoka matini chanzi ya Kiacholi na Kiingereza hadi matini lengwa ya Kiswahili. Majina haya hayakuwa na mashiko katika hadhira lengwa. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki wakati mtafsiri alipojaribu kutafuta visawe katika matini lengwa.

Hii hapa ilikuwa ni mifano:-

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *He looks like the a ribe bird* | Anayeitwa **aribe** |
| | (Kiambatisho 2-K ubeti 9:5) |
| *The roots of* ***bomo*** | Mizizi ya **bomo** |
| | (Kiambatisho 2-J ubeti 36:1) |
| *The roots of* ***Ombwoye*** | Mizizi ya **Ombwoye** |
| | (Kiambatisho 2 -M ubeti 2:1) |
| *Eat the roots of* ***lurono*** | Kula mizizi ya **lurono** |
| *Bringt heripe seeds of* ***labikka*** | Leteni mbegu zilizoiva za ***labikka*** |
| | (Kiambatisho 2- M ubeti 2:4) |
| *Fresh wounds treated with* ***ogali*** *or* ***pobo*** | Majeraha hutibiwa kwa **ogali** au **pobo** |
| | (Kiambatisho 2- J ubeti 40:2) |

| | |
|---|---|
| *Like the giant **tido** tree* | Yeye ni kama **mkuyu** mkubwa (Kiambatisho 2-L ubeti 5:11) |
| *Like the dry trunk of the **poi*** | Kama kigogo cha **mti** Kilichokauka (Kiambatisho 2-L ubeti 6:3) |
| *Chew the shoots of **lapena** and **olim*** | Tafuna majani machanga ya **lapena** na **olim** (Kiambatisho M ubeti 7:6) |
| *If the crops are moved down by the **Okwil*** | Kama mazao yakichukuliwa na **Okwil** (Kiambatisho J ubeti 67:4) |
| *The **agogo** bird is silent* | Kwanza **bundi** hunyamaza (Kiambatisho J ubeti 70:11) |
| *The **Obiya grass** is flowering* | Huku na huku **majani** yanachanua (Kiambatisho E ubeti 22:3) |
| *And the **Pollok** blossoms* | Na **vichaka** vinatoa maua (Kiambatisho E ubeti 22:4) |
| *And the **white lilies*** | Na **mauayaporini** (Kiambatisho E ubeti 22:5) |
| *To collect the **red oceyu*** | kutafuta **uyoga mwekundu** (Kiambatisho E ubeti 24:4) |
| *Or to cut **oddugu** shrubs* | Au mboga ya **oduggu** (Kiambatisho E ubeti 24:5) |
| *From the streams of **Lututuru** hills* | kutoka milima ya **Lututuru**(Kiambatisho E ubeti 34:5) |
| *Like the **Okwik** birds* | Kama ndege **Okwik** (Kiambatisho H ubeti 19:4) |
| *In the **lajanawara grass*** | Katika **manyasimarefu.** (Kiambatisho H 20:3) |
| *And threatened to cut the **Okango*** | Kukata mti ule, **okango** (Kiambatisho M ubeti 14:2) |
| *Go on the **apet hunting*** | Kwenda vikundi vikundi **Kuwindaswala** (Kiambatisho G ubeti 52:2) |

| | |
|---|---|
| ***Oywelo** and **lucoro** and **kituba*** | *Miti ya* **Oywelo**,**lucoro** |
| | (Kiambatisho F ubeti 34:1) |
| ***Labwori** is alright* | Mti wa **Labwori** ni safi |
| ***Opok** i seasy* | **Opok** ni mti rahisi |
| ***Yaa** burns gently* | **Yaa** ni mti unaowaka taratibu |
| ***Poi** is no use for firewood* | **Poi** haufai kuni |
| | (Kiambatisho F beti 35 na 36) |
| *Like the ogilo bird* | Sauti ya **tetere** |
| | ( Kiambatisho G ubeti 14:9) |

**4.4 Kubainisha Changamoto za Ujumi**

Jordan(2016) alifafanua nadharia ya Reiss ya tafsiri aliyedokeza kuwa, kuna kaida saba za kudumisha dhana ya ujumi: utafsiri unafaa uwe na mwendelezo usiwe tuli, uwe na ubunifu na uwasiliane kiujumi, uzingatie kaida za mfumo wa kiisimu wa lugha lengwa, uingiliane na muktadha wa ujumbe uwe asili na huru, ukubalike na jamii lengwa na udhamirie kuwa na nafasi katika fasihi ya jamii lengwa., Ujumi ulihusisha urembo katika kazi ya kifasihi.

Katika shairi hili ujumi ulitokea kupitia masuala ya kiisimu na matumizi ya lugha kama vile muundo, mpangilio wa maneno, sauti, toni usambamba na masuala ya matumizi ya tamathali za usemi ambayo yalileta fasili ya dhana akilini. Mtafsiri alipobadili uteuzi wa maneno, mpangilio wa sauti yeye aliathiri ujumi. Masuala ya kiisimu yaliathiri tafsiri kwa sababu zifuatazo: Katika uchunguzi huu tulipata ya kuwa kwa kiwango fulani mtafsiri aliharibu vipengee vilivyotajwa hapo awali hivyo kuupoteza urembo wa shairi. Sababu ni kwamba, muundo wa shairi nzima uliathiriwa pakubwa ambapo katika baadhi ya beti katika shairi la Kiswahili iilikuwa na mishororo mingi au michache ikilinganishwa na matini chanzi.

Tukirejelea kiambatisho 2-A na2- B, tulipata ya kwamba idadi ya mishororo katika matini chanzi ilikuwa 14 na katika matini lengwa mishororo ilikuwa 15. Tuliporejelea alama za uakifishaji tulipata kuwa, kulikuwa na nukta moja. Vipumuo vitatu na nusu kolono moja katika matini chanzi. Katika matini lengwa, kulikuwa na nukta tatu, vipumuo vitatu na nu koloni moja. Hivyo basi, kwa kiwango fulani hapakuwa na udumishwaji wa alama hizi za uakifishaji kwa hivyo, kasi ya shairi haikudumishwa. Mshairi wa Kiingereza aliandika na kupanga maneno kwa njia isiyo ya kawaida ili kulipa shairi sura ya kipekee. Kwa mfano, baadhi ya mishororo ina neno moja tu.

Urembo huu haukudumishwa katika baadhi ya beti.Kwa mfano, kiambatisho 2-B ubeti wa tisa mshororo wa sita. Katika anwani za mashairi ya Kiingereza anwani zilikuwa zimeandikwa kwa njia ya mlazo tofauti na mashairi ya Kiingereza. Hivyo kulikuwa na ukiushi wa kigrafolojia.

Kwa kuangazia sauti tulipata ya kwamba katika matini chanzi takriri konsonanti zilikuwa katika konsonanti zifuatazo:- /m/, /n/, /y/, /t/, /b/, na /s/. Katika matini lengwa takriri konsonanti zilikuwa kama ifuatavvyo:-/m/, /n/, /s/, /h/, /j/ na /b/. Katika matini chanzi, takriri irabu ilikuwa katika irabu zifuatazo:- /u/, /e/, /i/ na /o/. Katika matini lengwa, ruwaza ilikuwa kama ifuatavyo:- /i/, /a/, /e/ na /u/. Kwa kiwango fulani hapakuwa na udumishwaji wa takriri irabu. Shadda katika matini lengwa tofauti na matini chanzi ilipatikana katika silabi ya pili kutoka mwisho.Jambo hili liliathiri wizani au mapigo ya sauti hasa katika sehemu ambazo zilikuwa na urudiaji au usambamba.Hata hivyo, kulikuwa na udumishwaji wa toni nzito ya moja kwa moja, matini wazi yenye kutoa wasifu na yenye uhalisi, maneno sahili na usambamba.

Hata hivyo katika matini chanzi usambamba ulihusisha viwakilishi nafsi huru ilhali katika matini chanzi usambamba ulihusisha viwakilishi nafsi viambata.Jambo hili liliathiri dhana ya msisitizo ambao mara nyingi huwa katika neno la kwanza. Aidha ujumi ulijitokeza kupitia takriri neno. Katika tafsiri baadhi ya takriri neno zilipotea hivyo mapambo ya lugha yalitoweka. (Rejelea kiambatisho 2-A ubeti wa tatu).Aidha mshairi hakudumisha matumizi ya italiki katika anwani za mashairi hivyo kuathiri ujumi(Rejelea kiambatisho 2. Katika kiambatisho 2-B urembo wa Clementine umeupamba shairi asilia kwa matumizi ya sitiari, tashbihi na chuku. Hata hivyo katika tafsiri yya Kiswahili ujumbe uliathirika kwa kukosa kisawe cha Kiswahili kwa mfano, katika ubeti wa kwanza mshororo wa tatu neno ‘*beautiful’* lilipewa kisawe cha ‘mzuri’. Pia katika ubeti wa tatu sitiari ‘red- hot’ imetfsiriwa kama tashbihi ‘kama makaa ya moto unaowaka.’

Pia tulipopiga darubini katika anwani za sura katika shairi hili tulipata kuwa baadhiyazo hazikuleta athari kwa wasomaji kama ilivyokuwa katika matini chanzi kwa sababu kulikuwa na baadhi ya maneno kutoka matini chanzi ambayo yalilazimishwa katika matini lengwa kwa mfano hapa kulikuwa na ukishi wa kileksia:-

i. *The Graceful Giraffe Cannot Become a Monkey /* Hawezi Twiga kugeuka kuwa Nyani (Kiambatisho 2-E). Sitiari hii haikuwa na mashiko kama ilivyokuwa katika matini chanzi kwani matumizi ya lugha ni sehemu ya tamaduni ya lugha husika. Dhana ya "**graceful**" ilipotea katika tafsiri.

ii. *Let them prepare the Malakwang dish /* Hebu wakutengenezee chakula cha Malakwang(Kiambatisho2-M). Neno '*Malakwang'* halikuwa na athari katika matini lengwa bila ufafanuzi zaidi.

iii. *Themother stone has a hollow stomach*/Jiwe-mama lina shimo tumboni. (Kiambatisho 2-F) Neno *jiwe –mama* halina mashiko katika matini lengwa bila ufafanuzi.

iv. *My husband's house is a dark forest of books /* Nyumba ya mume wangu ni msitu mkubwa wa vitabu. (Kiambatisho 2-L) Sitiari hii ni sehemu ya utamaduni wa kiacholi hivyo basi haina mashiko kwa hadhira lengwa.

v. *From the mouth of which river/*Tokamdomowamtogani*?* (Kiambatisho2- I) Anwani hii pia ni sitiari kutoka matini chanzi ambapo walengwa wanafaa waelekezwe.

*vi.* *The last safari to Pagak /* SafariyamwishokwendaPagak. (Kiambatisho2-J).Neno Pagak lina mashiko zaidi katika hadhira ya matini chanzi.

*vii.* *Buffaloes of poverty knock the people down /* Mbogo wa umaskini huwaangusha watu (Kiambatisho2-J). Sitiari hii haina mashiko katika hadhira lengwa.

Kulikuwa na istilahi ambazo zilipatikana katika Kiacholi tu, Kiingereza na Kiacholi lakini hazikupatikana katika Kiswahili. Hii ndio sababu mtafasri alidumisha baadhi ya maneno ya Kiacholi kama yalivyodumishwa na mtafsiri wa Kiingereza. Wakati mwingine mfasiri alilazimika kudondoa, kuchopeka,kudumisha, kutumia visawe kutumia maneno mbadala japo kulikuwa na visawe katika lugha ya Kiswahili au pia kutoa maelezo fulani ya istilahi fulani.

Kwa mfano:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Saltless ash* | Makapi ya magadi (Kiambatisho 2-A ubeti 5:3) |
| ***Ojuu** insect* | Kama **duduvule** (Kiambatisho2- A ubeti 9:4) |
| *The **lyonno** lily* | Mizizi ya **michuga** (Kiambatisho 2-A ubeti 11:2) |
| ***Buffalo** hornet* | Nyigu (Kiambatisho 2-A ubeti 11:7) |
| *Wildcat* | Kimbulu (Kiambatisho2-B ubeti 3:10) |

| | |
|---|---|
| The woman wirh whom<br>I share my husband | Huyo mwanamke<br>**hawala** wa mume wangu<br>(Kiambatisho2-B ubeti 11:10).<br>Hapa kuna udhaifu mtafsiri anapotoa maana ya "*share*" kuwa "hawala" |

Kulikuwa na baadhi ya misemo na jazanda ambazo hazikuleta athari kama ilivyokuwa katika lugha chanzi ta Kiacholi. Kwa mfano:chakula chenye thamani ya juu. Hivyo Ocol alihimizwa asiharibu tamaduni za Kiacholi ambazo zililinganishwa na "boga"(Kiambatisho 2-B).Kulikuwa na tasifida kama vile katika shairi la nane

(Kiambatisho 2-H)

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| *Who has ever prevented The cattle from the saltlick?* | Nani aliyeweza kumzuia ng'ombe<br>Asirambe chumvi? |

Tasfida hii ilikuwa inawalenga wale waliofungiwa kusherehekea ujana wao kwa sababu dini la kikristo haikuwaruhusu. Kulikuwa na methali: *Mboga ulioota mahameni usidiriki kuung'oa*. (Kiambatisho 2-B) Maelezo ya methali hii hayatakuwa na uzito katika matini lengwa ambao hawakuwa na uzoefu wa methali hii. Hapa Lawino alikuwa anamsihi Ocol asidharau mila na desturi ya waacholi. Hapa kulikuwa na ukiushi wa kisemantiki ambapo maana ilihamishwa katika matini lengwa.

Tukiangazia toni tulipata ya kwamba mtafsiri alijaribu kudumisha dhana ya tashtiti. Hata hivyo dhana hii iiathiriwa kwa kiasi fulani kwa sababu alidumisha maneno mengine ya Kiacholi katika tafsiri yake. Kwa hivyo hakuifikia jazba aliyokuwa nayo mwandishi alipoandika shairi hili.Shairi ni tungo lililotiririsha taswira, mawazo na ujumbe kwa lugha nzito ya mkato, yenye mnato wa maana. Umbo la shairi lilirejelea idadi ya beti zake. Hata hivyo, kila ubeti ulifaa kuwasilisha ujumbe kamilifu uliowiana na maana ya shairi nzima. Hata hivyo kulikuwa na changamoto katika mishororo ifuatayo: (Kiambatisho2-H ubeti 16:10-14).

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| “*Maria the **clean** woman* | Maria **Mtakatifu** |
| *Mother of the **Hunchback*** | Mama wa Mungu |
| *Pray for us* | Utuombee |
| *Who **spoil** things* | Sisi wakosefu |
| *Full of **Graciya**.*” | Uliyejaa neema.” |

Matini chanzi ni kinaya na imetumia lugha ya mzaha kimakusudi. Mtunzi wa ubeti huu analenga kukejeli imani na mafunzo ya Kikatoliki. Matini tafsiri imepuuza dhamira hii nabadala yake ikatumia lugha ya kawaida ya heshima na uungwana. Kwa kufanya hivi, tafsiri imeikaidi dhamira na mwelekeo wa mwandishi wa matini chanzi. Hapa kulikuwa na ukiushi wa kisemantiki.

### 4.5 Hitimisho

Ni dhahiri kwamba, vipengee vya kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi visipotiliwa maanani na mtafsiri katika mchakato wa kutafsiri basi kutakuwa na vijisehemu ambavyo havitatafiriwa kikamilifu, kutafsiriwa kupita kiasi cha haja au kutotafsiriwa.Matokeo ya utafiti huu ni kuwa kulikuwa na changamoto za tafsiri zilizoathiri tafsiri ya *Wimbo wa Lawino* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.Kutafsiri lugha moja kwa lugha nyingine huwa jambo lisilokuwa rahisi haswa kama ni ushairi. Ilikuwa vigumu kupata istilahi za Kiswahili zilizolingana na istilahi zilizotumiwa katika Kiacholi na Kiingereza.

Ni dhahiri kuwa kulikuwa na mawazo mengi katika mashairi ya Kiingereza yaliyoelezea mawazo ambayo hayakuwapo katika Kiswahili wala katika ustaarabu wa Waswahili.Lugha ya shairi ilikuwa na matumizi ya maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana yasiyo ya kawaida. Hii ilikuwa ni sifa muhimu ya kisemantiki ya lugha hii ya shairi. Pia lugha hii haikuwa wazi kwa hivyo ilileta utata katika kubaini maana.Sifa ya kipragmatiki ilikuwa ni sifa nyingine ya kiisimu iliyoathiri tafsiri za kishairi. Maneno katika lugha ya kishairi yalitofautiana katika maana na yalileta athari tofauti kutegemea ni nani aliyasema, aliyesemea wapi na aliyasema lini. Jambo jingine lililozingatiwa la kipragmatiki lilikuwa ni utata, usio dhahiri na shaka zilizopatikana katika matini za shairi.

Kauli zingine za kishairi zilihitaji ufafanuzi wa kishairi ili kuelewa kilichomaanishwa. Kulikuwa na sifa zingine ambazo ziliathiri tafsiri za kishairi. Mojawapo wa sifa hizi ilikuwa ni tofauti za mifumo ya kishairi ya lugha chanzi na lugha lengwa. Mfumo wa kishairi ulifungamana sana na utamaduni wa watu na historia yao. Dhana za kishairi, mila na desturi zilitofautiana kutegemea jamii husika. Kutafsiri shairi kulihusisha kutafsiri kutoka mfumo mmoja wa shairi hadi mwingine. Mfumo wa kishairi wa Kingereza ni tofauti sana na mfumo wa kishairi wa Kiswahili hivyo kuendeleza utata katika kutafsiri.

Baadhi ya mapendekezo kwa mtafsiri ni kama vile:-

i. Kuhamisha istilahi jinsi zilivyo katika matini chanzi endapo hakuna visawe katika matini lengwa ili kuepuka kupotosha maana
ii. Mtafsiri awe na umahiri wa kiisimu, kitamaduni na kiujumi ili asiwapotoshe wasomaji.
iii. Awe na tajriba na uzoefu wa kufahamu miundo ya kishairi katika matini lengwa na matini chanzi ili aweze kubaini mbinu mwafaka ya kuhamisha ujumbe .

# SURA YATANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii iliangazia sehemu tatu kuu yaani, muhtasari kulingana na maswali yautafiti, mahitimisho na mapendekezo kwa mtafsiri na mapendekezo ya utafiti zaidi..Ugumu au changamoto za kutafsiri mara nyingi ulitokana mtazamo wa mwandishi mwenyewe, kuhusu maana na ujumbe. Mwandishi alidhamiria kutimiza moja wapo au zaidi ya baadhi ya malengo: kuarifu, kuelimisha, kushawishi au kutumbuiza.

## 5.2 Muhtasari

Mtafiti alipata ya kwamba kulikuwa na changamoto za kiisimu ambapo sababu kuu zilikuwa ni kwamba lugha hizi mbili zilikuwa na tofauti ya kiisimu kwa misingi ya fonolojia, mofolojia na sintaksi. Kadhalika kulikuwa na utofauti katika istilahi. Jambo hili lilipelekea mfasiri kudumisha baadhi ya maneno, kuchopeka, kudondoa au kutoa maelezo zaidi katika tanbihi.Kulikuwa na changamoto katika matumizi ya lugha. Mtafiti alipata kwamba masuala kama tamathali za kiusemi na tamaduni jamii hayakutumika katika jamii lengwa kama ilivyokuwa katika jamii chanzi. Hii ni kwa sababu, kila lugha ilikuwa na tamathali zake za usemi mahsusi na tamaduni tofauti. Hivyo kulikuwa na mabadiliko katika uteuzi wa maneno na mpangilio wa sauti.

Tatizo hili lilihusu majina mengi yaliyoeleza mahusiano ya watu katika familia, kwa sababu tamaduni za kimagharibi zilibainisha maana hizi kiwango tofauti na tamaduni kama zile za Kiafrika.Kulikuwa pia na changamoto za kiujumi ambazo zilichangiwa na changamoto za kiisimu na za matumizi ya lugha. Ujumi ulilenga hasa suala la maana katika muktadha mahsusi (Pragmatiki). Mtafiti alipata ya kwamba jamii lengwa haikupata athari sawa kama ilivyokuwa katika jamii chanzi. Hii ni kwa sababu kulikuwa na istilahi hasa zilizohusiana na masuala ya tamaduni jamii ambazo zililazimishwa katika matini chanzi. Kwa hivyo, ushairi kama utanzu wa fasihi ulichimbuka kutoka tamaduni maalum.

Utamaduni wa jamii husika ulikuwa ni chimbuko la maudhui ya ushairi na vipengee vya fani kama vile picha, ishara na tamathali nyingine za usemi. Mtafiti alipata kwamba, tafsiri ya kishairi iliweza kuhasirika na kunufaika kutokana na tofauti kati ya utamaduni wa shairi la awali na utamaduni wa shairi la pili. Kulitokea baadhi ya picha na ishara kukosa maana katika utamaduni wa pili.

Kwa mfano, kulikuwa na majina ya mimea na wanyama yenye maana katika lugha ya Kiacholi ambayo yalillazimishwa katika Kiingereza na Kiswahili. Kwa muhtasari, kulikuwa na uwiano kati ya lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili na katika tamaduni za lugha hizo mbili. Hii ndio sababu mfasiri aliweza kufanya utafsiri.

Kadhalika, kulikuwa na utofauti kati ya lugha hizo mbili. Tofauti hizi ndizo zilizoibua haja ya kutafsiri ili kufanikisha mawasiliano kati ya wasemaji wa lugha hizo mbili. Hata hivyo, tofauti hizi ndizo zilizosababisha ugumu wa kutafsiri. Sababu ni kwamba, katika ushairi kulikuwa na uwiano kati ya fani na maudhui ambazo zilileta mguso kwa mlengwa kwa njia maalum. Tofauti kati ya lugha moja na nyingine; mfuatano wa sauti na maneno, tofauti kati ya kaida za kishairi kati ya lugha moja na nyingine na ya utamaduni kati ya walengwa, haikuwezekana kuwa na uhusiano wa fani na maudhui kujitokeza bayana katika lugha ya pili.

**5.2.1 Kubainisha Changamoto kiisimu**

Kimaandishi tulipata kwamba lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza zilikuwa tofauti kwani kila lugha ilikuwa na mfumo wake. Lugha ya Kiingereza ilikuwa ya mfumo funge ilhali ya Kiswahili ilikuwa ya mfumo wazi. Kadhalika, Kiswahili tofauti na Kiingereza kilikuwa ni lugha ambatanishi. Lugha ya Kiingereza ilifuata mfumo wa unyumbuaji. Jambo hili lilipelekea kuwe na athari katika wizani au mita hivyo muundo wa mishororo ulibadilika katika baadhi ya beti. Mtafsiri alidumisha umbo la mashairi ambao ulikuwa huru. Kulikuwa na udumishaji wa mistari mishata na mistari kifu katika tafsiri. Katika sauti vokali za Kiswahili tofauti na za Kiingereza zilikuwa fupi na hazikuunganishwa.Katika kitengo cha mshikamano, kulikuwa na urudiaji uliodumishwa katika vitengo mbali mbali vya maneno lakini katika tafsiri ya Kiingereza kulikuwa na uradidi wa viwakilishi nafsi huru. Mkao wa fonti katika Kiingereza ulikuwa tofauti na ule wa Kiswahili. Idadi ya mishororo katika shairi la Kiingereza ilikuwa ni tofauti katika baadhi ya beti.

Katika uakifishaji kulikuwa na utofauti ambapo katika baadhi ya mishororo alama za kuakifisha hazikudumishwa. Katika kipengele cha vina, shairi la Kiingereza lilikuwa na urudiaji katika vina vya mwisho katika baadhi ya beti.Katika Kiswahili ruwaza hii ilibadilika na badala yake uradidi ulikuwa mwanzoni mwa baadhi ya mishororo hiyo. Katika kiwango cha ujulishaji tulipata ya kwamba kutokana na utofauti wa kileksia na kisintaksia katika Kiingereza na Kiswahili kulikuwa na mabadiliko katika usambazaji wa maelezo.

Kwa ujumla kulikuwa na ukiukaji wa kigrafolojia ambapo katika shairi la Kiingereza kingo za mishororo katika upande wa kushoto hazikuwa sambamba kama ilivyokuwa katika tafsiri ya Kiswahili.Mtafsiri pia aliunganisha baadhi ya mishororo hivyo hakudumisha muundo wa shairi katika baadhi ya beti. Tafsiri ya ukiushi wa kimofolojia na kifonolojia ulikuwa tata kwa sababu ya tofauti za muundo katika lugha mbili ambazo hazina uhusiano wa karibu. Mathalan, kanuni za uundaji wa maneno katika lugha asilia na lugha pokezi ni tofauti. Mtafsiri alilazimika kutumia muundo unaokubalika katika lugha pokezi. Mtafsiri aliunda visawe katika lugha pokezi na kuwa na takriri ya silabi tofauti.

### 5.2.2 Kubainisha Kubainisha Changamoto za matumizi ya lugha

Kulikuwa na changamoto za matumizi ya lugha. Lugha ya Kiingereza haikuweza kubeba tamaduni nyingine yaani ya Kiacholi na ya Kiswahili. Matumizi ya lugha yaliambatana na mila na desturi ya kijamii. Msamiati ulifungamana na utamaduni. Usahihi wa matumizi ya lugha ulifungamana na misingi ya kijamii. Tafsiri iliathiriwa na matumizi ya lugha kwa misingi ya ekolojia, violwa, mila na desturi siasa na dini. Matatizo ya kutafsiri semi, nahau visawe, na mafumbo yalizuka katika nadharia ya kiisimu.Kulikuwa na tashbihi iliyofungamana na tamaduni ya waacholi. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki na wa kilahaja pale ambapo mtafsiri alishindwa kupata visawe katika matini lengwa.Mtafsiri alilazimika kuhamisha misimu na majina ya Kiacholi ambayo hayakuwa na mashiko katika matini lengwa. Hapa kulikuwa na ukiukaji wa kilahaja. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki alipojaribu kubadilisha maneno hayo na visawe katika matini lengwa.

Majina ya flora (ilihusisha mimea yote ya Kiacholi au ya kipindi maalum) na fauna (ilihusisha mkusanyiko wa wanyama wote katika mazingira ya Kiacholi) yalihamishwa kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Majina haya hayakuwa na mashiko katika hadhira lengwa. Kulikuwa na ukiukaji wa kisemantiki wakati mtafsiri alipojaribu kutafuta visawe katika matini lengwa.Tafsiri iliegemea upande wa mawasiliano, nadharia ya mawasiliano ilifaa zaidi kukidhi ufinyu wa kiisimu. Katika utafiti huu, tofauti hizi ndizo zilizosababisha ugumu wa kutafsiri shairi.

### 5.2.3 KubainishaChangamoto zaUjumi

Kulikuwa pia na changamoto za kiujumi ambazo zilichangiwa na changamoto za kiisimu na za matumizi ya lugha. Ujumi ulilenga hasa suala la maana katika muktadha mahsusi (Pragmatiki).

Suala lingine lililopelekea kuwe na changamoto ya ujumi lilikuwa ni kutafsiri toni ya lugha chanzi. Toni ilikuwa ni msimamo wa mshairi kuhusu ushairi wake:Iwapo dhamira ilikuwa ni kuchekesha, kutilia chumvi, kutoeleza kikamilifu au kuonyesha ukweli wa mambo.

Mtafiti alipata ya kwamba jamii lengwa haikupata athari sawa kama ilivyokuwa katika jamii chanzi. Hii ni kwa sababu kulikuwa na istilahi hasa zilizohusiana na masuala ya tamaduni jamii ambazo zililazimishwa katika matini chanzi. Kwa hivyo, ushairi kama utanzu wa fasihi ulichimbuka kutoka tamaduni maalum.Suala la kiisimu liliathiri ujumi kwa sababu kama: kwa mfano kwa uchunguzi huu tulipata mfasiri aliharibu vipengee vilivyotajwa hapo awali hivyo kuupoteza urembo wa shairi kwa kiwango fulani. Hii ni kwa sababu  muundo wa shairi nzima uliathiriwa pakubwa ambapo katika baadhi ya beti katika shairi la Kiswahili iilikuwa na mishororo mingi au michache ikilinganishwa na matini chanzi.

Katika kuangazia alama za uakifishaji  kulikuwa na utofauti katika baadhi ya beti. Kwa kiwango fulani hapakuwa na udumishwaji wa alama hizi za uakifishaji kwa hivyo, kasi ya shairi haikudumishwa. Mishororo mingine iliunganishwa katika tafsiri.Kulikuwa na baadhi ya misemo, na jazanda ambazo hazikuleta athari kama ilivyokuwa katika lugha chanzi. Kulikuwa pia na istilahi ambazo zilipatikana katika Kiingereza na Kiacholi lakini hazikupatikana katika Kiswahili. Aidha kuna baadhi ya takriri neno ambazo hazikudumishwa katika tafsiri ya Kiswahili.Kwa kufanya hivi, tafsiri imeikaidi dhamira na mwelekeo wa mwandishi wa matini asili.Tofauti hizi ndizo zilizosababisha ugumu wa kudumisha ujumi.Ujumi uliathiriwa katika shairi wakati mshairi alipojaribu kuhifadhi maana ya kishairi. Kiswahili na Kiingereza ni lugha mbili zilizo katika mifumo tofauti ya kishairi na vilevile tamaduni tofauti za kijamii.

Totauti hizi  ndizo zilileta tofauti za mawazo. Kiingereza kilipotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ilikuwa ni taabu sana kuweza kuhamisha maana yote kwa ukamilifu na kuyatia katika hiyo lugha nyingine bila kupunguka hata kidogo. Jambo la kutiliwa mkazo ni kuwa ule upungufu wa maana usiwe mwingi hadi kugeuza sura ya maana asili.

**5.3 Hitimisho**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuonyesha iwapo kulikuwa na changamoto za kiisimu, matumizi ya lugha na ujumi katika tafsiri ya *WimbowaLawino* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Kutokana na utafiti huu ni dhahiri kwamba kulikuwa na changamoto za kiisimu zilizopelekea kuwe na changamoto za matumizi ya lugha na ujumi katika kutafsiri ushairi wa*WimbowaLawino* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Kupitia uchanganuzi wa matini, matokeo yalionyesha kwamba, utafsiri katika kiwango cha matini ulikuwa na mafanikio kwa kiwango fulani. Hata hivyo, katika kiwango cha nje ya matini, matokeo hayakuwa hayo. Shairi lilikuwa na istilahi nyingi za Kiacholi na sio istilahi zote ambazo ziliweza kufafanuliwa au kupatiwa visawe na mtafsiri.Tafsiri ya shairi lazima ingekuwa na upungufu ambao ungeathiri sana fani kuliko maudhui. Iwapo mtafsiri alitafsiri shairi kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi, lugha iliyotumiwa katika tafsiri ilikuwa nakala tu ya miundo ya tungo za kishairi ya lugha ya awali.Ni dhahiri kwamba, tafsiri iliyotafsiriwa haikuwa na mashiko kama ilivyokuwa katika matini chanzi.Jambo hili lilipelekea sehemu nyingine zisieleweke. Karibu tamathali zote za usemi zilitafsiriwa kwa mfumo wa tafsiri sisisi. Kama ilivyokuwa katika matini chanzi tafsiri ya shairi hapakuwa na sifa za kiarudhi ila kulikuwa na sehemu kadhaa ambazo zilikuwa na uradidi na usambamba. Toni ya shairi ilikuwa ya tashtiti. Ujumbe wa shairi ulikuwa ni kutuhamasisha dhidi ya ukengeushi.

Kwa kuhitimisha, tafsiri haikuwa tu mchakato wa kiisimu bali pia ilikuwa ni mchakato uliojumuisha masuala yaliyohusu utamaduni ulioathiri ujumi. Utofauti wa kitamaduni katika matini chanzi na matini lengwa uliweza kufanya shairi lililotafsiriwa kuhasirika au kunufaika kiasi cha kulifanya shairi lililotafiriwa kuwa jipya.

### 5.4 Mapendekezo kutokana na utafiti

Ingawa kuna kazi nyingi zimefanywa kuhusu ushairi ilibainika kuwa tafsiri ya mbinu zingine katika ushairi ziinaweza kuchunguzwa.Tafsiri za mashairi kutoka lugha moja ya kienyeji hadi nyingine ni chache sana. Wengi hupendelea kutafsiri kutoka lugha moja ya kienyeji hadi lugha kuu mathalan, Kiingereza. Hivyo, kuna pengo katika nyanja ya kutafsiri kazi za fasihi.
Katika maisha ya kisasa ambapo kuna masuala yanayohusu teknolojia na mawasiliano ya jamii mbalimbali na tamaduni tofauti, utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kuzindua vifaa vitakavyotumika na mbinu za kimatini zinazotumika kukidhi mahitaji ya kutafsiri masuala mbalimbali yanayohusu watu wa makabila tofauti.

## MAREJELEO

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19$^{th}$ Century Popular Swahili Poetry*. London: Oxford Press.

Abedi, A. (1954). *Sheriaza Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Achebe, C. (1975). *The African Writer and the English Language.* New York: Doubleday.

Adiel, M. S., & Ahmed, M. A. (2016). Problems in Translating Metaphorical Expressions. *ARC Journals*, 3(6), 46-50.

Adungo, C. (2018). *Fasili Mbalimbali* za *Dhanashairi*. Retrieved from www.swahilihub.com

Alpha Omega Translation. (2012). *Region Change through Word Exchange*: *The Need for Translation in Africa*. Retrieved from https://alphaomegatranslations.com/business-translation/region-change-through-word-exchange-the-need-for-translation-in-africa/

Andnesen, S. (2015). *Think Tank*. Retrieved from https://www.taus.net>thinktank>articles

Andrews, P. (2014). *The Importance of Content Translation in Creating Global Sites.* Retrieved from https://dzone.com/articles/importance-content-translation

Arberry, A. J. (1945). *Kings and Beggars*: *The First Two Chapters of Sadi's Gulistan.* London: Luzac and Co.

Babbie, E. (1992). *The Practice of Social Research* (6$^{th}$ ed.). Carlifonia: Wadsworth Publishing Company.

Babusa. H. O. (2005). *Vigezo Badilia Kuhusu Uainishaji wa Mashairi ya Kiswahili.* Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Baker, M. (1992). *In Other Words: A Course Book in Translation*. London: Routeledge.

Balikumi. B. (2017). *Isimu,* Retrieved from https://kijuekiswahili.wordpress.com.

Bassnett, S. (1991). *Translation Studies*. London and NewYork: Routledge.

Beaugrande, R. A.. & Dressler, W. U. (1981). *Introduction to Text Linguistics*. London: Longman.

Bell, R. A. (1991). *Translation and Translating: Theory and Practice*. London: Longman Group Ltd.

Berghout, A. (2005). *Lectures at Newcastle University. Retrieved from https://www.translationdirectory.com/articles/article2019.php*

Bhana, Y. (2014). *The Challenges of Translating for African Audiences,* Retrieved from https://www.translatemedia.com.

Buliba, F. A. (2001). *Lugha, Utamaduni na Jamii katika Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa katika Kiswahili*: A Tool for Develelopment- The Multidisplinary Approach. Eldoret: Moi University Press.

Catford, J. C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. New York: Oxford University Press.

Chacha, N. (1987). *Meaning and Interpretation of Swahili Poetry*: A Potrayal of Changing Society. Tasnifu ya Ph.D, Yale University (Haijachapishwa)

Cherry, K. (2018). *Sample Types and Errors in Research*. Retrieved from https://www.verywellmind.com

Chomsky, N. (1965). *Syntactic Structures*. The Hague: Mouton.

Clark, H., & Brennan, S. E. (1991). *Grounding in Communication.* In L. B. Resnick, J. M. Levine, & S. D. Teisley (Eds.); *Perspective on Socially Shared Cognition*. Washington, D. C: American Psychological Association.

Cohen, L., Manion, L. M., & Morris, K., (2000) *Research Methods in Education*. London: Routledge Falmer.

Cruz, U. S. (2017). *What is Linguistics*? Retrieved From linguistics.usc.edu.

Crystal, D. (1980). *A First Dictionary & Phonetics,* Colorado: Westview Press Boulder.

Cudden, J. A. (1976). The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory. England: Penguin Reference

Dastjerdi, H. V. (2004). S'adi's Oneness of Mankind Revisited. *Translation Journal,* 8 (4). Retrieved from https://www.translationdirectory.com/article231.htm

Dingwaney, A., & Maier, C. (1995). *Between Languages and Cultures: Translation and Cross Cultural Texts.* Pittsburgh: U of Pittsburg P.

van Dijk,. T. A. (1997). *The Study of Discourse.* In T. A. van Dijk (Eds.). *Discourse as Structure and Process*. London: Sage.

Donovan, J. (2009). *A Glance at Swahili Poetry*. Retrieved From www.tzaffairs.org.

Enyaga, E. (2019). *Sanaa Katika Tafsiri*: *Matatizo na Athari Zake*. Retrieved from sifeheifers.org.

Felix, D. L. (2018). *Aina za Mashairi.* Retrieved From swa.gafkosoft.com

Firth, J. R. (1951). *General Linguistics and Descriptive Grammer. Retrieved* from https://doi.org/10.111/j.1467-968x.1952.tb0249.x.

Flanagan, M. (2018). *What is Poetry? An Introduction.* Retrieved from https://www.thoughtco.com

Fowler, R. (1966). The Formaulaic Theory and its Application to English Alliterative Poetry. In Fowler, R. (Mh.) *Essays on Style and Language.* London: Routledge & Kegan.

Gay, L. R., Mills, G. E., & Airasian, P. (2006). *What is Stanza*. Retrieved from http://www.poewar.com/what-is-a stanza

Gessman, T. (2017). *The Most Common Challenges with Translations*. Retrieved from https://samedaytranslations.com

Gikandi, S. (1991). *Reading Chinua Achebe: Language, Ideaology and Fiction.* Nairobi: Heinemann.

Gyasi, K. A. (1996). *Writing as Translation: Translation and the Post-Colonial Experience: The Francophone African Text.* Ohio State University: Diss.

Halliday, M. A. (1994). *An Introduction To Functional Grammer*. Edward Anorld: London.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry.* London: Oxford University Press.

Hariyanto, S. (2018). Problems in Translating Poetry. Retrieved from https://www.researchgate.net

Hariyanto, S. (2015). Text Linguistics and Skopos: Theory and Their Applicationin Translation Teaching. *Jurnal Linguistik Terapan,* 8(1), 56-67.

Hatim, B., & Mason, I. (1990) *Discourse and the Translator.* London: Longman.

Heron, G. A. (1984). *Introduction to the Heinemann African Writers Series Edition of Song of Lawino and Song of Ocol*. Oxford: Heinemann.

Hitchens, W. (1962). *Inkishafi*. London: Oxford University Press.

Hymes, D. (1974). *Foundations of Sociolinguistics: An Ethnographic Approach.*.Philadelphia*:* U of Pennslyvania.

Musleh, B. (2019). *Lexical selection and archaisms in three English translations of the Sūrat Yūsuf (the Chapter of Joseph): A comparative linguistic and empirical investigation* (Doctoral dissertation, University of the West of England).

Kadkani, M. R. (2001). *The Music of Poetry*. Tchran: Aagach Press.

Kandoro, S. A. (1983). Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Shairi la Kiswahili. Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III,* Fasihi. Dar es Salaam. TUKI.

Kaviti, F. M. (2005). *Makosa ya Kisintaksia Katika Tafsiri za Makala Gazetini*. Retrieved From erepository.uonbi.ac.ke

Keenan, E. (1978). "Some Logical Problems in Translation." Katika Guentuner, F na G-Reutter Wan. (1978). *Meaning and Translation Philosophical and Linguistic Approaches.* London: Duckworth.

Khatibi, M. (2016). *Challenges of Literary Translation*: *Kahlil Gibran's the Prophet as a Case Study*. Retrieved from https://papers.ssm.com

King'ei, G. K. (2007). "*Athari za Washairi Wakongwe juu ya Washairi wa Kisasa:* Mfano wa Muyaka bin Haji na Ahmed Nassir." Katika *Kioo cha Lugha,* Juzuu la 5. Dar es Salaam: TUKI.

Koop, M. (2003). *Poetry in Translation.* Retrieved from https://www.poetryintranslation.com/

Kroulek, A. (2016). *Why Translation is Important in an English Speaking World- K International.* Retrieved from https://www.k-international.com

Kuvuna, S.M, Mvati, M.N., & Maliachi P.A. (1992). *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Labov, W. (1966). *The Social Stratification of English in New York City.* Washington D.C: Center for Applied Linguistics.

Larson, M. L. (1984). *Meaning-Based translation. A Guide Based To Cross Language Equivalence.* New York: University press of America.

Laura, H. (2016). *What Makes Poetry Translation Different*. Retrieved from languagebylaura.com

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman.

Lefevere, A. (1975). *Translating Poetry*: *Seven Strategies and A Blue Print*. Asse: Van Gorcum.

Lehmann, W. P. (1978). *Syntactic Typology*: *Studies in The Phenomenology of Language*. Texas: University of Texas.

Libert, A. (2005) Lectures at Newcastle University.

Liyong, T. (2001). *The Defence* of *Lawino*. Fountain Publishers: Uganda.

Maaitah, E. (2017). Speech Act Theory, Retrieved from https://www.docsity.com

Macmahon, B. (2009). *The Handbook of English Linguistics*. Oxford: Blackwell.

Massamba, D. (1983). *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili*. *Fasihi* [Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili III], imehaririwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: 55-94.

Mason, I. (2001). *Text Parameters in Translation, Transitivity and Institutional Cultures. Translation Studies.* Theories and Applications. London: Routledge.

Mathieu, M. (2015). *Lexical-Semantic problems,* Retrieved from https://culturesconnection.com

Mayoka, J. M. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mberia, K. (1990). *Umbo la Mashairi*. *Mwamko* 5 [Jarida La Chama Cha Kiswahili Chuo Kikuu Cha Nairobi]: 80-111.

Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mbonea, E. (2017). *Jicho la Arusha*: *Kwaheri Paul.* Retrieved from https://jicholaarushablogspot.com

McIntosh, A., & Halliday, M.A. (1964). *Syntax and The Consumer*. Washington DC: Georgetown University Press.

Medhat, V. (2011). Linguistic Deviationin Poetry. *Journal of Language Teaching and Research*, 2 (6), 1329-1336.

Mnyapala, M. (1965). *Diwani ya Mnyamplepa*. EALB: Nairobi.

Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainikakatika Ushairi wa Kiswahili.* Tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mule, K. (2002). Translation, Mistranslation & Culture: African Inflections, Challenges and Prospects. *Journal of African Cultural Studies*, 16(2), 143-159.

Mulokozi, K. & Kahigi, K. (1979). *Kungaza Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M., & Kahigi. K. K. (1982). *Kutungaza Ushairi na Diwani Yetu*. TPH: Dar es salaam.

Mulokozi, M. M (2008). "*Nadharia ya Jadiya Ushairi wa Kiswahili: Je Upo?"* Katika Ogechi N.O, Shitemi, N.L. na Simala, K.I. (Wah.) *Nadharia ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press.

Mlamali, M. (1980). *Inkishafi*. *Ikisiri ya Muhamadwa Mulamali*. Nairobi: Longman.

Munday, J. (2001). *IntodocingTranslationStudies*. *Theories and Applications*. London & New York: Routeledge.

Mutugi, K. (2010). *Tathmini ya Tafsiri Kutoka Kiswahili hadi Kipsigis*. Retrieved from erepository.uoni.ac.ke

Mwai, W. (1988). *New Trends in Ushairi*. Tasnifu ya Kupata Digrii ya Uzamili (M.A.) ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

Mwalimu wa Kiswahili. (2016). *Tafsiri.* Retrieved from https:// mwalimuwakiswahili.com.tz.

Mwansonko, H. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Nastasi, A. (2013). *20 Poets on the Meaning of Poetry*. Retrieved from flavorwire.com.

Ndumaro. (2013). *Dhana na Dhima ya Ushairi wa Kiswahili*. Retrieved from chomboz. blogspot.com.

Newmark, P. (1981). *Approaches To Translation*. Oxford: Pergamon press.

Njogu, K. & Rocha C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta.

Niknasab, L., & Pishbin, E. (2011). On the Translation of Poetry: A look at Sohrab Sepehri's Traveller-SKASE. Retrieved from www.skase.sk

Nida, E. A., & Taber, C. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E. J. Brill.

Nord, C. (1997). *Translation as a Purposeful Activity.* Manchester: St. Jerome.

Nyaga, M. N. (2012). *Dhanaya Ulinganifu Katika Tafsiri ya Fasihi*;*tathmini ya usaliti mjini*. Retrieved from www.researchkenya.or.ke

Nyerere, J. K. (Trans.) (1969). *MabepariwaVenisi*. (The Merchant of Venice by William Shakespear). Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (Trans.) (1963). *Juliasi Kaizari*. (Julius Caeser by William Shakespeare). Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (Trans.) (1996). *Utenzi wa Enjili:Kadiri ya Utungo wa Luka* (Gospel of Luke). Ndanda, Tanzania: Benedictine Publication.

Okere, B. (2018). Linguistic Challenges in Translating Song of Lawino from English to Kiswahili. *International Journal of Literature and Translation,* 1(4), 58-62.

Okot, P' B. (1972). *Song of Lawino*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Omboga, Z., & Michira, N. (2006). *Vitendi Usemi na Ulinganifu wa Maana Katika Tafsiri*. Retrieved from https://www.academia.edu.

Orthofer, M. A. (2015). *Song of Lawino and Song of Ocol- Okot p'Bitek*- Complete review. Retrieved from www. Complete-review.com

Osman, A. (2017). *Defination of Translation*. Retrieved from https://translationjournal.net

Paltrige, B. (2012). *An Introduction to Discourse Analysis* ($2^{nd}$ ed.). Abingdone: Routeledge.

Renatus, L. (2017). *Dhana ya Ushairi Ilivyofafanuliwa na Wataalamu Mbalimbali*. Retrieved from leonardrenatus.blogspot.com

Renee, E. (2016). *Why is Translation Important*?*Publishing African Literature Across Languages*. Retrieved from https://africainwords.com

Robert, S. (1958). Hotuba Juu ya Ushairi. *Journal of the East African Swahili Committee*, 28(1), 37-42.

Robert, S. (1968). *Ushairi na Utofauti wa Mawazo juu ya maana ya ushairi*. Retrieved from Manyama 1.blogspot.com.

Roy, M. (2014). *Ushairi wa Kiswahili Kuanzia Karne ya 16 Mpaka Karne ya 20*. Retrieved from https://www.researcggate.net

Rwezaura, B. (2009). Constrainung Factors to the Adoption of Kiswahili as a Language of the Law in Tanzania. Retrieved from https://www.cambridge.org/core/journals/journal-of-african-law/

Sausssure, F. (1966). *Course in General Linguistics*. New York: Mc Graw-Hill.

Savory, T. (1968). *The Art of Translation*, London: Jonathan Cape Lt.

Scott, J. (2009). *Contemporary Theories on Translation:Octavio Paz.* Retrieved from translation-blog.trustedtranslations.com.

Searle, J. R. (1977). *Metaphor in A. Ortony (ed.)Metaphor and Thought.* Cambridge: Cambridge University Press.

Shannon, C. E., & Weaver, W. (1949). *The Mathematical Theory of Communication*. Urbarc: University of Illinois Press.

Silverman, D. (2001). *Interpreting Qualitative Data*. London: Sage.

Sozigwa, P. (1975). *Wimbo wa Lawino*. Nairobi: Afropress Ltd.

Stockinger, P. (2003). *Semiotics of Cultures, Culture, Language and Translation*. Paris: EscoM.

Suryawanita, Z. (1982). *Analisisdan Evaluasiterhadap Terjemchan Novel Sasra the Adventure of Huckleberry Finndari Bahasa Ingrisske Bahasa Indonesia*. Unpublished Desertation, IKIP: Routeledge.

Taylor, T. J., & Cameron, D. J. (1987). *Analysing Conversation*. Oxford: Pergamon.

Tesson, K. J. (2002). *Dynamic Networks. An Interdisciplinary Study of Network Organisation in Biological and Human Social Systems*. PHD. Thesis.

Topan, F. (1974). *Dibaji* Katika Kezilahabi, Kichomi. Nairobi: Heinemann.

Troolin, T. (2015). *Form and Meaning in Poetry.* Retrieved from https://study.com.

Venuti. L. (2000). *The Translation Studies Reader*. London: Routeledge.

Vermeer, H. J. (2000). *Skopos and Commission in Translational Action pp.227-237*. Translation Studies Reader. (2nd ed.). NewYork: Routledge.

Vinay, J. P., & Darbelnet, J. (1995). *Comparative Stylistics of French and English:A Methodology for Translation.* Amsterdam/ Philadephia: John Benjamins.

Wamitila, K. W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. English Press: Nairobi.

Wangari, M. (1988). *Mabadiliko Katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi*. Retrieved from www.qucosa.de.

Wanjala, W. (2011). *Tofauti Kati ya Ukalimani na Tafsiri.* Retrieved from tunuzakiswahili.blogspot.com.

Wanjiru , M. (2018). *Isimu Pamoja na Matawi Mbalimbali ya Isimu Katika Kiswahili*. Retrieved from www.swahilihub.com

Wardhaugh, R. (1985). *How Conversation Works*. Oxford: Basi; Blackwell.

Walsh, V. (2017). *What Makes a Good Translation*? Retrieved from https://theopenmic.co.

Wills, K. W. (2017). *How to Define Research Design*. Retrieved from https://penandthepad.com.

Wrong, M. (2017). Overturning the Hierarchy of Languages, Retrieved from https://www.the-tis.co.uk.

Zhang, M. (2015). *Introduction to Discourse Analysis in Translation Studies*. Retieved from https://researchgate.net.

## KIAMBATISHO 1 :Umbo

| MATINI CHANZI | MATINI LENGWA | MATOKEO |
| --- | --- | --- |
| 1.***Myhusband'stongu eisbitter***<br>Aina: Huru | 1.**Ulimiwamumewanguni mkali**<br>Aina: Huru | Ilidumishwa |
| **Muundo:** Ruwaza sahili | Muundo: Ruwaza sahili | Ilidumishwa |
| **Mishororo** | | |
| Ubeti 1: Mishororo 14<br>Ubeti 3: Mishororo 4<br>Ubeti 5: Mishororo 5 | Ubeti 1: Mishororo 15<br>Ubeti 3:Mishororo 5<br>Ubeti 5: Mishororo7 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa<br>Haikudumishwa |
| **Uakifishaji:** | | |
| Ubeti 1: .(1), , (3), ;(1)<br>Ubeti 3: , (2), ! (2), ; (0)<br>Ubeti 5: , (1), * (1), ;(1), ?(1) | Ubeti 1: . (3), , (2), ; (1)<br>Ubeti 3:, (2), ! (1), ; (1)<br>Ubeti 5,(1), *(1) ;(1), | Hazikudumisha<br>Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa |
| 2.***The woman with whom I share my husband*** | 2.**Mwanamke Ninayeshirikiana Naye Mume** | |
| **Aina**: Huru<br>**Muundo**:Ruwaza sahili | **Aina**: Huru<br>**Muundo**: Ruwaza sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 1: 4<br>Ubeti 2:10<br>Ubeti 3: 6 | Ubeti 1: 4<br>Ubeti 2: 10<br>Ubeti 3: 5 | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa<br>Haikudumishwa |
| **Uakifishaji:** | | |
| Ubeti 1: . (2) ,(1) | Ubeti 1: .(1) , (2) | Hazikudumishwa |

| | | |
|---|---|---|
| Ubeti:2 . (1) , (1) ! (1) | Ubeti 2:,(1), .(3) | Hazikudumishwa |
| ***3.I do not know the dances of the white people*** | **3.Sizijui ngoma za wazungu** | |
| **Aina**: Huru<br>**Ruwaza**: Sahili | **Aina**: Huru<br>**Ruwaza**: Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo** | | |
| Ubeti 8:Mishororo 5<br>Ubeti 9 Mishororo 12<br>Ubeti 10: Mishororo 9 | Ubeti 8: Mishororo 3<br>Ubeti 9: Mishororo 9<br>Ubeti 10: Mishororo 6 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa<br>Haikudumishwa |
| **Alamazauakifishaji**: | | |
| Ubeti 8: .(1)<br>Ubeti 9: . (2) ;(1)<br>Ubeti 10: .(1) , (3) | Ubeti 8: . (1) , (2)<br>Ubeti 9: .(1) ,(6)<br>Ubeti 10: .(1) , (3) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumisshwa<br>Hazikudumishwa |
| ***4.My name blew like a horn among the Payira*** | **4. Jina langu lilivuma kama parapanda miongoni mwa watu wa payira** | |
| Aina: Huru<br>Ruwaza: Sahili | Aina: Huru<br>Ruwaza: Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 3: Mishororo 9<br>Ubeti 4: Mishororo 8<br>Ubeti 5: Mishororo 6 | Ubeti 3: Mishororo 7<br>Ubeti 4: Mishororo 4<br>Ubeti 5: Mishororo 6 | Haikudumishwa<br>Haikudumisshwa<br>Ilidumishwa |
| **Alama za uakifishaji** | | |
| Ubeti 3: , (2), . (1)<br>Ubeti 4: . (1) ,(3) : (1)<br>Ubeti 5: . (2) ,(1) | Ubeti3: , (2), . (2),<br>Ubeti 4: . (2) , (2)<br>Ubeti 5: .(1) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa |
| 5.***The graceful giraffe cannot become a monkey*** | 5.**Hawezi twiga kugeuka kuwa nyani** | |

| | | |
|---|---|---|
| **Aina**: Huru<br>**Ruwaza**: Sahili | **Aina :** Huru<br>**Ruwaza**: Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 1: 5<br>Ubeti 2: 5<br>Ubeti 3: 3 | Ubeti 1: 5<br>Ubeti 2: 4<br>Ubeti 3 : 3 | Ilidumishwa<br>Haikudumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Alama za uakifishaji**: | | |
| Ubeti 1: . (2)<br>Ubeti 2: , (1), .(1)<br>Ubeti 3: . (1) | Ubeti 1: . (2)<br>Ubeti 2: , (1), .(1)<br>Ubeti 3: . (1) . (1) | zilidumishwa<br>zilidumishwa<br>Hazikudumishwa |
| ***6.The mother stone has a hollow stomach*** | **6.Jiwe-mama lina shimo tumboni** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 2:12<br>Ubeti 5:7<br>Ubeti 8:8 | Ubeti 2:11<br>Ubeti 5:8<br>Ubeti 8: 6 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa<br>Haikudumishwa |
| **Alamaza uakifishaji**: | | |
| Ubeti 2: . (1) , (2)<br>Ubeti 5: , (2) ? (1) !(1)<br>Ubeti 8: . (2) * (1) , (1) | Ubeti 2: . (1) ; (1)<br>Ubeti 5: ; (1), ? (1), ! (1)<br>Ubeti 8: . (2) * (1) .(1) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa<br>Zilidumishwa |
| ***7.There is no fixed time for breast feeding*** | **7. Hakuna saa maalum za kunyonyesha mtoto** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 2:10 | Ubeti2:8 | Haikudumishwa |

| | | |
|---|---|---|
| Ubeti 3:4<br>Ubeti 4:7 | Ubeti 3: 7<br>Ubeti 4: 4 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa |
| **Alama za uakifishaji**<br>: | | |
| Ubeti 2: ,(1), ; (1), :<br>(2) ? (1)<br>Ubeti 3: . (1), !(1)<br>Ubeti 4:! (4) | Ubeti 2: ,(1), ; (1), : (1) ?<br>(1)<br>Ubeti 3: . (2) ;(1)<br>Ubeti 4: , (1), . (1) | Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa |
| **8.** ***I am ignorant of the good word in the clean book*** | **8. Silijui neno jema lililomo katika kitabu kitakatifu** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 2: 6<br>Ubeti 16: 8<br>Ubeti 19: 6 | Ubeti 2: 6<br>Ubeti 16: 8<br>Ubeti 19: 6 | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Alama za kuakifisha** | | |
| Ubeti 2: , (2), ! (1)<br><br>Ubeti 16: , (1) * (1) . (1)<br><br>Ubeti 19: . (1) . (1) | Ubeti 2: , (2), . (1)<br><br>Ubeti 16: , (2) : (1) . (1)<br><br>Ubeti 19: . (1) | Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa |
| ***9.From the mouth of which river?*** | ***9.*****Toka mdomo wa mto gani?** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 15: 6<br>Ubeti 16: 9<br>Ubeti 17: 11 | Ubeti 15: 5<br>Ubeti 16: 8<br>Ubeti 17: 14 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa<br><br>Haikudumishwa |

| | | |
|---|---|---|
| **Alama za uakifishaji:** | | |
| Ubeti 15: , (2), :?(1)<br>Ubeti 16: , (1) ?(2)<br>Ubeti 17: ? (2) | Ubeti 15: , (3) ?(1)<br>Ubeti 16: , (1) ?(2)<br>Ubeti 17: ? (4) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa |
| ***10. The last safari to Pagak*** | **10. Safari ya mwisho kwenda Pagak** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo**: | | |
| Ubeti 70: 14<br>Ubeti 73:3<br>Ubeti 74: 10 | Ubeti 70: 12<br>Ubeti 73: 3<br>Ubeti 74: 11 | Haikudumishwa<br>ilidumishwa<br><br>Haikudumishwa |
| **Alama za uakifishaji:** | | |
| Ubeti 70: , (3), !(1),<br>Ubeti 73: !(1), . (2)<br>Ubeti 74: , ( 3), ! (1) .(1, | Ubeti 70: . (4), , (1)<br>Ubeti 73: , (1), ! (1)<br>Ubeti 74: , (2), .(4) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa |
| ***11.Buffaloes of poverty knock the people down*** | **11. Mbogo wa umaskini huwaangusha watu** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo:** | | |
| Ubeti 1:4<br>Ubeti 5: 5<br>Ubeti 4: 8 | Ubeti 1:4<br>Ubeti 5: 3<br>Ubeti 4: 6 | Ilidumishwa<br>Hazikudumishwa<br><br>Hazikudumishwa |
| **Alama za uakifishaji** | | |
| Ubeti 1: ;(1), , (1) | Ubeti 1: ;(1), , (1) | zilidumishwa |

| | | |
|---|---|---|
| Ubeti 4: !( 2), ?(1)<br>Ubeti 5: ! (1) | Ubeti 4: !( 3), ?(1)<br>Ubeti 5: ! (1) | Hazikudumishwa<br>zilidumishwa |
| ***12.My husband;s house is a dark forest of books*** | **12.Nyumba ya mume wangu ni msitu mkubwa wa vitabu** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo:** | | |
| Ubeti 6: 9<br>Ubeti 8:13<br>Ubeti 19: 10 | Ubeti 6: 8<br>Ubeti 8:15<br>Ubeti 19: 10 | Haikudumishwa<br>Haikudumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Alama za uakifishaji:** | | |
| Ubeti 6:,(2) .(1)<br>Ubeti 8: , (5) . (1); (1)<br>Ubeti 19 , (1) .(1) ! (1) | Ubeti 6:,(1) .(2)<br>Ubeti 8: , (2) , ;(1), .(1)<br>Ubeti 19: ! (1) .(1) | Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa<br>Zilidumishwa |
| ***13. Let them prepare the Malakwang' dish***<br>**Aina:** Huru | ***13.*****Hebuwakutengenezee chakula cha Malakwang'** | |
| **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | **Aina:** Huru<br>**Ruwaza:** Sahili | Ilidumishwa<br>Ilidumishwa |
| **Mishororo:** | | |
| Ubeti 2: 3<br>Ubeti 3:7<br>Ubeti 16: 10 | Ubeti 2: 3<br>Ubeti 3:8<br>Ubeti 16: 9 | Ilidumishwa<br>Haikudumishwa<br>Ilidumishwa |
| Ubeti 2: . (1)<br>Ubeti 3: , (2) !(1)<br>Ubeti 16 : (1) | Ubeti 2: . (1)<br>Ubeti 3: . (2) ,(1)!(1)<br>Ubeti 16 : .(2): (1) | Zilidumishwa<br>Hazikudumishwa<br>Hazikudumishwa |

**KIAMBATISHO 2: matini za Wimbo wa lawino**

**Kiambatisho A**

**My Husband's Tongue is Bitter**

1.*Husband, now you despise me*
*Now you treat me with spite*
*And say I have inherited the stupidity of my aunt,*
*Son of the chief,*
*Now you compare me,*
*With the rubbish in the rubbish pit*
*You say you no longer want me*
*Because I am the things left behind*
*In the deserted homestead*
*You insult me*
*You laugh at me*
*You say I do not know the letter A*
*Because I have not been to school*
*And I have not been baptized*

*2.You compare me with your little dog,*
*A puppy.*
*My friend, age-mate of my brother,*
*Take care,*
*Take care of you tongue,*
*Be careful what your lips say.*

*3.First take a deep look, brother,*
*You are now a man*
*You are not a dead fruit!*
*To behave like a child does*
*Not befit you!*

**Ulimi wa Mume Wangu Ni Mkali**

1.Mume wangu, Sasa unanidharau,
Sasa unanipuuza kabisa
Ukisema nimerithi upumbavu
Wa shangazi yangu.
Ewe mwana wa chifu,
Sasa unanilinganisha na
Takataka za jaani.
Unasema huna haja na mimi tena
Kwa sababu nafanana na ghasia
Zilizoachwa mahameni
Unanitukana: unanicheka
Unasema sijui kusoma hata alifu A
Kwa sababu sikuwahi kwenda shule
Wala sikubatizwa!

2.Unanilinganisha na kijibwa,
Kitoto cha mbwa.
Rafiki yangu, Rika la kaka yangu,
Angalia, jihadhari ulimi wako,
Angalia neno linalotoka mdomoni mwako.

3.Kwanza jifikirie sana, ndugu,
Sasa wewe ni mtu mzima;
Wewe si embe mbovu!
Kufanya vitendo kama mtoto mdogo
Si mahali pako.

*4.Listen Ocol you are the son of a Chief*
*Leave foolish behaviour to little Children,*
*It is not right that you should*
*Be laughed at in any song!*
*Songs about you should be songs of praise!*

4.Sikiliza Ocol,
Wewe ni mwana wa chifu,
Mambo ya kijinga waachie watoto wadogo;
Haifai tena wewe
Uje uimbwe ngomani!
Wewe unapoimbwa inafaa
Uimbwe nyimbo za sifa!

*5.Stop despising people*
*As if you were a little man,*
*Stop treating me like salt-less*
*ash**

5.Acha kudharau watu
Kama kijitu kipumbavu,
Acha kunifanyia visa
Kama makapi ya magadi*

*8. He says Iam rubbish,*
*He no longer wants me!*
*In cruel jokes, he laughs at me,*
*He says I am primitive*
*Because I cannot pay the guitar,*
*He says my eyes are dead*
*And I cannot read,*
*He says my ears arre blocked*
*And cannot hear a single foreign word,*
*That I cannot count the coins.*
*He says I am like sheep,*
*The fool.*

8.Anasema mimi ni takataka,
Hana haja name tena!
Kwa kejeli mbaya hunicheka,
Alisema mimi ni mshamba
Kwa sababu siwezi kupiga gita;
Kwa sababu siwezi kusoma,
Asema masikio yangu yameziba,
Siwezi kusikia hata neon moja
La lugha ya kigeni,
Wala siwezi kuhesabu fedha.
Asema mimi ni kama
kondoo mpumbavu.

*9.Ocol treats me*
*As if I am no longer a person,*
*He says I am silly*
*Like the ojuu insects that sit on the beer pot*

9. Ocol ananiona
Kama kwamba si mtu tena,
Anasema mimi ni mjinga kama duduvule
Juu ya mtungi wa pombe.

*11.My husband's tongue*

11.Ulimi wa mume wangu ni mchungu

*Is bitter like the roots of the*
*Lyonno lily,*
*It is hot like the penis of the bee,*
*Like the sting of the kalang!*
*Ocol's tongue is fierce like the*
*Arrow of the scorpion,*
*Deadly like the spear of the*
*Buffalo-hornet*
*It is ferocious*
*Like the poison of the barren woman*
*And corrosive like the juice of the gourd.*

Kama mizizi ya mchunga.
Unawasha kama mwiba wa nyuki:
Kama mwiba wa sungusungu.
Ulimi wa Ocol ni mkali
Kama mshale wa nge
Unaumiza kama mwiba
Wa nyigu mkubwa,
Unafoka kama sumu
Ya mwanamke tasa,
Na unachubua
Kama utomvu
Wa kibuyu kichanga.

*13.His eyes grow large,*
*Deep black eyes*
*Ocol's eyes resemble those of*
*The Nile pearch*

13.Macho yanamtoka, macho meusi sana;
Macho ya Ocol yanafanana na
Macho ya kitoga, samaki wa mtoni

**Kiambatisho B**

| ***The woman with whom I share my husband*** | **Mwanamke tunayeshirikiana Mume** |
|---|---|
| *1.Ocol rejects the old type.* | 1.Ocol hapendi wanawake wa kizamani |
| *He is in love with a modern woman,* | Anampenda mwanamke wa kisasa |
| *He is in love with a beautiful girl* | Anampenda msichana mzuri |
| *Who speaks English.* | Ajuaye kiingereza. |
| | |
| *2.But only recently* | 2.Lakini miaka michache iliyopita |
| *We would sit close together,* | Tulikuwa tukikaa pamoja |
| *Touching each other!* | Karibu- karibu, tukigusana |
| *Only recently I would pay* | Miaka michache tu iliyopita |
| *On my bow-harp* | Nilikuwa nikipiga zeze la kikwetu |
| *Singing praises to my beloved* | Nikiimba nyimbo za kumsifia mpenzi wangu. |
| *Only recently he promised* | Miaka michache tu iliyopita |
| *That he trusted me completely* | Alisema alinipenda kabisa |
| *I used to admire him speaking in English.* | Nami nilikuwa nikipenda Alivyokisema Kiingereza |
| | |
| *3.Ocol is no longer in love with* | 3.Sasa Ocol hampendi tena |
| *the old type,* | Mwananmke wa kizamani |
| *He is with a modern girl.* | Anampenda mwananmke wa kisasa |
| *The name of the beautiful one* | Jina lake msichana huyo mzuri |
| *Is Clementine.* | Ni Clementine |
| *Brother, when you see Clementine!* | Ndugu, Ukimwona huyo Clementine |
| *The beautiful one aspires* | Anayeitwa mzuri! |
| *To look like a white woman;* | Anavyotamani kujigeuza Mzungu; |
| *Her lips are red-hot* | Midomo yake myekundu |
| *Like glowing charcoal,* | Kama makaa ya moto unaowaka, |
| *She resembles the wild cat* | Ananfanana na kimbulu |
| *That has dipped its mouth in blood,* | Alivyochovya domo lake katika damu; |
| *Her mouth is like raw yaws* | Mdomo wake kama buba changa, |

| | |
|---|---|
| *It looks like an open ulcer,* | Kama kidonda kinachotoja damu |
| *Like the mouth of a field!* | Kama mdomo wa shetani! |
| *Tina dusts powder on her face* | Tina anajitia poda usoni, |
| *And it looks so pale;* | Uso unaonekana mweupe; |
| *She resembles the wizard* | Anafanana na mchawi |
| *Getting ready for the midnight dance* | Anayejitayarisha kwenda kuwanga. |
| | |
| *6.I do not like dusting myself* | 6.Mimi sipendi kujipaka poda; |
| *With powder:* | Hiyo inawafaa wenye ngozi nyekundu |
| *The thing is good on pink skin* | Maana ngozi yao tayari imepauka. |
| *Because it is already pale,* | Lakini mwanamke mweusi akijipaka poda |
| *But when a black woman has used it* | Anakuwa kama anaharisha damu. |
| *She looks as if she has dysentery;* | Tina anaonekana kama mgonjwa, |
| *Tina looks sickly* | Na mwendo wake wa unyonge. |
| *And she is slowly moving* | Anatia huruma! |
| *She is a piteous sight.* | |
| | |
| *8.And she believes* | 8.Naye anaamini |
| *That this is beautiful* | Kuwa huo ndio uzuri, |
| *Because it resembles the face of* | Kwa sababu anafanana |
| *A white woman!* | Na ngozi ya mwanamke wa Kizungu! |
| *Her body resembles* | Mwili wake unafanana na |
| *The ugly coat of the hyena;* | Ngozi mbaya ya fisi; |
| *Her neck and arms* | Shingo yake na mikono yakeIna ngozi nzuri ya kibinadamu! |
| *Have real human skins!* | Anakuwa kama mtu aliyepigwa na radi |
| *She looks as if she has been* | Au ameungua kama kongoni |
| *Struck* | Aliyesakwa kwa moto. |
| *By lightning;* | |
| *Or burnt like the kongoni* | |
| *In a fire hunt.* | |
| | |
| *9.And her lips look like bleeding* | 9.Na midomo yake kama inatoka damu |
| *Her hair is long* | Nywele zake ni ndefu |

| | |
|---|---|
| *Her head is huge like that of*<br>*the owl,*<br>*She looks like a witch*<br>*Like someone who has lost her*<br>*head*<br>*And should be taken*<br>*To the cline shrine*<br>*Her neck is rope – like,*<br>*Thin, long and skinny*<br>*And her face sickly pale.* | Kichwa chake kikubwa,kama cha bundi,<br>Anafanana na mchawi;<br>Kama mtu aliyepandwa kichaa,<br>Anayestahili kupelekwa tambikoni.<br>Shingo yake kama kamba,<br>Nyembamba,ndefu,mifupa mitupu,<br>Na uso wake mweupe kama mgonjwa |
| *10, Forgive me brother,*<br>*Do not think I am insulting*<br>*The woman with vhom I share my*<br>*My husband!*<br>*Do not think my tongue*<br>*Is being sharpened by jealousy.*<br>*It is the sight of Tina*<br>*That provokes sympathy from*<br>*My heart.* | 10.Samahani kaka,<br>Usifikiri natukana mwanamke<br>Ninayeshirikiana naye mume;<br>Ukadhani ulimi wangu umekuwa mkali<br>Shauri ya wivu.<br>Tina ameharibika, hapendezi machoni,<br>Ndiyo sababu moyo wangu unamhurumia. |
| *11.I do not deny*<br>*I am a little jealous.*<br>*It is no good lying,*<br>*We all suffer from a little jealousy,*<br>*It catches you unawares*<br>*Like the ghosts that bring fevers;*<br>*It surprises people*<br>*Like earth tremours:*<br>*But when you see the beautiful*<br>*woman*<br>*With whom I share my husband*<br>*You feel a little pitty for her24When I have* | 11.Wivu kidogo ninao,sikatai;<br>Hakuna sababu ya kudanganya;<br>Wote tunao wivu kidogo moyoni.<br>Wivu unakujia ghafla<br>Kama shetani aletavyo homa,<br>Unawashangaza binadamu<br>Kama tetemeko la nchi.<br>Lakini ukimwona<br>Mwanamke huyo, hawala ya mume wangu,<br>Hata wewe utamhurumia kidogo! |

*another woman*
*With whom I share my husband*

*15.She looks as if*
*She has been ill for a long time!*
*Actually she is starving*
*She does not eat*
*She says she fears getting fat,*
*That the doctor has prevented her*
*From eating,*
*She says a beautiful woman*
*Must be slim like a white*
*Woman;*
*And when she walks*
*You hear her bones rattling*
*Her waist resembles that of th Hornet*
*On a dry river bed.*

15.Ukimwona amekondeana kama mgonjwa
Aliyeugua maradhi ya siku nyingi.
Kwa kweli anakufa njaa,hali,
Kwa hofu ya kunenepa;
Daktari kumkataza kula,
Asema mwanamke mzuri
Sharti awe mwembamba
Kama memsahib wa kizungu.
Na anapotembea mwanamke huyo,
Unasikia mifupa yake inavyogongana,
Kiuno sawa na cha nyigu.
Mwanamke aliyekuwa mzuri
Kama kisiki hana hata nyama
Kama simbi katika mto uliokauka!

*24.I am glad*
*A woman who is jealous*
*Of another, with whom  she shares*
*man,*
*Is jealous because she is slow,*
*Lazy and shy,*
*Because she is col, weak,*
*clumsy!*

24. Nafurahi kuwa na mwanamke mwingine
Kushirikiana naye mume
Mwanamkeanayemwonea wivu mwenziwe
Anayechangia naye mwanamume
Yu goigoi,
Au mvivu, au amezidi haya;
Afahamu yeye mwenyewe hana joto,
Mnyonge wala hakuchangamka.

*25.I do not understand*
*The ways of the foreigners*
*But I do not despise their customs.*
*Why should you despise yours?*

25.Tabia za wageni mimi sielewi
Lakini hata hizo sipuuzi
Wewe vipi wapuuza mola zako?

*26.Listen my husband,*
*You are the son of a chief,*

26.Sikiliza, mume wangu,
Weweni mwana wa chifu.

| | |
|---|---|
| *The pumpkin in the old* | Mboga ulioota mahameni |
| *Homestead* | Usidiriki kuung’oa. |
| *Must not be uprooted!* | |
| | |
| *28..Listen Ocol, my old friend,* | 28.Sikiliza Ocol, rafiki yangu, |
| *The ways of your ancestors* | Maisha ya wahenga wetu ni mazuri, |
| *Are good,* | Tabia zao zina msingi imara, |
| *Their customs are solid* | Si shimo tupu kama mwanzi. |
| *And not hollow* | Mila zao si kitu duni |
| *They are not thin, not easily* | Kinachovunjika upesi; |
| *Breakable* | Haziwezi kupeperushwa ovyo |
| *They cannot be blown away* | Kwa upepo uvumao; |
| *By the winds Because their roots reach deep* | Mizizi yake ni mirefu |
| *Into the soil.* | Iliyoingia ndani arthini. |

**Kiambatisho C**

***I Do Not Know the***
***Dances of White People***

**Sizijui Ngoma za Wazungu**

*8.A girl whose waist is stiff*
*Is a clumsy girl*
*That is the lazy girl*
*Who fears greinding the kabir*
*Millet.*

8.Msichana mwenye kiuno kigumu
Msichana goigoi, mvivu,
Aogopaye kazi ya kusaga mtama.

*9.You adorn youself in Acoli*
*Costumes*
*You tie lacucuku rattles*
*Or bells on your legs.*
*You wear bead skirts or string*
*Skirts*
*Or a tiny piece of cloth*
*And a ten-stringed bead*
*Around your waist;*
*Bangles on your arms*
*And giraffe-tail necklaces on*
*Your tall neck.*

9.Unajivika mavazi ya ki-Acoli
Unafunga njuga au kengele miguuni,
Unavaa kipande kilichofumwa shanga tupu,
Au kitambaa cha kamba za kufuma,
Au kitambaa chochote kinachofaa,
Na shanga kumi umejifunga kiunoni,
Bangili mikononi,
Kamba ya usinga wa twiga
Umejifunga kwenye shingo yako ndefu.

*10.A young man wears the odye*
*and lacomi,*
*He puts his lover's beads*
*On his neck,*
*Beautiful white feathers on his*
*head,*
*He blows his horn*
*And other young men feel*
*Jealous of him.*

10.Mvulana anavaa *odye* na *lacomi,*
Shingoni anajivika ushanga wa mpenzi wake,
Manyoya meupe, mazuri, anayapamba kichwani,
Analipulza pembe lake mpaka
Vijana wenzake wanamwonea wivu.

*14.When the daughter of the Bull*
*Enters the arena*
*She does not stand here*
*Like stale beer that does not*
*Sell,*
*She jumps here*
*She jumps there.*
*When you touch her*
*She says 'Don't touch me!''*

14.Binti ya mtu anapoingia uwanjani
Hasimami kimya papo hapo
Kama pombe isiyo thamani.
Anaruka-ruka huko na huko
Na ukijaribu kumshika hataki,
Asema, "Usiniguse."

*17. They come to the dance deaddrunk*
*They drink white men's drinks*
*As well as waragi.*
*They close their eyes,*
*And they do not sing as they dance,*
*They dance silently like wizards*

17**.**Wanaocheza dansi huja wamelewa chopi
Wanakunywa pombe za kizungu
Pamoja na gongo;
Wakicheza wanafumba macho,
Na wala hawaimbi wakati wakicheza
Wanacheza kimya-kimya kama wachawi.

*19.Women throw their arms*
*Men hold the waists of the*
*Women*
*Arond the necks of their partners*
*And put their cheeks*
*On the cheeks of their men.*
*Tightly,tightly...*

19.Wanawake wanaitupa mikono yao
Shingoni mwa wale wanaocheza nao
Na kuweka mashavu yao
Juu ya mashavu ya wanaume zao.
Wanaume wanakamata viuno vya wanawake,
Na kuwakumbatia kwa shauku.

21.Modern girls are fierce
Like *Labeja*, the *jokofAlero**
That captures even the heads of
*Nephews,*
*They coil around their nephews*
*And lie on the chests of their*
*Uncles*

*21.Wasichana wa siku hizi ni wakali*
*Kama Labeja, shetani wa Alero**
*Wanaodiriki kushika vichwa vya wapya zao*
Na kulala vifuani mwa wajomba zao
Na kuchoma vifua vya kaka zao
Kwa matiti yao.

*And prick the chests of their*
*Uncles*
*And prick the chests of their brothers*
*With their breasts.*

*25.It is hot inside the house*
*It is hot like inside a cave*
*Like inside a hyena's den!*
*And the women move like fish*
*That have been poisoned,*
*They stagger*
*They fall upwards*
*Like fish that are dead drunk*
*With lugoro or ober;*
*Like small fish out of water.*

25.Kuna joto ndani ya nyumba
Joto kali kama ndani ya pango,
Kama ndani ya shimo la fisi.
Na wanawake wanatembea
Kama samaki waliolewa chopi
Sumu ya *lugoro* ama *ober*
Kama visamaki vilivyotolewa
Nje ya maji

*30.The stench from the latrine*
*Knocks you down, from afar!*
*You enter;*
*It is as if you have entered*
*Into a lion's mouth*
*The smell of jeyes*
*And the smell of dung*
*Rise to the roof*

30..Harufuinayotoka chooni ni kali;
Harufu ya chooni
Inakuangusha kwa mbali
Unaingia;
Kama kwamba umeingia
Kinywani mwa samba.
Harufu ya Jeye na harufu ya mavi
Inarukia paani.

*31.The entire floor*
*Is covered with human dung*
*All the tribrs of human dung!*
*Dry dungs and dysentery*
*Old dungs and fresh dungs*

31.Sakafu nzima imefunikwa na mavi,
Kabila zote za mavi ya mwanadamu!
Mavimakavu na bawasili,
Mavi makongwe na mapya,
Mavi yanayofuka joto,
Mafupi na manene,
Yaliyoketi kama vijilima,

Yenye mshabaha wa nyoka,
Yaliyojizongeresha kama chatu;
Vijimavi vidogo vilivyoketi,
Mimavi mikubwa iliyolala ubavu
Kama mashina ya mti.

*32.Young ones that are still*
*Steaming,*
*Short thick dungs*
*Sitting like hills,*
*Snake-like dungs*
*Coiled up like pythons.*
*Little ones just squatting there,*
*Big ones lying on their sides*
*Like tree trunks*

*35.I wish I could become*
*A meteorite*
*And I would know*
*Where to fall!*

35.Natamani ningegeuka kimondo
Hapo ningejua pa kuangukia!

**Kiambatisho D**

***My Name Blew***
***Like a Horn Among***
***The Payira***

**Jina langu lilivuma miongoni mwa watu wa Payira**

*1.I was made chief of the girls*
*Because I was lively,*
*I was bright,*
*I was not clumsy nor untidy*
*Iwas not dull.*
*I was not heavy and slow.*

1.Nikapewa hadhi ya kuwa
Kiongozi wa wasichana,
Kwa sababu nilikuwa
Mwenye akili nimechangamka.
Sikuwa lege-lege, au mchafu;
Sikuwa mpumbavu,
Sikuwa mzito au goi-goi

*3.When Ocol was woing me*
*My breasts were erect,*
*And they shook*
*As I walked briskly,*
*And as I walked*
*I threw my long neck*
*This way and that way*
*Like the flower of the lyonno lily*
*Waving in a gentle breeze.*

3.Wakati Ocol alipuokuwa ananiposa,
Matiti yangu yalikuwa yamesimama
Nikitembea kwa vishindo nayo yanatetema.
Shingo yangu ndefu nikiitupa
Huko na huko, yapendeza
Kama ua zuri la *lyonno*
Linalotikiswa na upepo.

*4.And my brothers called me*
*Nya-Dyang*
*For my breasts shook*
*And beckoned the cattle,*
*And they sang silently:*
*Father prepare the kraal,*
*Father prepare the kraal,*
*The cattle are coming.*

4.Na kaka zangu wakiniita
*Nya-Dang* kwa sababu
Maziwa yangu yalitetema
Kana kwamba yananong'ona:
*Baba ,tayarisha zizi,*
*Baba,tayarisha zizi,*
*Ng'ombe wanakuja.*

*5.I was the leader of the girls,*

5.Nilikuwa kiongozi wa wasichana

*And my name blew*
*Like a horn*
*Among the Payira.*
*And I played on my bowharp*
*And praised my love.*

Na jina langu likavuma
Kama parapanda
Miongoni mwa Payira.
Nami nilijua kupiga kizeze
Nikimsifia mpenzi wangu.

*6.Ocol, my husband,*
*My friend,*
*What are you talking?*
*You saw me when I was young.*
*In my mother's house*
*This man crawled on the floor!*
*The son of the Bull wept*
*For me with tears,*
*Like a hungry child*
*Whose mother has stayed long*
*In the simsim field.*

6.Ocol, mume wangu,
Rafiki yangu, unasema nini?
Uliniona nilipokuwa msichana
Katika nyumba ya mama yangu;
Mwanamume huyu alipiga magoyi chini!
Mwana wa dume alilia,
Akatokwa machozi kwa ajili yangu
Kama motto mwenye njaa
Mamaye yuko katika shamba la ufuta!

*8.You loved my giraffe-tail bangles,*
*My father bought them for me*
*From the hills in the east*.

8.Ulizipenda bangili zangu
Zilizosukwa kwa usinga wa twiga
Baba yangu alizoninunulia
Kutoka milima ya mashiriki

*9.The roof of my mother's house*
*Was beautifully laced*
*With elephant grass;*
*Mu father built it*
*With the skil of the Acoli*

9.Kipaa cha nyumba ya mama yangu
Kiliezekwa vizuri kwa manyasi;
Baba yangu aliijenga
Kwa ufundi wote wa ki-Acoli

*10.You admired my sister's*
*Colourful ten-stringed lion beads;*
*My mother threaded them*

10.Ulizipenda shanga za dada yangu
Mitungo kumi ya shanga nene-nene
Mama yangu alizozitunga

*And arranged them with care.*

Na kuzipanga kwa ufundi.

*13.My man,what are you talking?*
*My clansmen, I ask you:*
*What has become of my husband?*
*Is he suffering from boils?*
*Is it ripe now?*
*Should they open it*
*So that the pus may flow out?*

13.Mwanamume wangu, unasema nini?
Nawauliza wenzangu:
Mume wangu anasumbuliwa na nini?
Anaugua majipu?
Yamekwisha iva?
Yapasuliwe ili usaha utoke?

*14.I sang sweetly*
*When I was grinding millet*
*Or on the way to the well*
*Nobody's voice was sweeter*
*Than mine!*
*And in the arena*
*I sang solos*
*Loud and clear*
*Like the ogilo bird*
*At sunset.*

14.Nilikuwa kiongozi wa vijana
Kwa sababu ya adabu yangu,
Kwa sababu kiuno change kilikuwa laini
Nilijua kuimba vizuri.
Nikisaga mtama ama nikienda kisimani,
Hakukuwa na sauti ya mwanamke
Iliyokuwa tamu kama yangu
Na uwanjani, ngomani,
Niliimba nyimbo kwa sauti
Kali na tamu, kama ya ndege;
Sauti ya terere
Wakati wa machweo ya jua.

*15What is all this?*
*My husband refuses*
*To listen to me,*
*He refuses to give me a chance.*

15Upuuzi gani huo?
Mume wangu anakataa kunisikiliza,
Anakataa kunipa nafasi

*16.He has put a road block*
*But has not told me why*
*He just shouts*
*Like houseflies*
*Settling on top of excrement*

16.Akikasirika anabwata tu,
Kama kundi la nzi
Lililokurupushwa juu ya kinyesi.
Mume wangu amenifungia mlango kabisa

*When disturbed!*
*My husband has blocked up my path completely.*

*18.Like beggers*
*You take up white men's adornments,*
*Like slaves or war captives*
*You take up whie men's ways*
*Didn't the Acoli have adornments?*
*Didn't black people have their ways?*

18.Kama maskini wanaoomba barabarani
Umeiga mavazi ya wazungu;
Kama watumwa
Au mateka wa kivita.

*21And you cannot sing one song*
*You cannot sing a solo*
*In the arena.*
*You cannot beat rythm on the half-gourd*
*Or shake the rattle- gourd*
*To the rythm of the orak dance!*
*And there is not a single bwola song*
*That you can dance.*

21Wala huwezi kuimba hata wimbo mmoja
Huwezi kuanza wimbo ngomani,
Huwezi kupiga-piga kibuyu ngomani,
Huwezi hata kupiga manyanga
Kufuatisha mapigo ya ngoma ya orak
Wala hakuna hata wimbo mmoja wa *bwola*
Ambao ukiimba unaweza kucheza.

*20.Like drunken men*
*You stagger to white men's*
*Games,*
*You stagger to white men's*
*Amusements.*
*Is Lawala* not a game?*
*Is cooro* not a game?s*
*Didn't your people have Amusements?*

20.Kama walevi, mwapepesuka
Mkienda kucheza michezo ya kizungu.
Mnajidai kushika ala za kigeni,
Mwawayawaya, wazungu wakiwacheka!
Lawala* si mchezo?
Wazee wetu hawakuwa na michezo yao?

**Kiambatisho E**

***The graceful giraffe cannot Become***
***A monkey***

*1.My husband tells me*
*I have no ideas*
*Of modern beauty.*
*He says I have stuck*
*To old fashioned hair styles.*

*2.He says*
*I am stupid and very backward*
*That my hair styles*
*Makes him sick*
*Because I am dirty.*

*3It is true*
*I cannot do my hair*
*As white women do.*

*4.Listen*
*My father comes from Payira,*
*My mother is a woman of Koc!*
*I am a true Acoli I am not a half-caste*
*I am not a slave girl.*

*6.You once saw me,*
*You saw my hairstyle*
*And you admired it,*
*And the boys loved it.*
*At the arena*
*Boys surrounded me*
*And fought for me.*

**Hawezi twiga**
**kugeuka kuwa nyani**

1.Mume wangu ananiambia
Sina fununu
Ya uzuri wa kisasa
Asema nimekwama
Katika misukosuko ya nywele ya kizamani

2.Anasema mimi ni mpumbavu
Na niko nyuma sana,
Misuko yangu inamtapisha
Kwa sababu mimi ni mchafu.

3.Ni kweli
Siwezi kuchana nywele zangu
Kwa mitindo ya wanawake wa kizungu.

4.Sikiliza,
Baba yangu anatoka Payira,
Mama yangu mwnamke wa Koc!
Mimi si chotara, ni mu-Acoli halisi
Mimi sina damu ya kitumwa;

6.Uliponiona zamani
Uliniona na nywele zangu
Ukazipenda na vijana wakazipenda.
Uwanjani, ngomani
Vijana walinitafuta kwa hamu
Wakapigana kwa ajili yangu.

*14If you put on a black string-skirt*
*You do your hair with akuku*
*Glitter in the evening sun*
*And the healthy sweat*
*On your bosom*
*Is like yhe glassy fruits of Ocuga*

14Kama umevalia nguo nyeusi
Nywele zako unazipaka masizi
Au kikapu kipyaMwili unameta-meta kwa mafuta ya uto
Na chale za kifuani na shingoni
Zinang'ara kwa mionzi ya jua la jioni
Na jasho linatoka maziwani
Kwa sababu ya afya
Kama utomvu
Wa tunda tamu la *Ocuga*

*15.Young girls*
*Whose breasts are just emerging*
*Smear shea butter on their bodies*
*The beautiful oil from Labwor omor.*

15Vigori, maziwa yanapoanza kuota,
Wanajipaka samlimiilini mwao
Na mafuta ya mti, labwor-omor

*17.Butter from cow's milk*
*Or the fat from edible rats*
*Is cooked together with lakura*
*Or atika;*
*You smear it on your body today*
*And the aroma*
*Lasts until the next day.*

17.Siagi ya maziwa ya ng'ombe
Au mafuta ya panya, huchemshwa
Pamoja na miti yenye harufu
Lakura au atika
Unajipaka mwilini
Na kunukia kwake
Kutaendelea mpaka kesho yake.

*18.And when you balance on your head*
*A beautiful water pot*
*Or a new basket*
*Or a long-necked jar*
*Full of honey*
*Your long neck*
*Resembles the alwiri spear.*

18.Na ukiuweka vizuri kichwani mwako
Mtungi wa maji,
Mtungi wa maji au kikapu kipya,
Au kibuyu kirefu kilichojaa asali
Shingo yako ndefi inafanana
Na mkuki wa ainaa ya *alwiri*

*19.And as the fragrance*
*Of the ripe wild berrie*
*Hooks the insects and little birds,*

19.Kama harufu ya matunda ya porini, yaliyoiva
Yanapowavuta wadudu na ndege wadogo,

*As the fishermen hook the fish*
*And pull them up mercilessly.*

Kama mvuvi anavyomchoma samaki ndoana.
Akamtupa mchangani bila huruma

*21And when you balance your head*
*A beautiful water pot*
*Or a new basket*
*Or a long- necked jar Full of honey*
*Your long neck*
*Resembles the alwiri spear.*

21Na ukiuweka vizuri kichwani mwako
Mtungi wa maji au kikapu kipya
Au kibuyu kirefu kilichojaa asali
Shingo yako ndefu inafanana
Na mkuki wa aina y\a *alwiri*.

*22.And as you walk along the pathway*
*On both sides*
*The obiya grasses are flowering*
*And the pollok blossoms*
*And the wild white lilies*
*Are shouting silently*
*To the bees and butterflies.*

22. Na ukipita njiani
Huku na huku majani yanachanua
Na vichaka vinatoa maua.
Na maua ya porini yanapiga kelele
Polepole kukataza nyuki na vipepeo.

*24.And when you go*
*To the well*
*Or into the freshly burnt woodlands*
*To collect the red oceyu,*
*Or to cut oduggu shrubs,*
*You find them*
*Lurking in the shades*

24.Ukienda kisimani
Au katika nyika iliyochomwa moto
Kutafuta nyoga mwekundu
Au mboga ya *oduggu*.
Unawakuta, wanangoja kivulini,
Kama chui jike wenye watoto.

*14If you put on a black string-skirt*
*You do your hair with akuku*
*Glitter in the evening sun*
*And the healthy sweat*
*On your bosom*
*Is like yhe glassy fruits of Ocuga*

14Kama umevalia nguo nyeusi
Nywele zako unazipaka masizi
Au kikapu kipyaMwili unameta-meta kwa mafuta ya uto
Na chale za kifuani na shingoni
Zinang’ara kwa mionzi ya jua la jioni
Na jasho linatoka maziwani

Kwa sababu ya afya
Kama utomvu
Wa  tunda tamu la *Ocuga*

*15.Young girls*
*Whose breasts are just emerging*
*Smear shea butter on their bodies*
*The beautiful oil from Labwor omor.*

15Vigori, maziwa yanapoanza kuota,
Wanajipaka samlimiilini mwao
Na mafuta ya mti, labwor-omor

*17.Butter from cow's milk*
*Or the fat from edible rats*
*Is cooked together with lakura*
*Or atika;*
*You smear it on your body today*
*And the aroma*
*Lasts until the next day..*
*And when you balance on your head*
*A beautiful water pot*
*Or a new basket*
*Or a long-necked jar*
*Full of honey*
*Your long neck*
*Resembles the alwiri spear.*

17.Siagi ya maziwa ya ng'ombe
Au mafuta ya panya, huchemshwa
Pamoja na miti yenye harufu
Lakura au atika
Unajipaka mwilini
Na kunukia kwake
Kutaendelea mpaka kesho yake.
18.Na ukiuweka vizuri kichwani mwako
Mtungi wa maji,
Mtungi wa maji au kikapu kipya,
Au kibuyu kirefu kilichojaa asali
Shingo yako ndefi inafanana
Na mkuki wa ainaa ya *alwiri*

*19.And as the fragrance*
*Of the ripe wild berrie*
*Hooks the insects and little birds,*
*As the fishermen hook the fish*
*And pull them up mercilessly.*

19.Kama harufu ya matunda ya porini, yaliyoiva
Yanapowavuta wadudu na ndege wadogo,
Kama mvuvi anavyomchoma samaki ndoana.
Akamtupa mchangani bila huruma

*34.You twist another cross-like handle;*
*It is cold water,*
*Clean like the cooling fresh waters.*

34.Kuna maji mengi
Nyumbani mwa mume wangu
Maji baridi na maji moto

*From the sreams*
*Of Lututuru hills.*

*39. Ocol, my friend*
*Look at my skin*
*It is smooth and black*
*And my boy friend*
*Who plays the nanga*
*Sings praises to it*

Unazungusha kidude kama msalaba
Na maji yanatoka,
Ya moto, yanatoa mvuke
Kama mkojo wa tembo.
Unazungusha kidude kingine
Sasa ni maji baridi
Maji safi kama yale
Yanayotiririka kutoka milima ya lututuru.

39.Ocol, rafiki yangu,
Tazama ngozi yangu,
Ni nyeusi na laini
Na Yule rafiki yangu
Anayepiga zeze
Anaimba kusifia.

**Kiambatisho F**

***The Mother Stone***
***Has a Hollow Stomach***

**Jiwe- mama lina Shimo tumboni**

*2.He says*
*He is ashamed of me*
*Because when he opens*
*The tin of lobster*
*I feel terribly sick,*
*Or when he relates*
*How, when he was in the white*
*Men's country*
*They ate frogs and shells*
*And tortoises and snakes*
*My stomach rebels*
*And throws its contents out*
*Through my mouth.*

2.Anasema namtia aibu
Kwa sababuakifungua kopo
Lililojaa kamba- koche
Moyo unanichafuka;
Au anaposimulia
Jinsi wanavyokula vyura
Katika nchi za wazungu,
Na konokono, kasa na nyoka
Tumbo langu lachafuka
Na kutoa vyote nilivyokula,
Kupitia mdomoni.

*5.I cannot use the primus stove*
*I do not know*
*How to light it,*
*And when it gets blocked*
*How can I prick it?*
*The thing roars like a lion,*
*It frightens me!*

5.Siwezikupikia stova
Sijui hata kuliwasha
Na kama likiziba
Mimi nawezaje
Kulitia mwiba lizibuke?
Dubwana linanguruma
Kama samba ndume;
Linanitia kihoro!

*8.The electric fire kills people.*
*They say*
*It is lightning,*
*They say*
*The white man has trapped*
*And caught the Rain- cock**
*And imprisoned it*

8.Jiko la umeme huua watu,
Wanasema umeme ni radi.
Wanasema wazungu wametega
Na kumnasa *jogoowamvua**
Kumfungia katika nyumba
Ya chuma kigumu.

*In aheavy steel house.*

*12Whoever cooked standing up?*
*And the stove*
*Has many eyes.*
*I do not know*
*Which eye to prick*
*So that the stove*
*May vomit fire*
*And I cannot tell*
*Which eye to prick*
*So that fire is vomited*
*In one and not another plate*

12.Mwanamke gani apikaye wima?
Na jiko lenyewe lina macho mengi
Sijui nibonyeze jicho gani
Ili jiko litapike moto,
Na wala sijui nibonyeze jicho gani
Ili moto utke mahali hapa
Na siyo mahali pengine.

*18.They are for warming up*
*Tinned beef, tinned fish,*
*Tinned frogs, tinned snakes,*
*Tinned peas, tinned beans,*
*Tastlesslikethecooro!*

18.Yanafaa kupasha moto
Nyama ya makopo;
Samaki, vyura, nyoka,
Mbaazi, maharage au
Soya, yote makopo,
Hayana ladha kama *cooro!*

*29.On this stone*
*They also grind*
*Dried beans and  peas.*
*The sister stone,*
*The smaller one,*
*Cleaned and beautifully oiled*
*Like a girl*
*Ready for the jok dance,*
*Is the simsim grinding stone.*

29.Katika  jiwe hili
Wanasagia pia
Maharage na mbaazi kavu,
Jiwe lile linguine, dogo zaidi,
Safi na limepakwa mafuta,
Kama msichana aliyejiandaa
Kucheza ngoma ya *jok*
Ndilo la kusagia ufuta.

*34.Oywelo and lucoro and kituba*
*Are no use as firewood,*
*They burn like paper*

34.Miti ya *oywelo*, *lucoro*
Na *kituba* haifai kuwa kuni
Inaungua haraka, kama karatasi,

| | |
|---|---|
| *They are like pawpaw* | Ni kama mpapai; |
| *Heir fires are cold* | Moto wake ni baridi |
| *Like the firefly's fire.* | Kama moto wa kimeta. |

| | |
|---|---|
| *35.Labwori is alright* | 35.Mti wa labwori ni safi |
| *It is perfectly dry.* | Mradi ukauke sana. |
| *But if it is still green* | Lakini kama ni mbichi |
| *The smoke it produces* | Moshi unaotoa unachoma |
| *Is like a spear!* | Kama mkuki! |
| *It is useful for* | Hutumika kuwafukuza wanaume |
| *Chasing men from the hut* | Waondoke vibandani |
| *Men who sit too close* | Wanaume wanaoganda jikoni |
| *To the cooking place* | Macho yao kuangalia chungu! |
| *Their eyes fixed into the pot!* | *Odure** nani asiyesikiliza |
| *Odure* who does not* | Wengine waimbapo |
| *Listen when others sing* | *Toka*, Odure, |
| *Odure,comeout* | *Ondokajikoni*. |
| *Fromthekitchen* | *Motowa jikoni* |
| *Firefromthestove* | *Utaunguzauchiwako*! |
| *Willburnyourpenis*! | |

| | |
|---|---|
| *36.Opok is easy* | *36.Opok* ni mti rahisi |
| *To split with the axe;* | Kuchnja kwa shoka; |
| *Yaa burns gently* | *Yaa* ni mti unaowaka taratibu' |
| *It burns like oil;* | Unawaka kama mafuta |
| *Poi is no use for firewood* | *Poi* haufai kwa kuni |

| | |
|---|---|
| *51.But my bones are strong.* | 51.Lakini mifupa yangu ni imara |
| *I can dance all night long* | Naweza kucheza ngoma kucha. |
| *Listen to the song* | Sikiliza wimbo wanaoniimbia: |
| *They sang about me:* | |

*The beautiful one*
*Dances all night long*
*Alyeker prevents me sleeping.*
*I wait on the pathway*
*She refuses to come to me*
*The beautiful one*
*Dances  all night long*

*Yule msichana mzuri*
*Hucheza usiku kucha*
*Alyeker haniachi nikilala*
*Namgojea njiani*
*Anakataa kula kwangu.*
*Msichana mzuri*
*Acheza usiku kucha*

*52.What is the good thing in eggs?*
*Can it not be found*
*In other foods?*
*My husband,*
*I do not complain*
*That you eat*
*White men's food.*
*If you enjoy them*
*Go ahead!*
*Shall we just agree*
*To have freedom*
*To eat what one likes?*

52.Ni kitu gani kizuri katika mayai?
Hakiwezi patikana
Katika vyakula vingine?
Mume wangu
Silalamiki kwamba
Unakula vyakula vya kizungu.
Kama unavipenda, endelea kula!
Si ingefaa tukubaliane
Kuwa na uhuru
Mtu kula apendacho?

**Kiambatisho G**

***There is No fixed Time For Breast Feeding***

**Hakuna saa maalum za kunyonyesha mtoto**

*2.He asks me*
*How many days*
*There are in a year,*
*And how many weeks*
*In four moons;*
*But I cannot answer:*
*The number of moons*
*In nine weeks*
*Icannot say!*
*How can I tell?*

2.Aniuliza kuna siku ngapi
Katika mwaka mmoja,
Na katika miezi mine
Kuna majuma mangapi;
Lakini sina jibu.
Sijui idadi ya miezi
Katika majuma kenda:
Mimi sijui, nitajuaje?

*3.Ocol has brought home*
*A large clock*
*It goes tock-tock-tock!*
*And it rings a bell.*

3.Ocol ameleta saa kubwa
Inagonga ngo-ngo-ngo-ngo
Na kupiga kengele.
Kwanza anaitia ufunguo
Halafu inakwenda,
Ila mimi sijapata kuigusa
Naogopa kuitia ufunguo.

*4.He winds it first*
*And then it goes!*
*But I have never touched it*
*I am afraid of winding it!*
*I wonder what causes*
*The noise inside it!*
*And what makes it go!*

4.Kwanza anaitia ufunguo
Halafu inakwenda,
Ila mimi sijapata kuigusa
Naogopa kuitia ufunguo.

*7.My head gets puzzled,*
*Things look upside-down*

7Kichwa changu kinatatanika
Mambo yanaonekana juu-chini;

*As if I have been*
*Turning round and round*
*And I am dizzy.*

Naona kizunguzungu
Kama mtu aliyekizunguka.

*19.But if your daughter*
*Has no manners*
*If she is so loose*
*That men sleep with her*
*Even in the grass,*
*Then even if you are ill*
*You must go to the well*
*To draw water*
*And the nanga players*
*Will sing you a song:*
*The mother of the beautiful girl*
*Dies on the way to the well*
*As if she has no daughter*
*Her girl has no manners*
*What is to be done?*
*The mother of the girl*
*Dies on the grinding stone*
*In the bush to collect firewood!*

19.Lakini endapo binti yako
Si binti mwenye adabu,
Kama ni Malaya mno
Kulala na wanaume vichakani,
Basi hata ukiwa mgonjwa
Itakubidi uende kisimani
Kuteka maji,
Na wacheza ngoma
Watakuimbia wimbo:
*Mama wa binti mzur*
*Anakufa akienda kisimani*
*Kana kwamba hana motto*
*Afanyeje, binti hana adabu?*
*Mama wa binti mzuri*
*Anakufa akisaga mtama*
*Au nyikani, akitafuta kuni!*

20.*At the orak dance*
*A good girl*
*Whose mother is blind*
*Dances vigorously*
*And glances at the sun,*
*She returns home*
*Before sunset*
*A good daughter*
*Releases her mother*

20.Katika  ngoma hiyo
Binti mwema, ambaye
Mamaye ni kipofu,
Hucheza kwa juhudi
Huku akiangalia jua
Arejee nyumbani
Kabla ya magharibi.

*She sits around the evening fire*
*And tells folk tales*
*T o her younger ones*

*21.My husband says*
*I am useless*
*Because I waste time*
*He quarrels*
*Because, he says,*
*I am never punctual*
*He says*
*He has no time to wate.*
*He tells me*
*Time is money,*

21.Mume wangu anasema
Sina faida kwa sababu
Napoteza muda bure.
Anagomba kwa sababu
Anasema sifanyi kitu
Kwa wakati wake.
Anasema hana muda
Wa kupoteza bure.
Anasema muda ni fedha.

*28.At the lineage shrine*
*The prayers are for chid birth!*
*At the ogodo dance*
*The woman who struts*
*And dances proudly,*
*That is the mother of many,*
*That is the fortunate one;*
*And she dances*
*And looks at her own shadow.*

28.Katikambiko za makaburini
Dua zote ni za kuzaa watoto,
Na mwanamke aringaye ngomani,
Akicheza kwa kutamba
Huyo ni mwanamke mzazi
Wa watoto wengi.
Huyo ndiye mwenye bahati
Maana hucheza
Akitazama kivuli chake mwenyewe.

*33.Children in our homestead*
*Do not sleep at fixed times:*
*When sleep comes*
*Into their head*
*They sleep,*
*When sleep their head*
*They wake up.*

33.Katika nyumba zetu
Hakuna saa
Ya watoto kulala.
Watoto hulala tu
Usingizi ukiwajaa kichwani;
Na usingizi ukiwatoka kichwani
Wanaamka

*39.The Acoli did not*
*Set aside a special day*
*For Jok*
*Whem misfortune heats the*
*Homestead*
*The clansmen gather*
*And offer sacrifices*
*To the ancestors:*
*When the rains*
*Refuse to come*
*The Raincock* prepares a feast.*
*A goat is speared*
*In the wilderness*
*And the elders offer prayers*
*To jok.*

39.Wa-Acoli hawakujiwekea
Siku maalum ya Mungu.
Nyumba ikiingiliwa na mkosi
Ndugu hukusanyika
Na kutoa sadaka
Kwa mizimu, waliotangulia:
Mvua zikikataa kunyesha
Jogoo wa mvua*
Huandaa karamu.
Mbuzi hupigwa mkuki porini
Na waxee wanaomba dua
Kwa *jok*.

*41.Periodically each woman,*
*Sees the moon,*
*And when a young girl*
*Has seen it*
*For the first time*
*It is a sign*
*That the garden is ready*
*For sowing,*
*And when the gardener comes*
*Carrying two bags of live seeds*
*And a good strong hoe*
*The rich red soil*
*Swells with a new life*

41.Kila mwanamke
Anaona mwezi,
Katika kipindi chake,
Msichana anapouona mwezi
Kwa mara ya kwanza
Na dalili kwamba
Bustaani ni tayari
Kupandwa mbegu.
Na mkulima anapokuja
Na mifuko miwili ya mbegu
Jembe kubwa mkononi
Ardhi hiyo yenye rutuba
Mara hutuna
Kwa uhai mpya.

*44.During the Ager period*
*Millet is sown,*

44.Majira yaitwayo *Ager*
Kabla ya mvua kuanza,

*Just before the rains*
*And as they sow*
*They raise much dust*

Watu hupanda mtama,
Wakitimua mavumbi.

*45.When the rains return*
*We say*
*The rains have fallen*
*The period is called*
*Poto-kot*
*Then the millet seeds germinate.*

45.Wakati wakipanda
Mvua zinaporejea
Twasema mvuanzimeanguka
Majira hayo huitwa *Poto-kot*.
Halafu mtama unaota.

*47And hunger begins*
*To bite people's tummies,*
*This period*
*Is called Odunge*
*Because fierce hunger burns*
*People's insides*
*And they drink*
*Vegetable soups*
*To deaden the teeth*
*Of the fire.*

47.Na njaa inaanza
Kusumbua matumbo ya watu
Majira hayo huitwa *Odunge*,
Kwa sababu
Njaa kali huunguza
Matumbo ya watu;
Wanakunywa mchuzi wa mboga
Kupunguza ukali wa njaa.

*48.Whose garden have I spoiled?*
*So the period*
*Just before the harvest*
*Is called*
*Abalo-pa-nga?*

48.Nimeharibu shamba la nani?
Kwa hiyo majira yale
Kabla ya mavuno
Huitwa *Abalo-pa-nga?*

*51.You hear otole dance drums*
*And funeral songs,*
*You hear the horns and trumpets*
*And the moonlight dance songs*

51.Utasikia ngoma za otole
Na nyimbo za maziko;
Utasikia baragumu na zomari
Na nyimbo zikivuma angani,

*Floating in the air.*

Za ngoma zinazocheza usiku
Katika mbalamwezi.

*52.Youths in small groups*
*Go on the apet hunting*
*Expeditions.*

52.Vijana hufunga safari
Kwenda vikunfi-vikundi
Kuwinda swala

*54.Dry seasons means wooing*
*And eloping with girls.*
*It means the moko dance*
*When youths and girls*
*Get stuck to one another*

54.Wakati wa kiangazi
Ni wakati wa kuposa
Na kutorosha vigori.
Ni wakati inapochezwa
Ngoma iitwayo moko

Ambapo wavulana na wasichana
Wanang'ang'aniana,
Kila mmoja na mwenzake.

*56.I know that Okang*
*My first born*
*Was born at the beginning*
*Of the dry season*
*And my little girl*
*In the middle of the rains,*
*Okang was born*
*In the middle of the famine*
*Called Abongo-wang-dako*

56.Najua*Okang*, kifungua mimba,
Alizaliwa mwanzo wa kiangazi.
Na msichana wwangu mdogo
Katikati ya masika.
Okang alizaliwa
Katikati ya njaa
Inayoitwa *Abong-wang-dako*

**Kiambatisho H**

***I am Ignorant of the***
***Good Word in the Clean Book***

*1.My husband*
*Looks down upon me;*
*He says*
*I am a mere pagan,*
*I do not know*
*The way of God.*
*He says*
*I am ignorant*
*Of the good word*
*In the clean Book*
*And I do not have*
*A Christian name.*

*2.Ocol dislikes me*
*Because, he says,*
*Jok is in my head*
*And I like visiting*
*The diviner- priest*
*Like my mother!*

*4.Ocol laughs at me*
*Because I cannot*
*Cross myself properly*
*In the name of the father*
*And of the son*
*And of the Clean Ghost*

*And I do not understand*
*The confession,*
*And I fear*

**Silijui Neno jema lililomo**
**Katika Kitabu kitakatifu**

1.Mume wangu ananidharau;
Anasema mimi ni kafiri tu,
Sizijui njia za Mungu.
Anasema silijui Neno Jema
Lililomo katika
Kitabu Kitakatifu
Na wala sina
Jina la Kikristo.

2.Ocol hanipendi
Kwa sababu, anasema,
Nina shetani kichwani mwangu
Na tena napenda kwenda
Kwa mpiga ramli
Kama niendavyo kwa mama yangu.

4.Ocol ananicheka kwa sababu
Sijui kupiga alama ya Msalaba
Ipasavyo kifuani, kusema,
*Kwa jina la Baba*
*Na la mwana na*
*La Roho Mtakatifu*
Na sielewi maungamo
Tena namwogopa padre
Mwenye madevu marefu
Na tumbo kubwa

*The bushy-faced, fat bellied Padre*
*Before whom people kneel*
*When they pray.*

Apigiwaye magoti
Na watu waombao,
Wanapoomba.

*10.You work as if*
*You are a new eloped girl!*
*The wives of protestant*
*Church teachers and priests*
*Are a happy lot.*
*They sit with their legs*
*Stretched out*
*And bask in the morning son.*
*All they know*
*Is hatching a lot of children!*

10.Unamenyeka kama msichana
Aliyetoroshwa juzi-juzi!
Wake wa walimu
Na mapadre wa kiprotestanyi
Ni wanawake wenye raha.
Wanakaa, miguu wamenyoosha,
Na kuota jua la asubuhi;
Kazi wanayoijua
Ni kuzaa watoto wengi.

*11.My elder sister*
*Was christened Erina,*
*She was a protestant*
*But she suffered bitterly*
*In order to buy the name*
*And her loin beads*
*No longer fitted her!*

11. Dada yangu alibatizwa
Akaitwa Erina
Wa madhehebu ya kiprotestanti
Lakini alitaabika sana
Kulinunua jina hilo.
Mpaka ushanga wake wa kiunoni
Ukamwaya!

*16.I once joined*
*The catholic Evening Speakers'*
*Class*
*But I did not stay long*
*I ran away,*
*I ran away from shouting*
*Meaninglessly in the evenings*
*Like parrots*
*Like the crow birds*

*16.Siku moja nikaingia*
Katika Darasa la Jioni la Wakatoliki
Lakini sikukaa sana,
Nilikimbia,
Nilikimbia kwa sababu
Ya kupiga makelele ya bure
Jioni kama kasuku
Kama kelele za kunguru:

| | |
|---|---|
| | *MariaMtakatifu* |
| *MariatheCleanWoman* | *MamawaMungu* |
| *Mother of the Hunchback** | *Utuombee* |
| *Pray for us who spoil things* | *Sisiwakosefu* |
| *Full of graciya.* | *Uliyejaaneema*. |

| | |
|---|---|
| *19.Heshouted words at us* | 19.Akatusema kwa maneno makali |
| *And we shouted back at him,* | Nasi tukamrudishia |
| *Agitated and angry* | Tukiwa na hasira |
| *Like the okwik birds* | Kama ndege okwik |
| *Chasing away the kite* | Anayemfukuza kipanga |
| *From the nest* | Kutoka katika kiota chake. |

| | |
|---|---|
| *20.We repeated the meaningless* | 20.Tulirudia maneno yale yale |
| *Phrases* | Tusiyoyaelewa, |
| *Like the yelloew birds* | Kama ndege wa manjano |
| *In the  lajanawara grass.* | Katika manyasi marefu. |

| | |
|---|---|
| *23.The drums of the ‘get- stuck’ dance* | 23.Ngoma zikavuma kutoka mbali |
| *Thundered in the distance* | Za mchezo ule wa kung’ang’aniana |
| *And the songs came floating* | Na nyimbo zikasikika |
| *In the air.* | Zikipaa angani. |

| | |
|---|---|
| *27.The girls are dancing* | 27.Wasichana wanacheza |
| *Before their lovers* | Mbele ya wapenzi wao |
| *Shaking their waists* | Wakitikisa viuno |
| *To the rythm of the drums;* | Kufuatisha mlio wa ngoma, |
| *And I* | Na mimi nakaa |
| *Sitting like the stale bread* | Kama mkate usiotakiwa |
| *On the rubbish heap;* | Wenzangu wanafurahi |
| *My companions are gay* | Wanacheza, na kuimba |
| *They are dancing* | Nyimbo zenye maana, |
| *And singing meaningless songs,* | Huko ngomani |

*In the arena*
*They are singing my songs;*

Wanaimba wimbo wangu.

*50.Ocol wanted me*
*To be baptised 'Benedeta',*
*He has christened*
*One daughter 'Matra'.*
*The other took*
*The name of the mother of the*
*Hunchback!*

50.Ocol alitaka nibatizwe
Niitwe Beneta.
Amembatiza motto mmoja
Akamwita Marta
Mwingine akachukua jina
La mama wa Mungu!

*Maria the Clean woman*
*Mother of the Hunchback*

*Maria Mtakatifu*
*Mama wa Mungu*

*51.His first born son is Jekson**
*And the second he calls Paraciko**
*One of his illegitimate sons is*
*Tomcon**
*And the other one Guilyemo Iriko**

51.Mtoto wake wa kwanza
Anaitwa Jecson*
Na wa pili Paraciko
Mmoja wa watoto wake
Wa nje ya ndoa Tomcon
Na mwingine Gulyemo Iriko.

*55.But my husband's name*
*Is so difficult to pronounce;*
*It sounds something like*
*Medikijedki Gilirigoloyo**
*It sounds to me like*
*'Give the people more vegetables,*
*Foxes make holes in the pathway'*

55.Lakini jina la mume wangu
Ni gumu sana kuliita
Mimi nababaika kulitamka
Medikijedeki Gilirigoloyo
Utasikia kama mtu anasema
" Waongeze watu mboga
Mbweha wanachimba
Mashimo njiani."

*56.It sounds like a praise name*
*Uttered by a stammerer!*
*What is the meaning of 'Marta'?*
*Gulyemo, Iriko,Jeckon'*

56.Linasikika
kama jina la sifa
Linalotajwa na mtu
Mwenye kigugumizi.

*Are those names of ancestors?*

*61.Apiyo and Acen*
*Are Jok names*
*Twins are Joks*
*And are deeply respected.*
*Akelo is the one*
*Who comes after twins*
*Ajok and Ajara*
*Grow extra fingers or toes*
*Adoc comes out of the belly first.*

*63.Some names are names of sorrows*
*Alobo, Abur, Ayiko, Woko*
*That fate has thrown*
*A large basket*
*To be filled*
*With dead children*
*64.My father'sname*
*Is Otoo Lenga-moi*
*In the battle ion the hills*
*Ocol's grandfaher's tittle*
*Is Lutany-moi*
*With your spear*
*Or gun or sword*

'Marta' maana yake nini?
Au Gulyemo, Iriko, Jekcon
Haya ni majina ya babu zetu?
61.Apiyo na Acen
Ni majina ya mizimu
Na wanaheshimika sana.
Akelo ni yule anayezaliwa
Baada ya mapacha.
Ajok na Ajara ni wale
Wanaoota kidole cha sita
Miguuni au mikononi.
Adok ni yule anayezaliwa
Kutanguliza miguu.

63.Majina mengine
Ni majina ya huzuni:
Alobo, Abur, Ayiko, Woko,
Mkosi umeteremsha
Kapu kubwa
Lijazwe maiti ya watoto
64.Jina la baba yangu
Ni Otoo Lenga-moi
Alilipata jina hilo
Lenga-moi
Wakati wa vita vya milimani.
Jina la babu ya Ocol
Ni Lutany –moi:
Unakipata cheo hicho, moi,
Kwa mkuki wako
Au bunduki, au panga.

**Kiambatisho I**

***From the mouth of which river?***

*13. She dug the clay*
*From the mouth of the Oyitino River*
*The place was well known among potters.*

**Toka mdomo wa mto gani?**

13.Udongo aliuchimba
Kutoka mdomo wa mto Oyitino.
Mahali hapo palijulikana sana
Miongoni mwa wafinyanzi.

*15.When Skyland was not yet there*
*And earth was not yet moulded*
*Nor the stars*
*Nor the moon,*
*When there was nothing,*
*Where did the Hunchback live?*

15.Kabla mbingu haijakuwepo
Wala Nchi haijaumbwa,
Wala mwezi, wala nyota,
Kulipokuwa hakuna chpchpte,
Huyo Mungu aliishi wapi?

*16.Where did the Hunchback*
*Dig the clay for moulding things,*
*The clay for moulding Skyland*
*The clay for moulding Earth*
*The clay for moulding Moon*
*The clay for moulding the Stars?*
*Where is the spot*
*Where it was dug*
*On the mouth of which River?*

16.Mungu alichimba wapi udongo
Wa kutengenezea vitu:
Udongo wa kutengenezea mbingu
Udongo wa kutengenezea Nchi,
Udongo wa kutengenezea Mwezi,
Udongo wa kutengenezea Nyota?
Shimo liwapi udongo ulipochimbwa;
Katika mdomo wa mto gani?

*17.And when the hunchback*
*Was digging the clay*
*Where did he stand?*
*And when he brought home*
*The clay for moulding things*
*Where did he put the clay*
*To season overnight*
*And when he was beating it*
*With the wooden hammer*

17.Na wakati Mungu
Alipokuwa akiuchimba Udongo
Alisimamia wapi?
Na aliporudi nao nyumbani
Udongo wa kutengenezea vitu
Aliuweka wapi?
Na aliporudi nao nyumbani
Udongo wa kutengenezea vitu
Aliuweka wapi

*On which rock*
*Did the Hunchback put the clay?*

Kucha nzima upate kukomaa?
Na alipokuwa akiupiga-piga
Kwa nyundo ya mti
Katika mwamba gani
Mungu aliuweka udongo?

**Kiambatishu J**

***The last safari to Pagak****

*27**.**Andwhen it is Jok Omara*
*That has caused madness,*
*Or O dude or Ayweya*
*That has brought troubles,*
*When jok Rubanga**
*Has broken someone’s back*
*Or jok Odude*
*Has tied up a woman’s womb,*
*And the husband*
*Cries over his lost bridewealth,*
*Saying*
*What is marriage without child birth?*

*36.The roots of bomo*
*For stomach aches*
*It klls poisons*
*As well as worms.*

*40.Fresh wounds are treated*
*With ogali or pobo.*
*The sticky juices*
*Gum up the broken skins*
*And the bitter poison*
*Keeps the houseflies at bay.*

*43.When fevers trouble my child*
*Frequently,*
*When all the diseases*
*Have fallen in love with him,*
*And all youthful diseases*
*Run after him*

**Safari ya mwisho kwenda Pagak***

**27.** Na kama ni Omara
Ndiye aliyeleta kichaa,
Au Odude au Anyweya
Ndiye aliyeleta maafa,
Kama shetani Rubanga*
Amevunja mgongo wa mtu
Au shetani Odude
Amefunga kizazi cha mwanamke,
Na mumewe anasikitikia
Mahari aliyopoteza bure,
Akisema, ya nini ndoa
Bila ya uzazi?

36.Mizizi ya bomo
Dawa ya tumbo inayogangua sumu
Na minyoo vilevile.

40.Majeraha hutibiwa
Kwa ogali au pobo;
Ulimbo wake hufunga kabisa
Majeraha katika ngozi.
Na sumu yake kali
Inamfukuza nzi, hatui hapo.

43.Mwanangu akisumbuka
Kuumwa homa mara kwa mara
Magonjwa yote yakimpendautotoni
Kumwandama yeye tu
Mithili ya msichana mzuri,
Akapata kukohoa na kuhara damu,

*As if he was a beautiful girl*
*So that he has coughs and dysentery*
*And throught trouble and eye sickness,*
*And his ears have pus*
*And his legs have ulcers*
*And he is bony, skinny*
*And his loin-string is loose,*
*I know that someone is behind it.*
*I know somwone has hidden*
*The child's excreta in a tree fork,*
*Or has buried his hair or nail paring*
*In a river-bed*
*I know that some jealous woman*
*Perhaps even a close relative*
*Has visited the shadow trapper*
*Who has captured the child's shadow?*

Magogole na magonjwa ya macho,
Masikio yake  yavuja usaha
Na miguu yake ina vidonda
Naye dhaifu, kakondeana,
Kamba yake ya kiunoni
Imeanza kumlegea,
Najua kwamba hayo si bure.
Najua yuko mtu anayeyatenda hayo
Yuko mtu aliyeficha choo cha mtoto
Katika panda la mti
Au amezika nywele zake,
Au kucha zake,
Kandoni mwa mto.
Najua kuna mwanamke
Mwenye kijicho,
Pengine hata ndugu yangu,
Amekwenda kwa mganga
Wa kushika vivuli
Akakichukua kivuli
Cha mtoto wangu

*44.When your child is weak and listless,*
*When his energy fails him,*
*When he withdraws from the fight*
*For life, and gives up quickly,*
*It means his head has been captured*
*An he is only a crawling corpse*

44.Mwanao akiwa mnyonge
Mwili umetepetea, nguvu hana;
Anapokata tama upesi,
Maana yake kichwa chake
Kimekwisha shikwa,
Mwili wake ni mzoga unaotembea.

*54.All misfortunes have a root,*
*The snake bite, the spear of the enemy,*
*Lightning and the blunt buffalo horn,*
*These are the bitter fruits*

54.Mikosi yote ina sababu
Kuumwa na nyoka,
Mkuki wa maadui, radi,
Na pembe la mbogo;

*Grown on the tree of fate*
*They do not fall anyhow,*
*They do not fall at random*
*They do not come our way by accident*

Haya ni matunda ya uchungu
Yanayoota juu ya mti
Unaoitwa Kudura.
Hayadondoki ovyo ovyo
Wala hayaanguki tu.
Hayatufikii kwa bahati mbaya,
Hatujistukii tumetumbukia tu.

*58.You suckled those wrinkled breasts*
*And that's what made you*
*The big man you are!*
*And even if your father is totally blind,*
*Even if his ears are dead,*
*Even if the world has boxed him*
*Even if his legs are dry like firewood*
*If he is rude to you,*
*You say, 'Thank you'*

58.Hata kama baba yako ni kipofu kabisa,
Hata kama masikio yake yameziba,
Hata kama amefungiwa na dunia nzima,
Hata kama miguu yake
Imekauka kama kuni,
Akikukemea kwa jeuri
Unasema, asante.

*67.When the rains fail*
*And famine threatens a fierce invasion*
*Fiercer than the spear of lango,*
*If the crops are moved down by okwil*
*Or the hail stones have rained*
*And ruined all the millet*

67. Mvua zisiponyesha
Na njaa ikitishia kuingia
Kwa ukali kuliko mkuki wa Lango,
Kama mazao yakichukuliwa na Okwil
Au kama mvua yam awe
Imeharibu mazao yote ya mtama

*70.When Death comes*
*To fetch you*
*She comes unannounced,*
*She comes suddenly*
*Like the vomit of dogs,*
*And when she comes*
*The wind keeps on blowing*
*The birds go on singing*

70.Kifo kinapofika, kukuchukua,
Huja bila taarifa.
Huja ghafla
Kama matapishi ya mbwa.
Na kinapokuja
Upepo unaendelea kuvuma
Na ndege wanaendelea kulia
Na wala maua hayajinamii.

*And the flowers*
*Do not hang their heads*
*The agoga bird is silent*
*The agoga comes afterwards,*
*He sings to tell*
*That death has been that way!*

Kwanza bundi hunyamaza
Halafu bundi hujitikeza
Analia taarifa ya Kifo
Aliyepita upande ule.,

*73.Mother Death*
*She  says to her little ones*
*Come!*

73.Mama kifo huwaita
Watoto wake wadogo,
Njoo!

*74.Her little children are good children*
*Obedient,*
*Loyal,*
*And when Mother Death calls*
*And offers simsim paste*
*Mixed with honey!*
*She says*
*My only child*
*Come,*
*Come, let us go.*

74.Watoto wake wadogo
Ni watoto wema
Watii, waaminifu.
Na mama kifo anapoita
Watoto wake wadogo huinuka,
Huruka kwa furaha.
Maana huwaita
Akawapa mbwimbwi la ufuta
Lililochnganywa na asali.
Huita, mwanangu wa pekee,
Njoo, njoo twende.

*76.White diviner priests,*
*Acoli herbalists,*
*All medicine men and medicine*
*Women,*
*Are good, are brilliant*
*When the day has not yet*
*Dawned*
*For the great journey*
*The last safari*
*To Pagak.*

76.Mapadre wa kizungu,
Wachawi wa ki-Acoli,
Waganga wote
Wa kike na wa kiume
Ni waganga wema, mahodari
Kama siku haijapambazuka
Ya kuanza safari ile kuu,
Safari ya mwisho
Kwenda Pagak.

**Kiambatisho K**

***Buffaloes of Poverty***

***Knock the People Down***

*1.With the coming*
*Of the new political parties,*
*My husband reams the country side*
*Like a wild goat;*
*He is up before dawn:*
*You think*
*He is going to hoe*
*The new cotton field*
*Or to sow the millet*
*Or to harvest the simsim*
*All day long*
*He is away,*
*He does not eat at home*
*As if I do not cook!*

*2..When he comes*
*He does not stay a moment,*
*He says*
*There is another meeting*
*At the homestead of the Hoe chief.*
*He is away all night,*
*And when he returns so late*
*He says*
*Their car got stuck*
*In the mud.*

*4.He says*
*They are fighting for uhuru*
*He says*
*They want independence and peace*

**Mbogowaumaskin**

**Huwaangushawatu**

1.Tangu kuja
Vyama vipya vya siasa,
Mume wangu Anatanga-tanga nchini
Kama mbuzi wa porini;
Huamka alfajiri:
Utadhani anakwenda lima
Shamba jipya la pamba,
Au kupanda mtama
Au kuvuna ufuta.
Kutwa nzima hayupo,
Hali chakula nyumbani
Kana kwamba mimi sipiki!

2, Na akirudi wala hakai,
Anasema kuna mkutano
Nyumbani kwa chifu wa jembe.
Anakaanhuko kucha nzima,
Na akirudi, amechelewa sana
Anaema gari lao
Lilinasa matopeni.

4.Anasema wanapigania Uhuru
Anasema wanataka Uhuru na Amani!
Na waaakikutana wanapiga makelele
Wakisema ‘Uhuru! Uhuru!’

*And when they meet*
*They shout 'Uhuru! Uhuru!'*
*But what is the meaning*
*Of Uhuru?*

Lakini Uhuru
Maana yake ni nini?

*5.He says*
*They want to unite the Acoli*
*And Lang'o*
*And the Madi and Lugbara*
*Should live together in peace!*

5.Anasema anataka kuwaunganisha Acoli na Lang'o
na Madi na Lugbara
Waishi wote pamoja kwa amani!

*6.He says*
*White men must return*
*To their own homes,*
*Because they have brought*
*Slave conditions in the country.*
*He says*
*White people tell lies,*
*That they are good*
*At telling lies,*
*Like men wooing women,*

6.Anasema lazima wazungu
Warudi nyumbani kwao,
Kwa sababu wameleta
Hali ya utumwa nchini humu
Anasema wazungu wanadanganya,
Wanaposema wao ni watu wema;
Wanadanganya kama wanaume
Wanavyotongoza wanawake

*Ocol says*
*They reject the famine relief*
*Granaries*
*And the forced labour system.*

Ocol anasema wanakataa
Msaada wa kutengenezea maghala
Ya chakula cha njaa,
Wanakataa mpango wa manamba.

*9.His brother wears a red and black robe,*
*He looks like the judge*
*Who condemns people to death*
*He looks like the male aribe bird*
*And shouts like the train.*
*He walks majestically*

9.Kakaye naye anavaa joho
Rangi ya nyekundu na nyeusi
Ukimwona tadhani jaji
Anayewahukumu watu kunyongwa.
Anafanana na ndege
Anayeitwa aribe,
Na kupiga makelele

*Like a bull elephant*

Kama gari-moshi;
Anatembea kwa maringo
Kama dume la tembo.

*10.My husbsnd is the leader*
*Of the Democratic Party.*
*When they greet each other*
*They shake their fists*

10.Mume wangu ni kiongozi wa chama
Kinachoitwa Democratic Party.
Wanaposalimiana wanatikisa ngumi.
Kakaye yumo katika chama
Kinachoitwa Uganda's Peoples' Congress.
Alama yao ni kiganja cha mkono.

*11.Ocol does not enter*
*His brother's house .*
*You would think*
*There was homicide between them*
*That has not been settled,*
*You would think*
*That the oput-drinking*
*Peace making ceremony*
*Has not yet taken place*
*And they fear the deadly ojebu taboo!*

11.Ocol haingii
Nyumbani mwa kaka yake.
Utadhani wamepasuana uchawi
Na kuna ugomvi ambao haujamalizika;
Utadhani tambiko za pombe
Za kuleta suluhisho hazijafanyika,
Na wanaogopa miiko ya *ojebu*!

*12. Ocol dislikes his brother fiercly,*
*His mother's son hatred*
*Resembles boiling oil!*
*The new parties have split the homestead*

12.Ocol anamchukia sana nduguye,
Chuki hiyo ya mtoto wa mamaye
Ni kama mafuta yanayochemka!
Vyama hivyo vipya
Vimegawa ndugu na nyumba

*13.Ocol does not enter*
*His brother's house.*
*You would think*
*There was homicide between them.*
*That has not been settled,*
*You would think*

13.Ocol haingii
Nyumbani mwa kaka yake.
Utadhani wamepasuana uchawi
Na kuna ugomvi ambao haujamalizika;
Utadhani tambiko za pombe
Za kuleta suluhisho hazijafanyika,

*That the*
*oput-drinking*
*Peacemaking ceremony*
*Has not yet taken place*
*And they fear the deadly ojebu taboo!*

Na wanaogopa miiko ya *ojebu*!

*31.And you eat green vegetables*
*Without the simsim paste*
*And your thin children*
*Collect the odir and ocenne*
*And eat them*
*And the children of others are fat,*
*And their wives grow larger buttocks,*
*They eat meat from the chest of bulls*
*And the skin of their legs*
*Shines with health!*

31.Na wewe unakula mboga
Zisizokuwa na mafuta
Na watoto wako, walikonda,
Wanakusanya wadudu
Wanawakaanga na kuwala.
Na watoto wengine wamenenepa
Na wake
zao wamejaza matako makubwa
Wanakula nyama ya kidari
Cha ng'ombe dume
Na ngozi ya miguu yao
Inametemeta kwa afya!

*45.And while those inside*
*Eat thick honey*
*And ghee and butter,*
*Those in the countryside*
*Die with the smell,*
*They re-eat the bones*
*That were thrown away*
*For the dogs.*

45.Na wakati walio ndani ya chama
Wanakula asali nzito
Na samli na siagi,
Wale walio vijijini
Wanakufa kwa harufu;
Wanafyonza mifupa
Iliyokwisha tupiwa mbwa.

*49.They return*
*To the countryside*
*For the next elections*
*Like the kite*
*That returns during the dry season.*

49. Wanarudi vijijini
Kwa uchaguzi unaofuata
Kama kipanga anavyorudi
Wakati wa kiangazi.

*61.Iam concerned*
*About the well being of our homestead!*
*The women there*
*Wear mourning clothes*
*The home stead is surely dead*
*The enemnity , the black heartedness,*
*The quarrels, the jealousies...*

61.Nina wasiwasi juu ya
Hali ya nyumba yetu.
Wanawake wa pale
Wanavaa nguo za msiba
Kwa kweli nyumba haina uhai
Uadui, husuda
Magomvi, kijicho...

*62.When the fiends*
*That sow smallpox*
*Go through our homestead*
*That people will be finished,*
*Because the insides of the*
*People are bad!*
*This will be the gift*
*That the political parties have*
*Brought!*

62.Basi shetani anayepanda ndui
Atakapopata nyumbani kwetu
Watu wote watamalizika
Kwa sababu mioyo ya watu
Ni mibaya!
Hiyo itakuwa ndiyo zawadi
Iliyoletwa na vyama vya siasa!

**Kiambatisho L**

***My Husband's House***
***is a Dark Forest of Books***

*1.Listen my clansmen,*
*I cry over my husband*
*Whose head is lost.*
*Ocol has lost his head*
*In the forest of books.*

*2.When my husband,*
*Was still wooing me*
*His eyes were still alive*
*His ears were still unblocked,*
*Ocol had not yet become a fool*
*My friend was a man then!*

*5.He abuses all things Acoli,*
*He says*
*The  ways of black people*
*Are black*
*Beacause his eye balls have exploded,*
*And he wears dark glasses,*
*My husband's house*
*Is a dark forest of books.*
*Some stand there*
*Tall and huge*
*Like the tido tree.*

*6.The backs of some books*
*Are hard like the rocky stem of*
*The poi tree,*
*Some are green*
*Others red as blood*

**Nyumba ya Mume wangu**
**Ni Msitu mkubwa Wa Vitabu**

1.Sikilizeni, ndugu zangu,
Namlilia mume wangu
Ambaye akili yake imepotea.
Ocol amepoteza akili yake
Katika msitu wa vitabu.

2.Wakati mume wangu
Alipokuwa akiniposa
Macho yake yalikuwa bado hai,
Masikio yake yalikuwa hayajazibika;
Hajawa mpumbavu Ocol wakati huo,
Rafiki yangu alikuwa mwanamume!

5.Nyumba ya mume wangu
Ni msitu mkubwa wa vitabu,
Vingine vimesimama wima
Virefu na vinene
Kama mbuyu.

6.Magamba ya vitabu vingine
Ni magumu Kama shina
la mti;
Mengine ni rangi ya kijani
Mengine mekundu kama damu.

*Some books are black and oily,*
*Their backs shine like*
*The dangerous ororo snake*
*Coiled on a tree top.*

Vitabu vingine ni vyeusi Na vinatereza,
Magamba yake yanametameta
Kama nyoka wa hatari
Aliyejizinga juu ya mti.

*8.The papers on my husband's*
*desk*
*Coil threatenly*
*Like the giant forest climbers,*
*Like the kituba tree*
*That squeezes other trees to*
*death;*
*Some stand up,*
*Others lie on their backs,*
*They are interlocked*
*Like the legs of the youths*
*At the orak dance,*
*Like the legs of the planks*
*Of the goggo fence,*
*They are tightly interlocked.*

8.Makaratasiyaliyo juu
Ya meza ya mume wangu
Yanakunjika ovyo
Kama ile mimea mikubwa
Inayotambaa juu ya miti
Kama mkweme Unaonyonga miti mingine
Mpaka ikafa
Vingine vimesimama,
Vingine vimelala chali;
Vimeshonana
kama miguu ya vijana
Walio katika ngoma,
Kama vishina vya mbao
Zilizojengewa uwigo.
Vimefungana kama mashina.

*19.He himself was agreat chief*
*Well beloved by his people.*
*At the otole dance*
*He was right in the middle*
*Completely surroundedby his host*
*Like the termite queen mother,*
*But you could spot him*
*By his huge head-gear*
*Waving like a field of flowering*
*Sugar-cane!*

19.Yeye mwenyewe amlikuwa chifu
mkubwa,
Aliyependwa sana na watu wake.
Katika ngoma ya *otole*
Alicheza katikati kabisa
Akizungukwa na wenyeji wake
Kama malkia wa mchwa
Lakini aliwez kutambulika
Kwa kilemba chake kikubwa
Kikitinga kama shamba la miwa
Inayotoa maua!

*21O my clansmen,*
*Let us all cry together!*
*Come,*
*Let us mourn the death of my husband,*
*The death of a Prince*
*The ash that was produced*
*By a great fire!*
*O, this homesteadis utterly dead,*
*Close the gates*
*With lucari thorns,*
*For the Prince*
*The heir to the Stool is lost!*
*And all the young men*
*Have perished in the wilderness!*
*And the fame of this homestead*
*That once blazed like a wild fire*
*In a moonless night*
*Is now like the last breaths*
*Of adying old man!*

21.E ndugu zangu
Njooni tulie pamoja,
Njooni tuomboleze
Kifo cha nune wangu,
Kifo cha mwana-mfalme,
Majivu yaliyotengenezwa
Kutoka katika moto mkubwa!
O nyumba hii imekufa kabisa.
Fungeni milango
Kwa miiba ya lacari;
Maana mwana-mfalme
Mrithi wa kiti kile
Amepotea!
Na vijana wote
Wameteketea nyikani!
Na sifa ya nyumba hii
Ambayo zamani iliaka
Kama moto wa mbugani
Katika usiku wa giza
Usiokuwa na mwezi,
Sasa hivi kama pumzi za mwisho
Za mzee anayekufa!

*22.There is not one single true son left,*
*The entire village*
*Has fallen into the hands*
*Of war captives and slaves!*
*Perhaps one of our boys*
*Escaped with his life!*
*Perhaps he is hiding in the bush*
*Waiting for the ssun to set!*

22.Hakuna hata mmoja
Mwana halisi aliyebaki.
Kijiji kizima kimeingia
Mikononi mwa wateka na watumwa.
Pengine mvulana wetu mmoja
Ametoroka na maisha yake,
Pengine anajificha vichakani
Kungojea jua lizame!

*23.Bile burns my inside!*
*I feel like vomiting!*

23.Nyongo yaniunguza ndani,
Naona kichefuchefu,
Nataka kutapika.

*24.For all young men*
*Were finished in the forest*
*Their manhood was finished*
*In the classrooms,*
*Their testicles*
*Were smashed With large books!*

24Maana vijana wetu wote
Walimalizika msituni,
Uwanaume wao ulimalizika
Madarasani.
Makende yao yamepasuliwa
Na mabuku makubwa!

**Kiambatisho M**

| | |
|---|---|
| ***Let them Prepare*** | **Hebu Wakutengenezee** |
| ***the Malakwang' Dish*** | **Chakula cha malakwang** |
| *3.Let them prepare the Malakwang' dish* | 3.Hebu wakutengenezee |
| *Eat the roos of lurono* | Chakula cha Malakwang. |
| *And the roots of your tongue* | Kula mizizi ya lurono |
| *Will be loosened* | Na mizizi ya ulimi wako |
| *When they have prepared lukut,* | Italegea. |
| *Eat it,* | Watakapopika lukut |
| *It will strengthen your knee!* | Wewe kula, |
| | Itaimarisha goti lako! |
| | |
| *2.Chew  the roots of Ombwoye* | 2.Tafuna mizizi ya *omwombye* |
| *It is very bitter* | Ni michungu mno |
| *But it will clear your throat.* | Lakini itasafisha koo lako. |
| | |
| *6.Bring the ripe seeds of labbika* | 6.Leteni mbegu za *labikka* |
| *And scratch Ocol's eye balls* | Mbegu zilizokomaa |
| *And remove the blood* | Mkwangue macho ya Ocol |
| *That has clotted there,* | Mkaondoa damu |
| *Put the rhino-horn powder* | Iliyoganda machoni; |
| *In his eyes!* | Tieni unga wa pembe la kifaru |
| *Let it stab away* | Machoni mwake |
| *The pus that blocks his eyes!* | Likateke ule usaha |
| | Tieni unga wa pembe la kifaru |
| | Machoni mwake |
| | Likateke ule usaha |
| | Unaoziba macho yake! |
| | |
| *7.The blindness you got in the  library* | 7.Uvimbe ulioziba koo lako |
| *Will be removed by the diviner!* | Utaponyeshwa na majani machanga |
| *The swelling that has blocked your throught* | Ya mti wa *lapena*. |
| *Will be treated with the shoots of lapena* | Tafuna majani machanga |

*Chew the shoots of lapena and olim,*
*Put some salt in the shoots*
*And swallow the bitter green juice!*

Ya *lapena* na *olim*;
Tia chumvi kidogo
Halafu meza mate
Ya uchungu
Ya rangi ya kijani!

*13.When you compared me*
*With the silly ojuu insects*
*That sit on the beer pot,*
*You were abusing your entire people.*

13Ulikuwa ukiwatukana
Babu zako na bibi zako,
Baba yako na mama yako.
Ulipokuwa uukinilinganisha

*14. When you took the axe*
*And threatened to cut the Okango*
*That grows on the ancestral shrine*
*You were threatening*
*to cut yourself loose.*
*To be tossed to the winds*
*This way and that way*
*Like the dead dry leaves*
*Of the olam tree*
*In thee dry season.*

14.Uliposhika shoka
Kukata mti ule *okango*.
Ulioota makaburini,
Ulikuwa unataka kukata
Nanga yako mwenyewe.

*16.Let me play and sing*
*The song of my youth:*
*She has taken the road to Nimule*
*She will come back tomorrow*
*His eyes are fixed on the road*
*Saying, Bring Alyeka to me*
*If I may see her*
*The daughter of the bull.*
*Has stayed away too long*
*His eyes are fixed on the road*

16.Ngoja nipige na kuimba
Wimbo wa ujana wangu:
*AmeshikanjiakwendaNimule*
*Atarudikesho*.
*Macho yake yamekaza kutazama njia*
*hiyo*
*Akisema niletee alyeka Nipate kumwona*
*Binti ya dume*
*Amekaa muda mrefu mno*
*Macho yake yamekaza Kutazama njia hiyo.*

*17.All I ask*
*Is that you give me one chance,*
*Let me praise you*
*Son of the chief!*
*Tie ankle bells on my legs,*
*Bring lacucuku rattles*
*And tie them on my legs.*
*Call the nanga players*
*And let them play*
*And let them sing,*

17.Ninaloomba tu
Ni kwamba uniruhusuMara moja tu
Nipate kukusifu
Mwana wa chifu
Funga njuga miguuni mwangu
Lete na *lacucuku*
Misewe inayovuma,
Ifunge miguuni mwangu
Waite wachezaji wa *nanga*
Wambie wapige ngoma
Wambie waimbe,

*18.Let me dance before you,*
*My love,*
*Let me show you*
*The wealth in your house,*
*Ocol my husband,*
*Son of the Bull,*
*Let no one uproot the Pumpkin.*

18.Uone nikuchezee ngoma,
Mpenzi wangu,
Nikuonyeshe mali
Iliyomo kaika nyumba yako.
Ocol, mume wangu
Mwana wa Dume
Asije mtu
Akaung’oa Mboga